Alhamisi Desemba 19, 2019 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

# Nipashe

ISSN 0856 • Na. 0580105

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

The Guardian digital nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710 LIKE & FOLLOW US

Albinism Hotline

- Jifunze kuhusu Ualbino
- Toa taarifa za nia ovu dhidi ya wenye Ualbino

0800 75 00 50

Piga simu bure

UNDER THE SAME SUN ARIGATOU INTERNATIONAL GNRC CEFA

215544702



## Magufuli asisitiza hataongeza hata siku moja kubakia Ikulu

UKURASA 2

# Viongozi, wanafunzi wa UDSM watimuliwa

• **Ni** baada ya kutishia kuandamana kudai fedha za mikopo...*Endelea uk.2*



## Mvua yaua wawili Dar

UKURASA 3

UKURASA 3

Mwenyekiti wa Chadema, Freeman Mbowe, akihutubia wanachama wa chama hicho katika mkutano wa kuchagua viongozi wakuu wa ngazi mbalimbali jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**



Scan Hapa

Fungua App ya QR Code Reader kisha scan kupakua APP yetu

Google Play App Store

# Lissu aomba Chadema imsaidie kurejea nchini

**MICHEZO** NCHIMBI AZUA UTATA KUSAJILIWA YANGA UK.32 **MAONI, KATUNI** UK.6

# Viongozi, wanafunzi wa UDSM watimuliwa

**Na Salome Kitomari**

WANAFUNZI watano wakiwamo viongozi wa Serikali ya Wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (DARUSO), wamesimamishwa masomo kwa madai ya kukiuka sheria ndogo ndogo za chuo.

Uamuzi huo umefikiwa baada ya serikali ya wanafunzi hao kutangaza mgomo kutokana na Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu (HESLB) kushindwa kuwapa mikopo kama inavyotakiwa, jambo lililosababisha wanafunzi wanaoishi kwa kutegemea mikopo hiyo kupata shida.

Juzi Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Joyce Ndalichako, alitoa saa 24 kwa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, kueleza hatua walizochukua dhidi ya wanafunzi waliotoa tamko kinyume cha taratibu za chuo zinazowazuia kufanya maandamano.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa jana na Makamu Mkuu wa Chuo, Prof. William Anangisye, wanafunzi hao wamekiuka sheria ndogo,ndogo chini ya vifungu 4.1 (i) na (iii) 4.2 (viii) (a&b), (xii), (xxiv) na (xxvi) na kifungu cha 9.

Aliwataja wanafunzi hao kuwa ni Hamis Maulid, Malekela Brighton, Milanga Hassan na Mariki Godson wote walianza chuo mwaka 2017 na Ititi Musa aliyeanza mwaka 2016.

"Tumechunguza kwa kina na kubaini wanafunzi watano wamekiuka sheria... uongozi wa chuo unaendelea kuchunguza na kufuatilia mienendo ya wanafunzi wote na kila atakayebainika kuhusika kwa namna moja ua nyingine atachukuliwa hatua stahiki za kinidhamu na kisheria," alibainisha.

Hivi karibuni, serikali ya wanafunzi wa UDSM walitoa saa 72 kwa HESLB, kutekeleza mambo manne ambayo ni kutoa mikopo kwa wanafunzi waliokaa chuoni toka kimefunguliwa bila fedha

INAENDELEA UK. 8



Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu (Uwekezaji), Angella Kairuki, akiongozana na Mkurugenzi wa SBC Pepsi, Avinash Jha (wa kwanza kushoto), wakati waziri alipotembelea kiwanda hicho, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Magufuli asisitiza hataongeza hata siku moja kubakia Ikulu

**Na Salome Kitomari**

RAIS John Magufuli amerudia kauli yake ya kutokuwa na mpango wa kuongeza hata siku moja wa kuwa madarakani kwa kutumikia nchi kwa mujibu wa Katiba na kuondoka.

Alitoa kauli hiyo wilayani Chato mkoani Geita jana, wakati akizungumza na wananchi kabla ya kuzindua majengo ya Shule ya Msingi Chato na visima vya maji vilivyojengwa kwa ufadhili wa serikali ya Falme za Kiarabu kwa harama ya Sh. milioni 346.

"Nimekuwa nikisisitiza kuwa nitazingatia Katiba na sheria na ndiyo maana sitegemei kuongeza hata siku moja nikishamaliza muda wangu," alisisitiza.

Alisema muda aliopewa kwa mujibu wa Katiba ndiyo muda ambao atakuwa amepewa na Mwenyezi Mungu kuwatumikiwa Watanzania.

"Nimeona nilizungumze hili kwa uwazi kabisa ili wale wanaofikiria kuongeza ongeza yale mawazo yawatoke kabisa, Watanzania milioni 55 kila mmoja anaweza kwa msaada wa Mwenyezi Mungu, hata mimi ninayaweza haya kwa msaada wa Mwenyezi Mungu, najua maendeleo tunayoyapata si nguvu zangu ni nguvu za Mungu kupitia kwangu ili nikalete maendeleo ya Watanzania," alibainisha.

"Unapoona tunajenga daraja la Busisi si nguvu zangu, kununua ndege 11

INAENDELEA UK. 8


bgtl

**BEST GROUP (T) LIMITED**

Debts collectors, Auctioneer, Commission Agent, Court Broker & Legal Consultant

**TANGAZO LA MNADA WA HADHARA(MARUDIO).**

Kwa idhini tuliyopewa na **MAENDELEO BANK PLC** tutauza kwa **MNADA WA HADHARA** dhamana za mikopo ya mdaiwa/mdhamini ambazo ni **NYUMBA KWA AJILI YA MAKAZI na GARI.** Mnada utafanyika kuanzia saa 4:00 asubuhi na kuendelea mahali dhamana ilipo kama inavyoonyesha hapo chini.

| NA. | JINA LA MDAIWA | DHAMANA MAHALI ILIPO | TAREHE YA MNADA |
|---|---|---|---|
| 1. | HUSSEIN AMEIR MZIYA | Nyumba ya Makazi yenye Hati ya umiliki Na.90542, kiwanja Na.228, Kitalu " C" eneo la Kilimanjaro Mkoa wa Morogoro iliyopo kwa jina la HUSSEIN AMEIR MZIYA. | 21/12/2019 |
| 2 | HUSSEIN AMEIR MZIYA | Gari aina ya BMW -735L yenye namba ya usajili T 502 DDF | 22/12/2019 |

**MASHARTI YA MNADA**

1. Dhamana itauzwa kama ilivyo.
2. Mnunuzi atatakiwa kulipa siku ya mnada asilimia 25% ya bei iliyofikiwa.
3. Malipo ya asilimia 75% yalipwe ndani ya siku kumi na nne (14). Kukamilisha malipo yote. Kushindwa kufanya hiyo mnunuzi atakuwa amepoteza malipo yote ya awali ya asilimia 25%, na mnada kurudiwa.
4. Gharama za kuona, kukagua, kuhamisha umiliki, kumtoa mdaiwa/mpangaji na zingine zinazoambatana na hilo ni jukumu la mnunuzi.

**Kwa Taarifa zaidi wasiliana na:** **AU**

**Mkurugezi Mtendaji**
**Best Group (T) LTD**
**Alli Hassan Mwinyi Road.**
**Green Acres Buliding, 2nd Floor.**
**P.O. BOX 1088**
**DAR ES SALAAM**
**MOBILE + 255 715-363537/+ 255 766-309913**

**Mkurugenzi Mtendaji**
**MAENDELEO BANK PLC**
**HQ,Luther House,**
**Sokoine Drive,**
**P.O. BOX 216**
**DAR ES SALAAM**
**el: +255-222110518**



DRC DANISH REFUGEE COUNCIL

**TANGAZO LA ZABUNI**

SHIRIKA LA KUHUDUMIA WAKIMBIZI LA DANISHI LINATARAJIA KUAJIRI MTOA HUDUMA YA UKAGUZI WA HESABU ZA FEDHA KWA MWAKA WA FEDHA 2018.

NYARAKA ZA KUJAZIA MAPENDEKEZO NA BEI ZINAPATIKANA KATIKA OFISI ZA DANISHI KIBONDO KUANZIA TAREHE 18.12.2019 HADI TAREHE 24.12.2019 SIKU ZA KAZI SAA 2:00 ASUBUHI MPAKA SAA 10:30 JIONI. TUNAPATIKANA BARABARA YA IRC KIBONDO.

**KWA MAWASILIANO ZAIDI PIGA 0623529029 au barua pepe steward.mbonalibaye@drc.ngo**

**ZABUNI ZITAFUNGULIWA HADHARANI TAREHE 27.12.2019 SAA 4:00 ASUBUHI OFISI ZA DANISHI KIBONDO NA KAMATI YA KUFUNGUA ZABUNI LA DANISHI.**

**UNAWEZA KURUDISHA ZABUNI KUPITIA rfq.tza@drc.ngo**

**AU KULETA MOJAKWA MOJA OFISINI VINGINEVYO NI BATILI.**

215559202


# ...Akerwa msongamano wa wafungwa

**Na Salome Kitomari**

RAIS John Magufuli, amevitaka vyombo vya usalama nchini kushirikiana kwa karibu ili kupunguza msongamano wa wafungwa na mahabusi kwenye mahakama nchini.

Aidha, amesema ni aibu kwa magereza kuwa na idadi kubwa ya mahabusi kuliko wafungwa, jambo linaloonyesha kuwa bado vyombo hivyo havijashirikiana vyema katika kumaliza kesi na kupunguza msongamano.

Rais Magufuli aliyasema hayo jana, wakati akizungumza na wananchi wa Chato kabla ya kuzindua jengo la Mahakama ya Wilaya na jengo la Zimamoto.

Alisema vyombo vyote vya kutoa haki lazima vishirikiane katika kuhakikisha haki za Watanzania zinapatikana, na kwamba wakati mwingine kesi

INAENDELEA UK. 8

## HABARI KITAIFA



Rais John Magufuli akiwa na Jaji Mkuu wa Tanzania, Profesa Ibrahim Juma, Rais wa Taasisi ya Al-Hikma Foundation, Sheikh Shariff Abdulqadir, pamoja na viongozi wengine wa dini wa Mkoa wa Geita, wakifunua pazia kuashiria uwekaji wa jiwe la msingi la ujenzi wa Msikiti Mkuu wa Wilaya ya Chato wa Al Huda mjini Chato jana. Msikiti huo utakaokuwa na uwezo wa kuchukua waumini 3,000 kwa ndani na 6,000 kwa nje kwa wakati mmoja, unajengwa kwa ufadhili wa Taasisi ya Al-Hikma Foundation kwa thamani ya Sh. bil. 1.6. **PICHA: IKULU**

# Lissu aiomba Chadema imsaidie kurejea nchini

**Na Enock Charles**

MWANASHERIA Mkuu wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema), Tundu Lissu, amekiomba chama hicho kimsaidie kurejea nyumbani haraka ili aendelee na majukumu ya kukijenga.

Akizungumza kwa njia ya video na mkutano mkuu wa chama hicho uliofanyika jana jijini Dar es Salaam, Lissu alidai kwa sasa ni mzima wa afya na yuko tayari kurejea nchini.

Kabla Lissu hajaanza kuzungumza na wajumbe wa mkutano huo, Katibu Mkuu wa Chadema, Dk.Vicent Mashinji, alidai mtaalamu huyo wa sheria yuko mjini Brussels, Ubelgiji alikokuwa amekwenda kwa ajili ya matibabu ya kibingwa baada ya mwili wake kuharibiwa na risasi alizopigwa Septemba 2017.

"Naombeni mshirikiane, mfanye kila linalowezekana niweze kurudi nyumbani haraka iwezekanavyo," Lissu aliuomba mkutano huo.

Ingawa Lissu hakuweka wazi aina ya msaada anaohitaji kutoka kwa chama hicho ili kurudi nyumbani, lakini hivi karibuni akizungumza na vyombo vya habari vya kimataifa, alidai ameshindwa kurejea nchini kwa sababu za kiusalama.

Lissu ambaye amekuwa nje ya nchi kwa matibabu kwa miaka mawili sasa, katika moja ya mahojiano yake hivi karibuni, alidai kuwa kurejea kwake nchini kutategemea na kuhakikishiwa usalama wake kutoka kwa viongozi wa chama chake.

Septemba 7, 2017, mbunge huyo wa zamani wa Singida Mashariki, alishambuliwa kwa kupigwa risasi na watu wasiojulikana wakati anajiandaa kushuka kwenye gari nyumbani kwake mjini Dodoma muda

INAENDELEA UK.26

# Mvua yaua wawili Dar

**Na Maulid Mmbaga**

MVUA kubwa iliyonyesha kwa takriban saa tano Dar es Salaam juzi, imesababisha vifo vya watu wawili na kuharibu miundombinu ya jiji hilo la kibiashara.

Akizungumzia athari za mvua hiyo jana, Kamanda wa Polisi Kanda maalum ya Dar es Salaam, Lazaro Mambosasa, alithibitisha kutokea kwa vifo hivyo.

Alidai mmoja wa waliokufa maji, alikuwa anajaribu kuokoa friji lililokuwa linaelea juu ya maji eneo la Jangwani na mwingine alikutwa akiwa anaelea juu ya maji akiwa ameshapoteza maisha.

Kamanda Mambosasa aliwataka wakazi wa jiji hilo kuchukua tahadhari kuhusu mvua inayoendelea kunyesha ili kujiepusha na madhara ya mafuriko.

"Natoa rai kwa wakazi wa Dar es Salaam kuwa makini na watoto na mali zao kutokana na mvua inayonyesha, pia walioko mabondeni waondoke ili kulinda usalama wao," alitahadharisha.

Mbali na vifo hivyo, mvua hiyo pia ilisababisha baadhi ya makazi ya watu kuharibika, huku kukisitishwa kwa muda kwa huduma ya usafiri wa daladala na mabasi yaendayo haraka kwenye barabara zinazokatisha eneo la Jangwani.

Salimu Iddi, dereva wa daladala, akizungumzia madhara ya mvua hiyo jana, alisema imewaathiri kutokana na kusimamisha huduma ya usafirishaji abiria ambayo ndiyo kazi wanayoitegemea kujipatia kipato.

"Barabara zilizoharibiwa na maji zifanyiwe ukarabati ili kuruhusu shughuli mbalimbali kuendelea," alishauri baada ya kuona baadhi ya barabara zilizoathiriwa na mvua hiyo kuwa zimefungwa.

# UVCCM yaanzia Iringa kufufua vyuo vyake

**Na Mwandishi Wetu**

KATIBU Mkuu wa CCM Dk. Bashiru Ally, ametangaza bodi ya mpito ya kushauri namna ya kuendesha vyuo vya Umoja wa Vijana wa CCM (UVCCM) vinavyofufuliwa, wakati utaratibu wa kusimamia vyuo hivyo ukiandaliwa.

Dk Bashiru alisema bodi hiyo itasaidia kusimamia vyuo vya UVCCM vinavyofufuliwa kama Ihemi na Kibaha na kuwashauri vijana wanaopata mafunzo katika taasisi hizo kufikiria kujiajiri.

Alisema hayo jana wakati wa uzinduzi wa chuo cha mafunzo Ihemi pamoja na majengo na miradi ya maendeleo inayoanzishwa chuoni hapo.

"Mwenyekiti Bodi ni Mwenyekiti wa CCM Mkoa wa Iringa, atasaidiwa na atakayekuwa mkuu wa chuo na atashika pia nafasi ya katibu wa bodi,wajumbe wengine ni mlezi wa chama atakayewakilisha kamati kuu kwenye bodi hiyo".

Wengine Katibu Mkuu alisema ni pamoja na mjumbe wa NEC Iringa na makatibu wa jumuiya za chama wa mikoa na kuwashauri wateua wajumbe wenye uwezo.

INAENDELEA UK.26

SHIRIKA LA UMEME TANZANIA

TANESCO
We light up your life

TAARIFA KWA UMMA

Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) lina watangazia wateja wake wote zikiwemo Taasisi za Serikali na binafsi, Mashirika ya umma, Viwanda na watu binafsi wenye madeni ya bili za umeme kuwa;

TANESCO inaendesha zoezi maalum la kusitisha huduma ya umeme kwa wateja wote wanaodaiwa bili za umeme.

Wateja wote wenye madeni wanatakiwa kulipa bili zao haraka ili kuepuka adha ya kusitishiwa huduma ya umeme katika msimu wa sikukuu.

TANESCO HAITATOA TAARIFA NYINGINE ZAIDI YA TANGAZO HILI.

Imetolewa Na:
OFISI YA UHUSIANO
TANESCO MAKAO MAKUU
18 Disemba2019

# Mwenyekiti Baraza Ardhi ahukumiwa kwa rushwa

**Na Khadija Kalil,** MKURANGA

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Wilaya ya Mkuranga mkoani Pwani, imemhukumu kifungo cha miaka mitatu au kulipa faini ya Sh. 500,000 aliyekua Mwenyekiti wa Baraza la la Ardhi Kata ya Tambani, Mussa Awilo Mataka, baada yakukutwa na makosa ya kushawishi na kuomba rushwa.

Mataka ametiwa hatiani kwa kupokea kiasi cha Sh. 100,000 kinyume cha kifungu cha 15(1) (a) cha Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa Na. 11 ya mwaka 2007.

Akisoma mashtaka mbele ya Hakimu wa Wilaya ya Mkuranga, Peter Mrosso, Mwendesha Mashtaka wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru), Euphrazia Kakiko, alidai kuwa kupitia kesi ya jinai Namba 2 ya mwaka 2019, kati ya Januari 20 na 24, mwaka 2018 mshtakiwa alitenda kosa la kushawishi kupewa rushwa ya kiasi cha Sh. 500,000.

Alidai zaidi kuwa Januari 24, 2019, alipokea rushwa ya kiasi cha Sh. 100, 0000 kupitia njia ya simu kutoka kwa mtoa taarifa ili amfanyie upendeleo katika shauri la ardhi lililokuwa linaendelea kusikilizwa na mshtakiwa, kitendo ambacho ambalo ni kosa kisheria na kinyume cha kifungu cha 15 (1) (a) cha Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa, Namba 11 ya mwaka 2007.

Hata hivyo, mshtakiwa alikwepa adhabu ya kwenda jela kwa alilipa faini hiyo kama mahakama ilivyoelekeza.

Akizungumzia hukumu hiyo, Kamanda wa Takukuru Mkoa wa Pwani, Suzana Raymond, alitoa wito kwa viongozi wote kutumia dhamana waliyopewa kwa kuwatumikia wananchi kwa kutenda haki na kuwajibika katika nafasi zao kwa kufuata sheria, kanuni na taratibu ili kuepuka vitendo vya rushwa.

Kamanda huyo alisema kwamba rushwa ndiyo msingi wa huduma mbovu kwa jamii.



Mafundi wakimwaga zege kwenye barabara inayotoka ITV kuelekea nyumba za maofisa wa serikali. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**




# Utafiti wafagilia vipimo vipya VVU kwa watoto

**Na Mwandishi wetu,** MBEYA

UTAFITI wa vipimo vya awali vya Virusi vya Ukimwi (VVU) kwa watoto wachanga waliozaliwa na kinamama wenye maambukizi, umeonyesha kuwa vipimo vipya vimefanya vizuri kwa asilimia 100 kubaini maambukizo ndani ya saa mbili.

Utafiti huo ujulikanao kwa jina la 'BABY', uliofanywa na Taasisi ya Taifa ya Utafiti wa Magonjwa ya Binadamu (NIMR) unaofanywa kwa kipimo cha Early Infant Diagnosis(EID) kwa kutumia mashine za GeneXpert .

Awali, upimaji wa kawaida ulikuwa unafanywa kwa watoto wachanga wenye wiki 4 hadi 6 na majibu yake yalikuwa yakichukua wiki mbili.

Mkurugenzi (NIMR) Mbeya, Dk. Nyanda Ntinginya, aliwaambia wanahabari wa kampeni ya 'Tumeboresha Sekta ya Afya' kuangalia mafanikio ya miaka minne ya serikali ya awamu ya tano kuwa kipimo hicho kwa mtoto anapozaliwa tu kinachukua siku mbili kutoa majibu.

Alisema utafiti huo uliofanyika Julai 2015 hadi Novemba 2016 kwa NIMR Mbeya kwa kushirikiana na Chuo Kikuu cha Munich cha Ujerumani, ulilenga kutathimini vipimo vya awali vya VVU kwa watoto wachanga ambao wazazi wao wameathirika.

"Huu utafiti ulilenga kufanya tathmini ya vipimo vya awali vya VVU katika kituo cha kutolea huduma na vipimo vilifanywa na wauguzi tofauti na upimaji wa sasa ambao huhitaji wataalamu wa maabara na hivyo kuhitaji usafirishaji wa sampuli za damu kwenda maabara ya kanda au ya mkoa," alisema.

Alisema matokeo ya utafiti yameonyesha vipimo hivyo vilifanya vizuri kwa asilimia 100, na vinatoa majibu ndani ya saa mbili tu, hivyo mgonjwa kupewa majibu yake siku hiyo hiyo ukilinganisha na upimaji wa kawaida ambapo huchukua wiki mbili au zaidi kupata majibu.

"Upimaji wa VVU wa awali kwa watoto wachanga umejumuishwa katika mwongozo wa sasa wa utoaji wa huduma za VVU nchini," alisema.

Hata hivyo, alisema matokeo ya utafiti huo uliofanywa nchini Tanzania, Afrika Kusini na Msumbiji yamepelekwa Shirika la Afya Duniani (WHO) kutoa miongozo ya upimaji wa VVU kwa watoto hao katika mwongozo wa utoaji wa huduma za VVU wa mwaka 2016.

"Moja ya miongozo hii ilikuwa ni kutumia vipimo vya upimaji vya PoC pale vinapopatikana ili kurahisisha upimaji wa VVU," alisema.

**CHANJO YA UKIMWI**

Akizungumzia kuhusu chanjo ya Ukimwi, Mkurugenzi huyo alisema kwa kipindi cha miaka minne NIMR Mbeya imefanikiwa kufanya utafiti mbalimbali wa chanjo ya VVU, hivyo kuiwezeza Tanzania kuwa miongoni mwa nchi chache duniani zilizoshiriki katika tafiti kubwa tatu za majaribio ya chanjo.

"Majaribio hayo yamefanywa kwa kushirikiana na Mtandao wa Chanjo za Ukimwi Duniani na Serikali ya Marekani, utafiti huu unalenga kuangalia usalama wa chanjo katika matumizi ya binadamu kuangalia ubora wa chanjo katika kusisimua kinga ya mwili dhidi ya VVU," alisema.

Aliongeza kuwa utafiti huo umeiwezesha NIMR kushirikiana na wanasayansi wengine duniani kushiriki kikamilifu katika utafutaji wa chanjo iliyo bora ya VVU, na bado tafiti zinaendelea.

## UNDP: Wanawake wasuasua kipato

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

SHIRIKA la Maendeleo la Umoja wa Mataifa (UNDP), limetoa ripoti ya maendeleo ya watu kwa mwaka 2019, ikionesha wanawake kutopiga hatua katika pato la mtu mmoja mmoja pamoja na kuwa nyuma kielimu ukilinganisha na wanaume.

Mratibu wa Ripoti za Maendeleo ya Binadamu, Amon Manyama, akitoa taarifa ya ripoti hiyo alisema ripoti ya mwaka 2018 inaonyesha pato la mwanamke kwa siku ni 2,436, huku mwanaume wakiwa ni 3,175 wakati kwa upande wa elimu ya msingi inaonyesha wanaume wameongezeka kuandikishwa kwa asilimia 8.0, huku wanawake ni asilimia 5.6.

Akizindua ripoti hiyo ya maendeleo ya watu jijini Dodoma jana, Katibu Mkuu Wizara ya Maliasili na Utalii, Prof. Adolf Mkenda, alisema ripoti imeonyesha kwa upande wa wanafunzi wanaomaliza elimu ya sekondari imeongezeka kwa kiasi kikubwa kwa wanaume kuliko wanawake, ambapo inaonyesha wanawake imeongezeka kwa asilimia 11.9 na wanaume asilimia 16.9. "Bado tunahaja ya kuweka usawa na lengo la kutoa ripoti hii ni kuweka wazi watu waone nafasi iliyopo kati ya wanawake na wanaume mfano, bungeni viti vya wanawake ni asilimia 37 wakati tunahitaji hamsini kwa hamsini, hivyo bado tunahitaji nguvu ya ziada ili tuweze kupiga hatua." Alisema.

Mkuu wa Mkoa wa Simiyu, Anthony Mtaka, alisema ripoti inaonyesha wanafunzi wanaomaliza elimu ya vyuo vikuu imepanda na changamoto ni uhaba wa ajira.

Mtaka alisema kuna haja ya kufanya mapinduzi ya mitaala ya elimu ili iendane na kasi kuhakikisha vijana wanaomaliza elimu ya juu na sekondari wanapata ajira na kupunguza mzigo wa utegemezi.

"Mfano China walifanya mapinduzi kwa kugeuza vyuo vikuu 600 kuwa vyuo vya ufundi... naamini hata Tanzania kuna haja ya kufanya mapinduzi hayo ili kuendana na kasi ya Rais ya kufikia uchumi wa kati ifikapo 2025," alisema.

# Kabendera, DPP bado kukubaliana

**Na Hellen Mwango**

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Kisutu, jijini Dar es Salaam imeelezwa kwamba mazungumzo kuhusu barua ya kukiri makosa kati ya mwandishi wa habari za uchunguzi, Erick Kabendera, na Mkurugenzi wa Mashtaka (DPP) dhidi ya kesi ya uhujumu uchumi inayokabili mwanahabari huyo, yanaendelea.

Kesi ilitajwa jana mbele ya Hakimu Mkazi Mwandamizi, Janeth Mtega.

Wakili wa Serikali Mwandamizi, Wankyo Simon, alidai kuwa kesi hiyo ilipangwa kwa ajili ya kutajwa, na kwamba upelelezi wake haujakamilika.

Hata hivyo, Wakili wa Utetezi, Jebra Kambole, alidai kuwa wanaendelea na mazungumzo na DPP baada ya kumwandikia barua ya kukiri na kuomba msamaha.

Alidai kuwa mazungumzo hayo yatakapokamilika wataijulisha mahakama.

Hakimu Mtega alisema kesi hiyo itaendelea Januari 2, 2020 itakapotajwa na mshtakiwa ataendelea kukaa mahabusu.

Kabendera anadaiwa kupanga na kushirikiana na genge la uhalifu na shtaka la tatu ni la kukwepa kodi zaidi ya Sh. milioni 173.

Katika kesi ya msingi, ilidaiwa siku na mahali pasipofahamika, mshtakiwa alijihusisha na genge la uhalifu.

Alidai katika tarehe tofauti kati ya Januari mwaka 2015 na Julai mwaka 2019, alitenda kosa la kutoa msaada kwa genge la uhalifu kwa nia ya kujipatia maslahi.

Katika shtaka la pili, Kabendera anakabiliwa na shtaka la ukwepaji kodi, zaidi ya Sh. 173,247,047.02.

Kabendera anadaiwa katika tarehe tofauti kati ya Januari 2015 na Julai 19, 2019, alishindwa kulipa kodi kiasi cha Sh. 173,247,047.02.

Katika shtaka la tatu, Kabendera anadaiwa kati ya Januari 2015 na Julai 2019, katika maeneo mbalimbali ya Jiji la Dar es Salaam, alitakatisha fedha kiasi cha Sh. 173,247,047.02.

DERM GROUP

NOTICE OF HOLIDAY SEASON CLOSURE

Derm Group wishes to inform its esteemed clients and business partners that our offices will be closed during the festive season with effect from Saturday 21st December 2019.

Business will resume on Monday 06th January 2020.

Our site operations in Arusha, Dar es salaam, Dodoma, Mara, Mtwara, Mwanza, Tanga, Bagamoyo and Zanzibar shall not be affected by this closure.

Any inconveniences caused is highly regretted.

We would like to thank all our clients and business partners in general for their continued patronage of our services throughout the year 2020.







115559702

DERM ELECTRICS (T) LTD
Electrical, HVAC, Security, ICT Co tractors
SKYLINE PROPERTIES LTD
Derm Elevators LTD
DTsmart

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Tutaachana lini na mafuriko haya?

**MAENEO** mengi ya Dar es Salaam yapo kwenye hatari ya kuzama kwenye mafuriko na kila mara serikali imekuwa ikipiga mbiu ya kuwahimiza wananchi wanaoishi mabondeni wahame.

Sheria ya Mazingira ya Mwaka 2004 inakataza kujenga mtoni au ufukweni na kuagiza mwenye kujenga karibu na mto aweke makazi yake umbali wa mita 60 kutoka mtoni bila kujali ni mjini au kijijini.

Tunaona kuwa kukaidi sheria na maelekezo ya serikali yamekuwa sababu ya watu kutumbukia kwenye mafuriko kila mwaka na imekuwa ni jambo ambalo halitibiki.

Kama Rais John Magufuli, alivyoelekeza jana nasi tunaungana naye kusisitiza kuwa kujiokoa na mafuriko ni lazima kutii sheria za nchi na mazingira ya asili.

Anasema kuwa watu wanapotaka kujenga eneo wawasiliane na wataalamu kujua ukweli wa mazingira ya asili ikiwamo mikondo ya maji na njia zake kwani kujenga juu yake kunasababisha mafuriko.

Ni vyema kukaa mita 60 kutoka mtoni au njia ya maji na pia kuachana na mazoea ya kujenga kwenye mikondo na njia hizo kwa kuwa zimekuwa tatizo kila mwaka.

Aidha, ni kosa kuizuia mikondo na njia hizo kwa kuwa ndiyo mwanzo wa mafuriko ikizingatiwa kuwa zama hizi ni za mabadiliko ya tabianchi.

Wakazi wa Dar es Salaam wameshuhudia jinsi ambavyo maji yanavyotishia maisha na kusababisha kitisho kikubwa kwa uhai kuanzia barabarani, njia za reli, mitaani na zaidi kwa wakazi wa mabondeni.

Hili siyo suala la kupuuza tena ni wakati wa kuzingatia maelekezo ya Mamlaka ya Hali ya Hewa (TMA) na kukumbuka kila wakati kuwa taasisi hii imekuwa ikionya kuhusu mvua nyingi na kubwa zinazotarajiwa kunyesha.

Maelezo ya TMA yachukuliwe pamoja na taarifa za wataalamu wa mazingira kuhusu athari za ongezeko la joto duniani linaloambatana na mabadiliko ya tabianchi.

Kwa kuwa athari zimeanza kuonekana na maafa yanakuwa makubwa kila mwaka ni wakati wa serikali kuwashughulikia waliojenga juu ya mikondo ya maji, kufunga njia za maji kwa kuweka kifusi na majengo makubwa juu yake.

Mamlaka zinazoshughulikia mipango miji hazina budi kuamka na kufanyakazi kikamilifu kwani hakuna atakayeionea nchi huruma wakati wavunja nchi ni wananchi wenyewe.

Wakazi wa Dar es Salaam wanachoka, kuna mafuriko kila mwaka kwa kuwa wakazi wake wanakaidi kuondoka mabondeni wanaishi kwenye bonde la Mto Msimbazi sehemu za Kigogo, Jangwani, Mkwajuni, Tabata na Buguruni.

Hawa ni baadhi ya waathirika wa tatizo hilo kila mwaka. Ni wazi kuwa kila mwaka athari hizo zinawakumba wananchi ambao mbali na kufariki dunia nyumba zao zinabomolewa, vifaa kama magari, mifugo ikiwamo kuku na wanyama wadogo wanakufa. Tunaona kuwa ni wakati wa kupata suluhu ya kudumu ya tatizo hilo, pamoja na kutumia taarifa za hali ya hewa serikali inaweza kuomba msaada wa kimataifa kutoka Taasisi ya International Telecommunication Union (ITU).

ITU inaweza kufanyakazi na Mamalaka ya Mawasiliano pamoja na TMA kuweka vifaa vya kuwakumbusha wananchi na kuwapa maonyo kuhusu mafuriko.

Ujumbe wa onyo na tahadhari za mafuriko kwa wananchi limekuwa likitumiwa kwenye mataifa ya Zambia na imewezekana kuokoa maisha.

Kuna imani kwamba taarifa za onyo na tahadhari zikitolewa mapema zinaweza kuwakumbusha na kuwahamasisha wananchi kuondoka mapema mabondeni na kuhamia milimani au maeneo salama.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Meneja Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Sabato Kasika

# Kwa majanga haya, bado kinga ni bora kuliko tiba

**MOJA** ya majanga, yanayozikabili nchi mbalimbali ikiwamo Tanzania ni mafuriko yanayotokana mavua kubwa na kusababisha maafa, ikiwamo watu kupoteza maisha, mifugo na uharibifu wa mali.

Dar es Salaam ni miongoni mwa mikoa ambayo imekuwa ikikumbwa na janga la mafuriko ya mara kwa mara kila mvua zinaponyesha na wakati mwingine kusababisha maafa.

Mvua zinaweza kuleta mafuriko yanayozoa watu, magonjwa ya mlipuko, kikiwamo kipindupindu na kusababisha vifo, hivyo ili kuwa salama, ni muhimu kuepuka majanga hayo ingawa ajali haina kinga.

Pamoja na kuwapo kwa tatizo hilo, juhudi mbalimbali zimekuwa zikifanywa na viongozi wa serikali ikiwamo kuelekeza wakazi wa mabonde kuhama maeneo hayo na kwenda kuishi kwingine, kwa ajili ya usalama wao.

Kama nilivyosema kwamba, Dar es Salaam huwa inakumbwa na mafuko ya mvua mara kwa mara, lakini yale yaliyotokea mwaka 2011, ni miongoni mwa yanayojadiliwa hadi leo.

Hiyo inatokana na jinsi baadhi ya nyumba za mabondeni zilivyozama kwa sehemu kubwa, huku nyingine zikianguka kabisa na kuifanya serikali ihamishie watu katika majengo ya shule na kisha eneo la Mabwepande.

Katika mafuriko hayo, mdau wa kupinga majanga, James Mbatia, alikaririwa na vyombo vya habari akitia neno kuwa sababu kubwa ya mafuriko hayo ni kutokuwa na mipango sahihi ya miji na miundombinu mibovu. Siyo tukio hilo tu, bali mwaka 2014, watu kumi waliripotia kufariki dunia huku wengine wakikosa mahali pa kuishi, kutokana na mvua kubwa zinazonyesha jijini Dar es Salaam wakati huo.

Kamanda wa Polisi wa Kanda Maalum ya Dar es Salaam, wakati huo, Kamishna Suleiman Kova, alikaririwa na vyombo vya habri akithibitisha kutokea kwa vifo hivyo.

Tangu wakati huo kila mvua zinaponyesha, jiji la Dar es Salaam huwa linakumbwa na mafuriko ya maji, ambayo husababisha uharibifu wa mali za watu na wakati mwingine vifo.

Nikirejea kwenye hoja yangu ni kwamba, Katibu Mkuu Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Uratibu na Uwekezaji), Dorothy Mwaluko, amelielekeza Jukwaa la Taifa la Usimamizi wa Maafa nchini, kutoa ushauri wa kitaalamu unaojikita katika hatua ya kabla ya maafa kutokea na sio wakati wa maafa yanapotea.

Anasema, wakati wa kukabili majanga na maafa kunakuwapo na mipango mingi, hutekelezwa na wadau wa menejimenti ya maafa na kwa uchache wakati wa urejeshaji hali wa maafa.

Katibu Mkuu huyo anasema, mipango ya kujiandaa na kuzuia maafa, ambayo hufanyika kabla ya maafa kutokea ili kuzuia au kupunguza madhara ya maafa yatakapotokea, huwa haitekelezwi. Alitoa kauli wiki hii jijini Dodoma, alipofungua kikao cha Jukwaa la Taifa la Usimamizi wa Maafa nchini na kulitaka kutoa ushauri wa kitaalamu unaojikita katika hatua ya kabla ya maafa kutokea.

Ushauri huu ni sawa na msemo wa "kinga ni bora kuliko tiba," hivyo ni jukumu la wahusika kuliona hilo na kulifanyia kazi, ili kuepusha maafa wakati wa majanga kuliko kusubiri yatokee na kuanza kutafuta mikakati.

Analielekeza jukwaa hilo kupitia Mkakati wa Taifa wa Kupunguza Athari za Maafa, kuhakikisha inaendana na uhalisia wa hali ya majanga yanayotokea katika jamii, ili uweze kutekelezeka kwa kuweka malengo yenye uhalisia.

Msisitizo mwingine, ni kutaka mkakati huo utafsiriwe kwa Kiswahili, ili utumiwe vizuri na walengwa kuanzia ngazi ya msingi ya maafa, ambayo ni kamati za vijiji, zenye watu wanaotumia lugha hiyo.

Aidha, analitaka jukwaa hilo kuwa na ushirikiano miongoni mwa wadau wake kwa kila mdau kuainisha majukumu yake na namna, ili kujua jukumu la kila mdau na anafanya nini na kwa wakati gani na hatimaye mipango ya kuimarisha usimamizi wa maafa iwe inayotekelezeka.

"Kupunguza madhara ya maafa ni suala mtambuka lenye mchango mkubwa, katika shughuli za maendeleo.Wakati mwingine wananchi wamekuwa wakipata madhara kwa kukosa uelewa.

"Hivyo, ni vyema kila mdau kuwajibika katika majukumu yake kwa kutoa fursa ya uratibu wa usimamizi wa maafa kwa ushirikiano wa wataalamu wa fani mbalimbali," anasema Mwaluko.

## Dar tujipange na mvua

**Mhariri,**

*JIJI la Dar es Salaam ni zuri na linapendeza kwa jina la muonekano katika sura moja, huku kuna sura inayoipa mlolongo wa upungufu.*

*Umaarufu huo unatokana na ukweli unaoanzia katika simulizi ya jiji lilikoanzia, makao makuu ya mengi hasa katika kipindi kabla ya mageuzi ya sasa makao makuu ya ya kiserikali yamehamia rasmi jijini Dodoma.*

*Hata vijijini, kuna dhana iliyojengeka mtu anapotaka mambo mazuri, anapaswa aelekee Dar es Salaam, ambako kuna wastani wa asilimia 10 ya wakazi wa nchi wanaishi humo, mahitaji na ajira imepatikana huko zaidi.*

*Ingawaje kuna ukweli kwamba katika sura ya pili ya shilingi inayoonyesha kuwapo baadhi ya maeneo hali yake ya mazingira na usafi wake, iko duni mno kupitiliza.*

*Mvua nayo imetoa darasa jipya kwa jiji la Dar es Salaam. Ghafla, mji na barabara zake zimefurika na kuleta balaa na kuiweka jiji katika hali mbaya kupitiliza.*

*Tumeona namna kila kitu kilivyokuwa kibaya katika janga hilo la mvu na kuna watu hadi sasa wako katika lindi la tabu ya mvua, vyombo vya habari vinatupa ushahidi kila kukicha.*

*Niseme zaidi, wale wanaokaa mabondeni, mjadala wao sasa umekuwa jambo la kawaida kila mvua zinaponyesha wanaangukia hali mbaya na hatujutii ufumbuzi wa kudumu kuhusiana na adha yao itakoma lini.*

*Ushauri wangu ni kwa Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam na manispaa zake tano, inapaswa ikae tena kutathmini mzizi wa athari za mvua na kile kinachowezekana kukabili kupitia busara zao, kifanyiwe kazi.*

**Maskoje Shange,**
**DDar es Salaam.**

# Wafungwa wanaosamehewa wahitaji maombi na semina kabla hawajatoka




**Na Beatrice Moses**

JUMLA ya wafungwa 5,533 waliachiwa huru na Rais Dk. John Magufuli, wakati wa Maadhimisho ya Miaka 58 ya Uhuru wa Tanzania Bara yanayofanyika kila Desemba 9 ya mwaka.

Hatua ya kuachiwa huru kwa wafungwa hao ni njema, ni wazi ilipokewa kwa furaha na wahusika, ndugu jamaa na marafiki zao.

Wahenga wanasema 'penye wengi pana mengi.' Ilidhaniwa wote walipokea kwa furaha taarifa hiyo, kumbe baadhi wako kinyume. Katika Gereza la Ruanda Mkoa Mbeya, aliyekuwa mfungwa Merad Abraham aligoma kutoka kwa madai hana pa kuishi. Kumbe habari hiyo njema ilikuwa mbaya kwa mfungwa huyo ambaye badala ya kufurahia, aliomba ahamishiwe Gereza la Ukonga, jijini Dar es Salaam. Alijeruhiwa kwa jiwe usoni na kupelekwa kutibiwa kwenye zahanati ya gereza hilo.

Anaelezwa kutumikia kifungo cha miaka 30 gerezani na alitarajiwa kutoka Juni 20, mwaka 2020 na aliingia gerezani Juni 20, mwaka 2000.

Kitendo cha mfungwa huyo kimezua mjadala nchini, kupitia mitandao ya kijamii. Watu wanamjadili, huku wengine wakishangaa hasa kwa kuzingatia kigezo jela siyo mahali pa kuvutia, bali penye vizuizi, kukosekana uhuru, kwa sababu saa 24 mtu anakuwa chini ya usimamizi wa askari Magereza. Mussa Msolwa, maarufu Hitler naye aliwashangaza wengi kwani akiwa miongoni mwa wafungwa walioachiwa kwa msamaha huo. Alifikishwa Polisi mkoani Njombe, akidaiwa kukamatwa kwa kukutwa anahusika kuvunja nyumba ya kulala wageni ya Nang'ano mjini Makambako.

Mnamo siku nane zilizopita, Kamanda wa Polisi Mkoa wa Njombe, Hamisi Issa, alidai Msolwa aliienda katika nyumba hiyo ya kulala wageni, lakini alikabiliwa na tamaa alipoona fedha zimehifadhiwa na akaanza njama za wizi. Mfungwa huyo alifanikiwa kupewa msamaha na Rais na akaondoka Njombe kwenda Makambako mchana, lakini baada ya saa nane tangu atoke gerezani, anadaiwa alishawishika kufanya tukio la uvunjaji.

Kamanda Issa anasema, mtuhumiwa huyo kabla ya kutoka gerezani aliwasihi wenzake kuwa wema, huku akiomba msamaha kwa viongozi waliofika gerezani kushuhudia wafungwa wakiachiwa.

Kutokana na matukio hayo, kuna mambo muhimu ambayo yalipaswa kufanyika kwa wafungwa wote walioonekana kukidhi vigezo vya kupatiwa msamaha.

Kwanza, viongozi wa dini zote walio karibu na maeneo husika walipaswa kushirikishwa, ili wajitoe kwa hali na mali kuzungumza nao na kuwatia moyo kwa hatua hiyo na kuwaonyesha kuwa jamii inawahitaji kwa kuwa wamebadilika kuwa wema. Wafungwa, pia walitakiwa kufanyiwa maombi maalum, Wakristo na Waislamu na hata imani tofauti wakiwapo.

Jambo lingine, kulikuwapo na umuhimu wa kuandaliwa semina elekezi kwa wafungwa wenye sifa za kusamehewa, wakufunzi wawe wataalamu wa masuala ya saikolojia na ustawi wa jamii.

Naamini haya yangefanyika yangewasaidia wahusika na pia jamii, pamoja na kuzuia kuibuka kwa vitendo ambavyo vinaitisha jamii kama alivyofanya Abraham.

Mtu anapojiamini akawa na ujasiri wa kujijeruhi, je, vipi mtu mwingine wakati huo sasa anaishi uraiani? Yawezekana kabisa, akaamua kutenda kosa kwa makusudi ili akamatwe ashtakiwe na kufungwa tena jela, hivyo atakuwa ametimiza azma yake kwa namna mbaya.

Kupitia runinga Julai 16, tulishuhudia malalamiko mengi mazito kutoka kwa wafungwa gerezani, wakati Rais Dk. Magufuli alipofanya ziara kwenye Gereza la Butimba lilipo mkoani Mwanza.

Kutokana na malalamiko kuhusu hali mbaya wanayokumbana nayo wafungwa kwenye magereza ni wazi isingetarajiwa awepo ambaye atatamani kuendelea kuishi huko, ndiyo maana kuna ulinzi mkali maana wapo wengine ambao wamekuwa wakifanya majaribio ya kutoroka. Magereza yana umuhimu wake katika jamii ikiwamo hiyo ya kusaidia kurekebisha tabia za watu.

Vyombo kadhaa vya habari vimewahoji baadhi ya waliopata neema hiyo ya kuachiwa huru, miongoni ni atokaye Kaliua mkoani Tabora, amemshukuru Rais Magufuli kwa kuwasamehe bila ya kujali makosa waliyofanya.

Mfungwa huyo wa miaka 30 kwa kesi ya unyang'anyi, alitumia nafasi hiyo kuwaomba msamaha viongozi wa serikali na jamii kwa ujumla, huku akijutia kosa alilofanya.

Alibainisha kuwa, hata hivyo hajutii kukaa humo kwa miaka 20, kwa kuwa amepata nafasi ya kujifunza ufundi uashi na kumudu kujenga majengo ya nyumba mbalimbali, zikiwamo za watumishi katika Jeshi la Magereza Mkoa wa Mwanza.

Pia alikaririwa akiwapongeza viongozi wa dini, waliokuwa wakihubiri katika gereza hilo kuwa wamewajenga kiroho na kimaadili.

**WASILIANA NASI:**

TUNAKARIBISHA BARUA NA MAONI YA MSOMAJI, UNAWEZA KUTUMA KUPITIA KWA MHARIRI S.L.P. 31042, DAR ES SALAAM AU mhariri@nipashe.co.tz

**KABWELA** — Na Fadhili Mohammed



# ...Akerwa msongamano wa wafungwa

INATOKA UK. 2

hucheleweshwa na polisi kwa kutopeleka ushahidi kwa wakati.

Aidha, wapo wenye kesi ndogo wapo magerezani na kwamba watu 751 wamesamehewa, ambao walitakiwa watolewe zamani kwenye mahabusu lakini wameachwa na wengine kwa kuonewa.

"Hakimu au jaji hawezi kujua kuna mahabusi wangapi kwa sababu yeye anawategemea watakapopelekwa kwenye uamuzi, kuwa na mahabusi wengi kwenye magereza si majaji au mahakimu bali kwa hawa wengine wanaoshindwa kutekeleza wajibu wao," alisema.

"Nchi hii si ya kukaa na mahabusi wanalia wakati wengine hawana makosa, watu wanapata shida sana magerezani...polisi ofisi ya mwanasheria mkuu, hakikisheni aliyepo mahabusu ndiye anastahili, ni aibu kuwa na wafungwa wachache kuliko mahabusi.

Aidha, alisema kwa sasa kuna wafungwa 12,000 na mahabusi 17,000, na kwamba watendelea kuwapunguza zaidi, huku akitoa wito kwa vyombo vya utoaji haki kushirikiana na mahakama ili kuimarisha mfumo wa utoaji haki na kuharakisha utoaji wa haki nchini.

Alisema mahali penye mahakama wafanyabiashara na wawekezaji hujisikia huru kufanya shughuli zao kwa kuwa wanakuwa na uhakika wa shughuli zao na hivyo kuchochea maendeleo ya kiuchumi.

Alisema eneo hilo lilikuwa halina mahakama kwa kuwa washtakiwa walikuwa lazima wapelekwe Biharamulo mkoani Kagera na wakati mwingine walikaa mwaka mzima kutokana na kukosekana na usafiri.

"Wakitaka ukae huko siku nyingi watasema gari halina mafuta na gari halipo au limeharibika, hata siku ya kusikilizwa kesi hutasikilizwa, wakati mwingine mahabusu ya Biharamulo ilikiwa inajaa unapelekwa Muleba, palikuwa na changamoto kubwa sana," alisema.

Alisema mahakama nyingi zilikuwa katika hali mbaya, na kwamba nusu ya watu waliopo gerezani ni mahabusi wanaosubiri kesi kusikilizwa, na kwamba kabla ya msahama wa Desemba 9, mwaka huu, kulikuwa na watu 35,803 kati yao wafungwa 17,547 na mahabusi 18,256.

Alisema ujenzi huo utapunguza idadi ya watu hao kwenye magereza, na kwamba serikali itaendelea kushughulikia changamoto za majengo kwa kadiri ya uwezo unavyopatikana ikiwamo kuongeza watumishi.

"Mahakama ni chombo muhimu sana... wananchi wana imani nacho sana, jiepusheni na rushwa, chukueni hatua kwa watumishi wote wanaojihusisha na vitendo hivi, ujenzi huu hautakuwa na maana endapo watumishi wataendekeza rushwa na kushindwa kutoa haki kwa wananchi wanyonge," alisema.

Alisema ni mara ya kwanza kushiriki shughuli ya Jeshi la Zimamoto nchini, na kwamba kwa sasa kazi zao zimeanza kuonekana, na kwamba kwa sasa kuna mabadiliko makubwa kwa utendaji kazi wao.

"Kati ya taasisi zinazolalamikiwa ni pamoja na Jeshi la Zimamoto, ingawa wanalalamikiwa kwa makosa ambayo siyo yao mfano watu kujenga kiholela na wao kushindwa kufika eneo la tukio na kuchelewa kwa taarifa," alisema.

Aidha, Rais alizindua mradi wa visima vya maji na Shule ya Sekondari Chato, huku akiwataka watumishi wa serikali kufuatilia utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwa kutumia fedha za ndani.

# JPM asisitiza hataongeza muda

INATOKA UK. 2

kwa mpigo si nguvu zangu, reli ya SGR si nguvu zangu, elimu bure, hospitali 352 kwa mpigo wakati miaka ya nyuma haikuwezekana si nguvu zangu ni nguvu za mola aliyeko juu, ni nguvu za maombi yenu, hatuna mkataba na Mungu huwezi kufikiria ya baadaye," alisisitiza.

Siku za hivi karibuni wamejitokeza viongozi wa ngazi mbalimbali wakiwamo viongozi wa ngazi za juu na wastaafu, kuonyesha matamanio yao kwa Rais Magufuli (pichani) kuongezewa muda wa kuongoza nchi kwa kufanya mabadiliko ya Katiba.

Kwa mara ya kwanza, mwaka jana mwanzoni, Rais Magufuli alipotembelea makao makuu ya Chama Cha Mapinduzi, alisema hana mpango wa kuongeza muda wa urais na kwamba muda wake ukiisha ataondoka kwa mujibu wa katiba.

## MAGUFULI NI YULE YULE

Rais Magufuli aliwashukuru wananchi wa Chato kwa kuendelea kumwombea na kumwamini huku akiwahakikishia kuwa hajabadilika, akitaja baadhi ya shughuli alizokuwa anafanya.

"Kwangu mimi ni yule yule Magufuli niliyekuwa napita hapa kwenda kuuza maziwa Jineli, ni yule yule nilikuwa naondoka na baiskeli kutoka ziwani hadi Ilemela kuuza furu, ni yule yule niliyekuwa nachunga ng'ombe kuzipeleka mlimani hadi ziwani, ni yule yule kamagufuli, naomba mtambue kwamba sijabadilika na ninamuomba sana Mungu asinibadilishe," alisema.

"Kazi hizi ni za kupita na maisha yetu ni ya kupita, lakini sisi viongozi tuna wajibu wa kuwatumikia wananchi hasa Watanzania maskani, siku zote nimekuwa nikiomba na nyinyi mniombee nisije nikawa na kiburi, nikasahau nilikotoka," alisema na kuongeza:

"Nikasahau kwamba kazi hii ni wajibu ambao amenipa Mungu kuwatumikia Watanzania bila kuwabagua katika kazi, kabila, dini na vyama vyao, mimi nitumike kama chombo kwa ajili yao , cha kuleta maendeleo na mabadiliko ya kweli kwa Watanzania kwa kuzingatia sheria na katiba."

## AWAONYA WALIOJENGA MABONDENI

Aliwaonya wananchi wanaojenga makazi na kufanya shughuli za kibinadamu kwenye vyanzo vya maji na kando ya mito.

"Mvua wakati mwigine zinazidi, lakini tunazichokoza, mfano ni pale Sengerema kuna bwawa linaleta maji, wakati ninafundisha Shule ya Sekondari Sengerema, lilikuwapo kwa miaka yote, watu wamevamia hadi njia ya kutolea maji wameziba kwa kujenga nyumba, maji yamekuja yameleta madhara mpaka vifo vya watu," alibainisha.

"Dar es Salaam watu wamejenga hadi mpaka mwisho wa mto, wengine wanaziba kwa maukuta makubwa, maji hayazuiliwi na hayupo mwenye uwezo wa kuzuia, tuepuke kujenga majengo kwenye mkondo wa maji au mto, tutaanza kuilaumu serikali kwani ndiyo ilikwambia ukajenga kwenye mto?" Alihoji.

Alitoa mfano wa mto wa eneo la Chato ambao umeshajengwa sehemu kubwa na kuwataka wananchi siku wakizolewa na maji wasiilaumu serikali, na kwamba wanaokwenda kujenga mabondeni wajue watapata madhara.

"Niwaombe Watanzania unapotaka kujenga nyumba yako uliza historia ya miaka 10 au 20 ya eneo hilo, bila hivyo tutailaumu serikali kwa makosa unayofaya wewe, na kiukweli serikali itanyamaza haitajibu maana mwalimu mzuri ni yule anayekufundisha kwa vitendo, ukiona sufuria yako inakwenda ziwani utajifunza," alisema.



Aliwataka wananchi kujihadhari na mvua na kutojenga maeneo hatarishi na kwamba mvua zinahitajika kwa ajili ya kupata vyakula vya kutosha kwa kuwa Tanzania ina soko kubwa ndani ya Afrika Mashariki.

## MADC NA NJAA

Pia aliwataka wananchi kufanyakazi kwa bidii ikiwamo kulima kwa wingi chakula kwa kuwa kuna ardhi ya kupanda chakula chochote na kupata mavuno.

"Nilazima tufanye kazi msikae bure, nasisitiza maana mkaa bure huishi bure, ni lazima tufanye kazi, nitashanga kumsikia mkuu wa mkoa au wilaya ananiambia wilaya yake ina njaa, wakati mvua zinanyesha siwasikii wakihamasisha watu kulima, ukiniambia wilaya ina njaa ujiandae kuondoka na njaa yako,"alisema na kuongeza:

"Huu ndiyo wakati wa kuhamasisha watu walime sasa unasubiri mvua iishe halafu uanze kusema kuna njaa sehemu fulani hapana, kwa sababu serikali haina shamba na asiyefanyakazi asile na asipokula? Aliwauliza wananchi ambao walijibu afe."

# Viongozi, wanafunzi wa UDSM watimuliwa

INATOKA UK. 2

licha ya kuwapo mkataba baina yao na bodi hiyo.

Jingine ni kurejesha fedha za wanafunzi zilizokatwa (vitabu na viandikwa, mafunzo kwa vitendo na utafiti), kuwapangia mikopo wanafunzi wa mwaka wa kwanza ambao rufani zao zimetupiliwa mbali ilihali ni wahitaji.

Jingine ni kumbadilisha ofisa mikopo wa chuo hicho ambaye pamoja na mambo mengine, viongozi wa wanafunzi hawaridhishwi na utendaji kazi wake hasa lugha anayoitumia kuzungumza na wanafunzi wanapokuwa na matatizo.

Aidha, wanafunzi hao walimjibu Waziri Ndalichako kupitia taarifa yenye kichwa cha habari 'majibu yetu kwa Waziri juu ya kauli yake ya tunatikisa kiberiti'.

"Sisi Daruso wa hali ya chini wenye matatizo kukosa pesa ya mikopo kwa miezi miwili kwa sasa tunapenda kumtaarifu Waziri Ndalichako kwamba njaa haina ustaarabu, hivyo kauli yake ya dharau haitaturudisha nyuma," ilisema taarifa hiyo na kuongeza:

"Hata aseme vipi ikitimia saa 72 tunakuja kwa 'style' yetu, sisi kauli yake tunaitafsiri ni kama weye shibe hamkumbuki mwenye njaa, tungemshauri tu, kuliko kukoleza machungu yetu wakati huu, angetakiwa atumie muda huo kushughulikia kero zetu kuliko haya afanyayo," alisema.

Katibu wa Mtandao wa Wanafunzi, Malekela Brighton, alithibitisha kuwa wamesimamishwa masomo.

## SUA WAMLILIA JPM

Wakati huo huo, Serikali ya wanafunzi Chuo Kikuu cha Kilimo cha Sokoine (SUA), imemuomba Rais John Magufuli, kuingilia kati ukata unaowakabili wanafunzi kutokana na kukosa mikopo.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa Serikali ya Wananfunzi (Suaso), takribani wanafunzi 250 wanaoendelea na masomo hawajapata kabisa mikopo tangu kufunguliwa kwa chuo Novemba 11, mwaka huu, huku baadhi yao hawakupata mitihani ya marudio.

Aidha, wanafunzi wengine hawajapata vitabu na viandikwa, mafunzo kwa vitendo, fedha za kujikimu pamoja na utafiti.

"Hali hii imepelekea wanafunzi wengi kuishi kwa taabu kukosa umakini darasani na kutokuelewa vyema masomo, kutafuta njia mbadala ya mikopo yenye riba kubwa zaidi ya asilimia 20 na 30 kwa wanafunzi wenzao ndani ya muda mfupi gharama zinazoweza kuepukika," alisema.

Aidha, walitoa mapendekezo ya kumuomba Rais Magufuli kuingilia kati ili wapate mikopo, na kuendelea na masomo, serikali kukamilisha usajili wa matumizi ya dolegumba kwa wanafunzi wanufaika na kutoa fursa kwa wanufaika kupata mikopo kwa wakati.

Pia, wameomba iongezwe nguvu kazi kwenye bodi ya mikopo na kuimarisha mfumo wa utunzaji takwimu ili kuongeza ufanisi.

## THRDC KUWATETEA

Akizungumza na Nipashe, Mratibu wa Mtandao wa Watetezi wa Haki za Binadamu (THRDC), Onesmo Olengurumwa, alisema wamekiuka haki zao kwa kuwa suala la kudai mikopo halijaanza leo, bali lilianza enzi la kina aliyekuwa Spika wa Bunge, Marehemu Samuel Sitta, na si wenyewe mwaka 2005 hadi 2206 walidai na kuandamana wakafukuzwa chuo kizima.

"Ni suala la kawaida wanafunzi kudai haki zao, ni kosa kwa uongozi wa chuo kuwachukulia hatua kwa wanaodai haki zao... tutawatetea na tutakwenda mahakamani kudai haki zao kama ambavyo tumekuwa tukifanya kwa wanafunzi wengine waliokumbwa na matatizo," alisema.

Aidha, alisema suluhisho si kuwafukuza bali kuwasikiliza, na kwamba zamani walidai na kuandamana na hawakuwahi kufukuzwa, lakini kwa sasa wametoa tamko kabla hawajaandamana wamesimamishwa.

# Hakimu mikononi mwa Takukuru tuhuma rushwa

**Na Jumbe Ismailly,**
SINGIDA

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru) Mkoa wa Singida, inamshikilia Hakimu wa Mahakama ya Mwanzo, Mtinko, katika Halmashauri ya Wilaya ya Singida kwa tuhuma za kupokea rushwa ya Sh. 250,000 kutoka kwa mtoa taarifa ili atoe upendeleo kwenye kesi ya madai inayomkabili katika mahakama hiyo.

Mkuu wa Takukuru Mkoa wa Singida, Adili Elinipenda, alimtaja hakimu huyo kuwa ni Bernard Modest Kasanda na kwamba alitenda kosa hilo Jumatatu kinyume cha kifungu cha 15 cha Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa namba 11 ya mwaka 2007.

"Mtuhumiwa Hakimu Kasanda alikamatwa na Takukuru Mkoa wa Singida baada ya kupokea kiasi cha Sh. 250,000 kutoka kwa mtoa taarifa ili aweze kutoa upendeleo kwenye kesi ya madai namba 137/2019," alisema.

Aidha, Elinipenda alifafanua kwamba mtuhumiwa huyo baada ya kupokea fedha hizo alizificha kwenye kasha la dawa ya meno.

Alisema bayana kwamba baada ya kumpekua, mtuhumiwa walimkuta na kiasi kingine cha fedha Sh. 489,100 pamoja na visu vitano, huku kimoja kikiwa kwenye soksi, vingine vikiwa kwenye droo ya meza yake na kwenye mkoba wake.

Alieleza kuwa baada ya tukio hilo, wananchi wawili waliodai wana mashauri yao mbele ya Hakimu Kasanda wakidai pia walimpatia fedha, huku mmoja akidai kutoa Sh. 50,000 na mwingine Sh. 200,000.

Elinipenda alibainisha Takukuru inaendelea kuchunguza mashauri hayo, na umma utajulishwa baada ya kukamilika.




Mkuu wa Wilaya ya Kisarawe, Jokate Mwegelo (wa pili kulia), akimsikiliza Mkuu wa Idara ya Biashara ya Kadi Benki ya NMB, Philbert Casmir, wakati wa mafunzo ya matumizi ya huduma mpya ya MasterBoda QR kwa waendesha bodaboda wa Wilaya ya Kisarawe na vitongoji vyake. Mafunzo hayo yamefanyika jana katika ukumbi wa mikutano wa Ofisi za Wilaya ya Kisarawe. Katikati ni Mkuu wa Kitengo cha Biashara za Serikali, Vicky Bishubo. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Bandari Ziwa Tanganyika sasa zapewa kipaumbele

**Na Elizabeth Zaya,** KIGOMA

MAMLAKA ya Usimamizi wa Bandari Tanzania (TPA) kupitia bandari zake za Ziwa Tanganyika, imeanza mchakato wa kuwekeza nguvu katika bandari za ziwa hilo ili liwe lango la uchumi nchini.

Imeelezwa kuwa uamuzi huo umezingatia uwapo wa fursa nyingi za kibiashara zinazotokana na uwapo wa ziwa hilo linalopakana na nchi tatu zenye rasilimali za kiuchumi ikiwamo Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC).

Meneja wa Bandari za Ziwa Tanganyika, Percival Salama, akizungumza na waandishi wa habari katika Bandari ya Kigoma jana, alisema mbali na rasilimali zilizopo nchini ambazo zimekuwa zikitumia bandari hiyo, bandari za ziwa hilo pia zimekuwa zikitumika kusafirisha bidhaa za DRC na nchi nyingine jirani.

Alisema bandari za Ziwa Tanganyika ndiyo zinatumika kusafirisha bidhaa zenye thamani kubwa ikiwamo dhahabu na mafuta. Salama alisema pamoja na kutegemea bandari zake kubwa za Kigoma, Kasanga na Kibirizi, wameanza kuboresha bandari nyingine ili kuongeza idadi ya bandari kwa lengo la kutimiza azma yao ya kulifanya ziwa hilo kuwa lango la uchumi.

Alisema bandari za Ziwa Tanganyika ziko katika mikoa mitatu ya Kigoma, Katavi na Rukwa kwa upande wa Tanzania. Mbali na Tanzania, ziwa hilo linagusa mipaka ya nchi zingine ambazo ni DRC, Zambia na Burundi.

"Na kama unatafuta asilimia ya kila nchi kwenye Ziwa Tanganyika, Tanzania ina asilimia 45, DRC 41, Burundi nane na Zambia asilimia sita. Na Ziwa Tanganyika ndiyo ziwa la pili kwa kina kirefu duniani, lina wastani wa urefu wa kina cha mita 1,470.

"Kwa hiyo, ukizungumzia uimara wa biashara ya kuhudumia nchi hizi nne, maana yake unazungumzia miaka mingi ijayo. Ni sahihi na ni vyema kwa serikali za nchi hizi nne zinapofanya uwekezaji wa miundombinu ya bandari na vyombo vya usafirishaji, kuhakikisha wananchi wa nchi hizo wanapata huduma," alifafanua.

## Rushwa ya ngono bado tatizo kazini

**Na Joseph Mwendapole**

RUSHWA ya ngono sehemu nyingi za kazi bado ni tatizo nchini, hivyo wafanyakazi wameshauriwa kufichua vitendo hivyo ili waweze kupata msaada wa kisheria na wahusika kuchukuliwa hatua.

Hayo yalisemwa jijini Dar es Salaam na Mkurugenzi wa Shirika la Wanawake katika Sheria na Maendeleo Afrika (WiLDAF), Anna Kulaya.

Alikuwa akizungumza kwenye mkutano kati ya shirika hilo na viongozi wa vyama mbalimbali vya wafanyakazi kuhusu ukatili na unyanyasaji wa kijinsia sehemu za kazi.

Alisema sehemu ya kazi inapaswa kuwa salama kwa mfanyakazi kwani ni sehemu ambayo mfanyakazi anachukua muda mrefu kuishi.

"Kuna ukatili mkubwa sehemu za kazi na kwa kuwa nyinyi ni viongozi sehemu zenu za kazi mtakuwa mnajua zaidi kuliko sisi na tumewaita hapa siyo kutafuta mchawi bali kutafuta namna ya kutokomeza hali hiyo," alisema Kulaya.

Alisema mwaka jana alituma timu ya wafanyakazi wake kwenda kuzungumza na wafanyakazi sehemu mbalimbali za kazi na walichokuta huko kinasikitisha sana.

Aidha, alisema wafanyakazi kwenye sehemu mbalimbali walizungumza kwa uwazi kuhusu rushwa ya ngono sehemu za kazi na ukatili wa kijinsia wanaofanyiwa hasa wanawake.

"Tulichoona huko ndicho kimetusukuma kuandaa mdahalo wa leo baina yetu ili tujadiliane na tuangalie namna ya kuweka mifumo ambayo itakuwa na msaada mkubwa wa kukabiliana na hali hii," alisema Mkurugenzi.

Mwajina Lipinga kutoka Ofisi ya Rais- Tamisemi, alisema serikali iliamua kuanzisha Mpango wa Kutokomeza Ukatili wa Wanawake na Watoto (MTAKUWWA) baada ya kuona hali inazidi kuwa mbaya.

Alisema wakati wa mchakato wa kuanzisha mpango huo wadau mbalimbali wakiwamo WiLDAF ambao alisema wamekuwa bega kwa bega na serikali katika utekelezaji wa mpango huo ambao unatarajiwa kufikia lengo mwaka 2022.

"Serikali iliona kuna shida kubwa kwenye ukatili hasa wanawake na watoto na lengo la Mtakuwwa ni kutokomeza ukatili kwa wanawake na watoto kwa asilimia 50 ikiwezekana kutokomeza kabisa," alisema.

Alisema maeneo ya umma na ya kazi si salama sana kutokana na vitendo vya ukatili vinavyofanyika hivyo wadau hao wanafanasi kubwa ya kuzuia na kumaliza vitendo hivyo.

## BoT yaipa tano benki ya ICB

**Na Mwandishi Wetu**

NAIBU Gavana wa Benki Kuu ya Tanzania (BoT), Dk. Bernard Kibesse, ameipongeza Benki ya Biashara ya Kimataifa (ICB) kwa jitihada zake za utoaji wa mikopo kwa wateja wake hali ambayo inachochea ukuaji wa uchumi nchini.

Akizungumza katifa hafla ya kuazimisha miaka 22 tangu kuanzishwa kwa benki hiyo hapa nchini juzi jijini Dar es Salaam, Dk. Kibesse, alisema benki hiyo imetekeleza vizuri wajibu wake kwa kutoa mikopo na ushauri kwa wateja wake.

“Miaka 22 ya uwapo wa benki ya ICB nchini imekuwa na mafanikio makubwa na imejitahidi sana kutoa mikopo kwa wateja wake, kama washauri wa benki zote hapa nchini tunafarijika na tunawaomba waongeze jitihada hizo ili kufikia azma ya ujenzi wa serikali ya kujenga uchumi wa kati na viwanda ifikapo 2025,” alisema Dk. Kibesse.

Alisema BoT itaendelea kushauri benki ziweze kufika maeneo mbalimbali ya nchi hususan vijijini ili kuongeza watumiaji wa huduma za kibenki hapa nchini.

“Tunapotekeleza azma ya ujenzi wa viwanda na uchumi wa kati kuelekea 2025 lazima pia tusisitize matumizi ya benki kwa watu wetu mijini na vijijini. Natumia nafasi hii kutoa wito kwa benki zote nchini kuendelea kutanua huduma zao hususani maeneo ya vijijini,” alisema.

Dk. Kibesse alieleza kwa sasa hali ya utoaji mikopo kwa benki imeimarika ukilinganisha na miaka miwili iliyopita na hivyo kuonyesha taswira nzuri ya kuimarika kwa uchumi .

“Miaka miwili iliyopita hali ya mikopo haikuwa nzuri, lakini kwa jitihada tulizofanya kwa kushirikiana na mabenki tumefika hatua nzuri ambapo mpaka mwezi Novemba mwaka huu utoaji wa mikopo ulikuwa umefikia asilimia 9.7,” alifafanua Dk. Kibesse.

Mmoja wa wabia wakuu wa Benki ya ICB Tanzania ambaye ni Mwenyekiti wa Bodi, Josephine Sevaretnam, alisema wameridhishwa na mazingira ya kiuwekezaji yaliyopo Tanzania na wamejipanga kuboresha zaidi huduma zao.

“Miaka 22 ya kuwapo kwetu Tanzania ilikuwa ya kujivunia na yenye mafanikio makubwa licha ya changamoto za hapa na pale tumejipanga kwa miaka mingine ijayo ambapo tutajikita katika kufanya uwekezaji zaidi na matumizi ya teknolojia ili kuwafikia wateja wengi zaidi,” alisema.

Aidha, alieleza matumaini yake kwa serikali ya Tanzania na sekta ya kibenki kwa namna inavyoweka mipango yake kwa kushirikisha wadau jambo ambalo limewapa nguvu zaidi ya kuwekeza Tanzania.

“Kama wabia wakuu tutaendelea kuwekeza Tanzania na tunajivunia kuwa katika sehemu ya kutimiza malengo ya nchi hii ya ujenzi wa uchumi wa kati na viwanda ifikapo mwaka 2025,” alisema na kuondoa uvumi wa kuuzwa kwa benki hiyo ambapo alieleza haijauzwa.

Benki ya ICB ilianzishwa mwaka 1997 na mpaka sasa imetimiza miaka 22 na ina matawi matano huku ikitarajiwa kufungua tawi la sita jijini Dodoma.

# Osha yapiga hatua zaidi usalama mahali pa kazi

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge, Kazi, Vijana, Ajira na wenye Ulemavu), Jenista Mhagama, amesema Wakala wa Usalama na Afya Mahali pa Kazi (Osha) imefanikiwa kwa asilimia kubwa katika kuhakikisha afya za wafanyakazi zinazingatiwa katika maeneo yao ya kazi hapa nchini.

Aliyasema hayo katika kikao cha tano cha Baraza la Tatu la Wafanyakazi wa Osha, baada ya kupokea taarifa ya utekelezaji wa majukumu ya taasisi hiyo katika nusu ya kwanza ya mwaka wa fedha 2019/2020.

“Niwapongeze sana kwa kazi nzuri mnayoifanya katika kuhakikisha kuwa afya za wafanyakazi ambao ndio wanaosaidia katika ukuaji wa uchumi wa Taifa hili zinazingatiwa katika maeneo yao ya kazi,” alisema Mhagama. Mhagama alisema Osha ambayo ni taasisi ya serikali, imepiga hatua kubwa katika utekelezaji wake wa majukumu na kwamba mazingira ya ufanyaji kazi kwa wafanyakazi wengi nchini hususani katika taasisi wamekuwa salama.

Aidha, Waziri Mhagama, aliitaka Osha kuongeza juhudi zaidi katika utendaji ikiwamo kushiriki kikamilifu katika mapambano dhidi ya maambukizi ya Virusi vya Ukimwi (VVU) katika maeneo ya kazi, alisema pamoja na takwimu kuonyesha kwamba maambukizi yanapungua kitaifa, changamoto hiyo inaendelea kuwakumba Watanzania hasa vijana wenye umri wa kati ya miaka 15 hadi 24. Naye Kaimu Mtendaji wa Osha, Khadija Mwenda, akiwasilisha taarifa ya taasisi hiyo kwa Waziri Mhagama katika kipindi cha Julai hadi Desemba alisema: “Waziri katika kipindi cha kuanzia Julai hadi Desemba mwaka huu tumepata mafanikio makubwa sana katika utekelezaji wa majukumu yetu. Tumesajili maeneo ya kazi 1,919 kati ya 2,324 yaliyopangwa, tumefanya ukaguzi katika maeneo ya kazi 8,234 kati ya 10,000 yaliyokuwa yamepangwa.”

Alisema mafanikio mengine ni kuwapima afya wafanyakazi 90,193 zaidi ya idadi ya wafanyakazi 75,032 iliyokuwa imepangwa, kutoa adhabu kwa waajiri 80 ambao walishindwa kukidhi vigezo vya afya na usalama katika maeneo yao ya kazi na kuandaa kanuni saba ambazo zipo katika hatua mbalimbali za utungwaji.



Mkurugenzi Mtendaji wa Mtandao wa Jinsia Tanzania (TGNP), Lilian Liundi, akizungumza na waandishi wa habari kwenye warsha ya kuwajengea uwezo namna ya kuandika habari za kuhamasisha wanawake kushiriki kwenye nafasi za uongozi ikiwamo siasa, ili wajitokeze kwa wingi kuwania uongozi kwenye uchaguzi mkuu mwakani. **PICHA NA MARCO MADUHU**

# Tari kuzalisha mbegu za kisasa

**Na Ashton Balaigwa,** DODOMA

TAASISI ya Utafiti wa Kilimo Tanzania (TARI) imesema ipo tayari kuzalisha mbegu za teknolojia ya kisasa za mazao mbalimbali ili kuondoa utegemezi uliofikia asilimia 70.

Jitihada hizo ni utekelezaji wa agizo la Rais John Magufuli, aliyeagiza Wizara ya Kilimo kuacha utegemezi wa mbegu kutoka nje na badala yake zizalishwe nchini.

Mkurugenzi Mkuu wa TARI, Dk. Geoffrey Mkamilo, alisema kwa kutumia mashamba ya taasisi hiyo wanaweza kuzalisha mbegu hizo ili kuwasaidia wakulima kupata mbegu bora na zenye ukidhani na magonjwa na hivyo kuachana na utegemezi wa mbegu kutoka nje ya nchi.

Alisema baadhi ya vituo vya Tari ambavyo vimepewa majukumu ya kuzalisha mbegu kulingana na mazao yanayolimwa katika maeneo yao yameanza kuzalishwa na kuwasaidia wakulima kupata mbegu hizo za teknolojia ya kisasa ambazo zina sifa nyingine ya kupambana na ukidhani wa wadudu.

“Kituo cha Ilonga-Morogoro kimepewa jukumu la kuzalisha mbegu za alizeti, mtama, mahindi, mazao ya mikunde na mazao ya mizizi.”

Mkurugenzi wa Tari Naliendele, Dk. Fortunatus Kapinga, alisema tatizo la upungufu wa mbegu za korosho na ufuta litakuwa historia kutokana na kituo hicho kuongeza uzalishaji baada ya kuanzisha mashamba mapya ya mbegu katika mikoa inayolima zao hilo kwa wingi. Naye Mkurugenzi wa Tari Tengeru, Arusha Dk. Stephano Sebastian, alisema wameshaweka mkakati wa kusaidia upungufu wa mbegu kwa mazao ya mboga na matunda ambayo yanatumika kama sehemu ya malighafi kwenye viwanda.

Mkurugenzi wa Tari Ilonga, Morogoro, Dk. Joel Meriyo, alisema mkakati uliowekwa kwa sasa ni kuzalisha mbegu za alizeti za teknolojia ya kisasa wastani wa tani 3,000 ambazo zitasaidia kuzalisha alizeti zisizopungua tani 60,000 na kupunguza kasi ya ugizaji wa mafuta ya kula kutoka nje ya nchi.

Naye Meneja wa Tari Dakawa Mvomero, ambao ni wazalishaji wa mbegu bora za mpunga, Dk. Andrew Ngereza, alisema wametafiti mbegu bora ya mpunga ya teknolojia ya kisasa aina ya saro 5 ambayo ina uwezo wa kukabiliana na ukidhani wa wadudu pamoja na ukame.





# Wakulima walia tembo kuharibu mazao

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

BAADHI ya wakulima wa Kijiji cha Lengast Kata ya Naisinyai wilayani Simanjiro mkoani Manyara, wamelalamikia vitendo vya tembo kula mazao yao mashambani.

Wakizungumza juzi mbele ya Mkuu wa Wilaya ya Simanjiro, Zephania Chaula, alipotembelea kijiji hicho, wakazi hao walidai kuwa tembo wamekuwa kero kwa wakulima.

Mmoja wa wakulima hao, Kanuga Lembesei, aliiomba serikali kuchukua hatua za kudhibiti wanyama hao kwani wakulima wanapoteza nguvu zao kufanyakazi ya kilimo, ambacho mwisho wa siku wanaambulia kilio baada ya mazao yao kuliwa na tembo.

Mkazi mwingine, Rebecca Laizer, alisema viongozi wa serikali wanapaswakuingilia kati jambo hilo kabla hawajaleta madhara kwa binadamu baada ya kumaliza mazao yao.

"Serikali ilisema haitagawa chakula cha msaada, hivyo watu walime nasi tumefanya hivyo, lakini tembo wamevamia na kuyaharibu mazao yetu nasi tunashindwa kufanya lolote," alisema Laizer.

Mkuu wa Wilaya ya Simanjiro, Zephania Chaula, aliwataka wakazi wa eneo hilo kutowasogelea tembo hao bali wakiwaona wawe na tahadhari ili wasiwadhuru.

Chaula alisema tembo walikuwapo hata ndani ya ukuta unaozunguka migodiya madini ya tanzanite Mji Mdogo wa Mirerani ila walitolewa.

"Pindi likitokea tatizo la tembo kula mazao mnapaswa kutoa taarifa kwa viongozi wa kijiji ili wafikishe suala hilo kwa maofisa wanyamapori ili mpate kifuta jasho," alisema Chaula.




Mkuu wa Wilaya ya Arusha, Gabriel Daqqaro, akijisajili kwa alama za vidole kwenye Kampuni ya Simu Tanzania (TTCL) jijini Arusha. **PICHA: WOINDE SHIZZA**

# Wafanyakazi wahamasishwa kuanzisha Saccos

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

WAFANYAKAZI waliopo katika mashirika na kampuni nchini, wamehamasishwa kuanzisha vyama vya akiba na mikopo (Sacos), katika maeneo yao ya kazi ili kujikwamua kiuchumi.

Hayo yalisemwa na Mwenyekiti wa Chama cha Akiba na Mikopo cha Wafanyakazi wa Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro, Marcel Bituro, wakati akizungumza katika mkutano wa jukwaa la vyama vya kuweka na kukopa mkoani Arusha.

Bituro alisema kuna umuhimu mkubwa wa mashirika na taasisi kuanzisha vyama hivyo kwani vinasaidia katika kujikwamua kiuchumi pamoja na kuweka akiba ya fedha, ambazo zitasaidia kutatua changamoto mbalimbali.

Aliema uwapo wa vyama hivyo pia unasaidia wanachama kubuni miradi ya maendeleo na wanapostaafu huwawezesha kujipanga kimaisha.

"Chama chetu kilianza mwaka 2002 na tuna wanachama 400 hadi sasa,

Na tumeanzisha mfuko wa elimu, ambao humwezesha mwanachama kuweka akiba kwa ajili ya ada za watoto," alisema Bituro.

Naye Mwenyekiti wa Chama cha Kilombero Multipurpose, Julius Akyoo, alisema wamewasaidia wanachama wake kujikwamua kiuchumi kwa kuwakopesha mikopo ya fedha ambayo hurejeshwa kwa riba nafuu.

Akyoo alisema wamejiwekea malengo ya kuanzisha vitega uchumi mbalimbali, ikiwamo kujenga jengo la ghorofa tano, na wapo katika hatua za mwisho za kuanza mradi huo.

Aidha, aliwataka viongozi wa vyama hivyo kufanya kazi zao kwa uwazi na kuwa na nidhamu ya matumizi mazuri ya fedha ili kuondoa migogoro mbalimbali katika vyama hivyo.

Mwenyekiti wa Chama cha Kuweka na Kukopa cha Wakulima wa zao la kahawa pori (AMCOS), Elirehema Maturo, alisema wamewasaidia wakulima wa kahawa kupata soko la uhakika kwa kununua kahawa yao kwa bei nzuri sambamba na kutoa elimu jinsi ya kuboresha kilimo hicho.

Alisema katika vyama hivyo ni lazima wakawapo viongozi bora na wasikivu, ambao watakuwa tayari kusikiliza changamoto za wanachama wao na kuzitatua kwa haraka pamoja na kuondoa migogoro.

# Wazazi watakiwa kuelimisha watoto

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

WAZAZI na walezi wametakiwa kuwa mstari wa mbele kutoa elimu kwa watoto, ili kuwawezesha kufichua vitendo viovu wanavyofanyiwa na kutoa taarifa kwenye vyombo husika.

Hayo yalisemwa na mwakilishi wa Kaimu Mkuu wa Taasisi ya Maendeleo ya Jamii Tengeru (TICD) ambaye ni msajili wa wanafunzi katika taasisi hiyo, Godfrey Meliyo, wakati akizungumza katika kongamano lililowashirikisha wanafunzi wa taasisi hiyo na wanaozunguka eneo hilo likiwa na lengo la kujadili na kuzungumza changamoto zinazowakabili watoto.

Meliyo alisema kongamano hilo limelenga kuwajengea uwezo na kutoa elimu kwa watoto hao ili wazifahamu haki zao za msingi na kujua sehemu sahihi ya kutoa taarifa za matukio yao wanapofanyiwa ukatili.

Alisema suala la kumlinda mtoto linamhusu kila mmoja kwa nafasi yake, hivyo ni vema kila mtu akatoa elimu kwa watoto ili wazifahamu haki zao na kujua sehemu sahihi ya kutoa taarifa ya matukio wanayokutana nayo.

Meliyo alisema uwapo wa mila na desturi katika jamii zinazowazunguka zinachangia kwa kiasi kikubwa jamii kushindwa kubadilika na kuzielewa ipasavyo haki za watoto hao.

"Kwa kweli serikali imeendelea kujenga mazingira mazuri kwa watoto ikiwamo kuwapo kwa sheria ya mwaka 2009 inayohakikisha haki za watoto zinazingatiwa sambamba na kutengeneza mazingira mazuri ya elimu katika kutoa elimu bure kwa kila mtoto," alisema Meliyo.

Naye Mkuu wa Idara ya Jinsia na Maendeleo wa Taasisi hiyo, Dickson Lukumay, alisema wao kama taasisi wamewakutanisha watoto kutoka shule zinazozunguka taasisi hiyo na kuwajengea uwezo wa kutambua changamoto zao na namna ya kukabiliana nazo ikiwa pamoja na kuzitolea taarifa katika vyombo husika.

Lukumay alisema kupitia kongamano hilo watoto hao watapata ujjasiri kueleza changamoto wanazokutana nazo na kutoa taarifa sehemu husika, na mwisho wa siku kupata ufumbuzi wa matatizo yanayowakabili.

Aliongeza kuwa watoto hawajajengewa uwezo wa kutosha na kupewa elimu sahihi namna ya kukabililana na changamoto wanazokabiliana nazo, ili hatua stahiki zichukuliwe, hivyo juhudi zaidi zinahitaji kuongezwa ili kumsaidia mtoto.

Baadhi ya wanafunzi walioshiriki kongamano hilo, Anna John na Juma Hassan, walisema kuwa wanakutana na changamoto mbalimbali katika jamii, ambazo huwawia vigumu kuzungumza, hivyo waliiomba serikali na wadau kuongeza juhudi ya kuwalinda na kuwajali watoto hao dhidi ya vitendo vya ukatili wanavyofanyiwa katika jamii.

# Barabara Seminari Uru yaharibika kwa miezi 10

**Na Godfrey Mushi,** MOSHI

BARABARA inayounganisha Kisawio na Seminari ya Uru wilayani Moshi Vijijini, imekatika kwenye eneo la kwa Ino, kwa takribani miezi 10 sasa.

Wakati hayo yakijiri wakazi wa kata ya Uru Kusini wameeleza kuteseka kwa kuzunguka umbali mrefu ili kufikia huduma wanazozifuata Moshi mjini.

Kundi linaloumia ni wajawazito, wazee na watoto wanaokwenda katika Hospitali ya Rufani ya Mawenzi pamoja na KCMC. Jana, Diwani wa Kata ya Uru Kusini, Wilhard Kitali, akizungumzia hali mbaya ya ubovu wa miundombinu ya barabara hiyo, alisema wakazi wengi wa vijiji vyake, wanahaha kutafuta mwarobaini wa tatizo hilo na wako tayari kuchanga fedha kwa ajili ya kununua vifusi vya changarawe vinaendelea.

Hata hivyo, wanasubiri iwapo Wakala wa Barabara za Mijini na Vijijini (Tarura) watafanya matengenezo ya dharura.

"Tunaomba Mkuu wa Wilaya ya Moshi, Kippi Warioba, iliangalie jambo hili, hali sio nzuri kwa watumiaji wa barabara hiyo, kwa sababu hakuna mawasiliano tangu Machi mwaka huu. Nimepiga kelele kwa mamlaka husika kusaidia kurejesha mawasiliano, lakini mpaka tunafika mwisho wa mwaka hakuna hata matengenezo ya dharura yaliyofanyika. Niwaombe Tarura waliangalie upya suala hili," alisema Kitali.

Barabara hiyo iliharibiwa vibaya na mvua za masika zilizonyesha maeneo mbalimbali nchini na kusababisha kuharibika miundombinu na hivyo wananchi kukaa kwenye adha ya usafiri kwa muda mrefu.

Aidha, baadhi ya wakazi wanaoishi karibu na Seminari ya Uru, Joseline Emmanuel na Omega Tesha, kwa nyakati tofauti walieleza kuwa ubovu wa barabara hiyo umesababisha wanawake wajawazito na watoto kushindwa kwenda hospitalini kupata huduma za afya.

Kutokana na hali hiyo, wananchi wa kata hiyo wameiomba serikali kutatua tatizo hilo, kwa kuwa wanalazimika kutumia gharama kubwa kukodi usafiri wa pikipiki baada ya mabasi madogo ya daladala kupandishwa nauli.

"Wajawazito na watoto ndiyo waathirika wakuu wa tatizo hilo kwa sababu wanalazimika kutembea zaidi ya kilomita 15 kuzunguka barabara nyingine kufuata huduma mbalimbali za kijamii kwenye kata ya jirani. Tunamwomba Mkuu wa Wilaya awasukume Tarura Wakala wa Barabara za Mjini na Vijijini, watusaidie kumaliza tatizo," alisema Joseline.

Alipotafutwa Meneja wa Wakala wa Barabara za Mjini na Vijijini (Tarura) katika Halmashauri ya Wilaya ya Moshi, Roy Johansen, kuzungumzia madai hayo na kama kuna uwezekano wa kufanyika matengenezo ya dharura, hakupatikana kutokana na simu yake kutokuwa hewani.



Kamati ya Mazingira katika Kijiji cha Mazingira wilayani Handeni, Mkoa wa Tanga, wakipanda juu ya jiwe lenye kichwa, pua mbili na mdomo mfano wa binadamu juu ya kilele cha jiwe hilo, wanapoishi nyoka wakubwa wenye rangi za kupendeza wasio na madhara kwa binadamu. **PICHA: BONIFACE GIDEON**

# Mkuu wa Mkoa aagiza utafiti 'kifo' cha kahawa

**Na Mwandishi Wetu,** SAME

KUZOROTA uzalishaji wa kahawa katika baadhi ya wilaya mkoani Kilimanjaro kumemsukuma Mkuu wa Mkoa huo, Dk. Anna Mghwira, kuagiza wataalamu wa kilimo kutafiti na kujua kile wakulima wanachotaka.

Alitoa maelekezo hayo kwa wataalamu wa Wilaya ya Same kutafiti kujua wakulima wanachotaka.

Mkuu wa Wilaya ya Same, Rosemary Senyamule, ilieleza kuwa serikali inataka kulifufua zao la kahawa ambalo kwa sasa wakulima wengi wameliacha kutokana na matatizo mbalimbali. Alisema uongozi wa mkoa umeona kuna haja ya kufanyika utafiti kwenye uzalishaji wa kahawa ili kujua wakulima wa Same wanahitaji elimu gani ili waandaliwe mafunzo yatakayowawezesha kufanya kilimo hicho kwa mafanikio zaidi.

"Alikuja Same na kuzungumza na wananchi wa Vudee na kuelekeza kufanya utafiti huo. Leo napenda kuutangazia umma kuwa tayari kazi hiyo imeanza chini ya wataalamu wetu na muda ukifika tutatoa majibu," aliahidi Senyamule.

Kwa mujibu wa maelezo yake, Dk. Mghwira alimwagiza Ofisa Tarafa na Mtendaji wa Kata ya Vudee, kutoa taarifa muhimu za zao hilo ikiwa ni pamoja na idadi ya mashamba pamoja na wakulima na mahitaji ya miche ya kisasa ya kahawa.

Wiki iliyopita, wadau wa uzalishaji wa kahawa nchini walinukuliwa na gazeti hili wakisema bei ndogo ya zao hilo katika soko la dunia hasa ile inayostawishwa Tanzania ni moja ya mambo yanayokwamisha jitihada za serikali kufufua kasi ya uzalishaji wake.

Makamu Mwenyekiti wa Taasisi ya Wadau wa Kahawa Tanzania, Noel Yatera, alieleza kuwa mtazamo wao kuhusu maendeleo ya zao hilo, wakati kikao chao katika Manispaa ya Moshi.

Katika mkutano huo, wadau hao walieleza masuala kama mabadiliko ya tabianchi kuwa nayo yanatajwa kuwa moja ya tatizo ambalo linaikabili sekta hiyo.

# Waziri Jafo atoa maagizo ujenzi kituo cha afya Longoi

**Na Godfrey Mushi,** HAI

SERIKALI imeagiza fedha za ujenzi wa majengo ya Kituo cha Afya cha Heshima cha Longoi zielekezwe kwanza kujenga jengo la wagonjwa wa nje la kinamama, watoto na maabara.

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi), Selemani Jafo, ndiye aliyetoa maelekezo hayo.

Kituo hicho kinajengwa kwa mapato ya ndani pamoja na michango ya wadau wa vyama vya ushirika.

Jana Mkuu wa Wilaya ya Hai, Lengai ole Sabaya, aliieleza Nipashe kuwa amepokea maelekezo ya waziri huyo na tayari ameagiza majengo hayo kupewa kipaumbele.

"Nimeshamwambia Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya, Yohana Sintoo, agizo la Waziri Jafo kuwa lianze jengo la wagonjwa wa nje, la mama na mtoto na upasuaji pamoja na maabara.

Ujenzi wa kituo hicho umetengewa Sh. milioni 388 hadi sasa kwa ajili ya majengo hayo ya awali.

Alisema likimalizika litamaliza tatizo la muda mrefu la wanawake na watoto waliokuwa wanatoka vijiji vya pembezoni ambao walilazimika kuvuka daraja la Mnepo-Kiyungi usiku wa manane ambalo lipo karibu na mashamba ya miwa ya kiwanda cha sukari cha TPC kilichopo Wilaya ya Moshi.

"Sasa hivi wanawake na watoto waliokuwa wanavuka usiku wa manane wanapitia pale Shirimgungani hadi Mijongweni kwenda mpaka Shirimatunda, hawatakwenda tena huko kufuata huduma, huduma zao sasa zimeletwa Longoi," alisema Sabaya.

Zaidi ya wananchi 27,000 wa Kata za Weruweru, Mnadani na Masama Rundugai wanatarajia kunufaika na huduma hiyo ya kuanzishwa kwa kituo cha afya cha Heshima Longoi.

Ujenzi wa kituo hicho, unakadiriwa kugharimu zaidi ya Sh. milioni 600 hadi kukamilika.

Mwanzoni mwa wiki hii, Mganga Mkuu wa Wilaya, Dk. Irene Haule, alisema wazo la ujenzi wa kituo hicho cha afya lilitolewa na Mkuu wa Wilaya na kwamba kitawasaidia wananchi wa kata hizo ambao baadhi yao wamekuwa wakitembea umbali zaidi ya kilomita 20 kila siku kufuata huduma za afya katika hospitali ya wilaya.

Kwa upande wake, Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Hai, Yohana Sintoo, aliahidi kuzisimamia kikamilifu fedha hizo ili ujenzi wa kituo hicho ukamilike kwa wakati.

Pia aliwataka wananchi wa eneo hilo wasiibe wala kuhujumu miundombinu ya mradi huo.

ama

ALHAMISI DESEMBA 19, 2019

AFYA NA MAZINGIRA



Ukurasa 20

**Kulala na kuamka kunavyoathiri ufanyaji kazi wa mtu siku nzima**



Ukurasa 16

Kamanda Muslim: Nahisi mwisho wa mwaka huu Polisi tutapumua na ajali



Ukurasa 14

**Papa afuta faragha kashfa za ngono**



## USHUHUDA UNAOSIKITISHA...

# Mama wa njiti wanne asimulia mazito, milima na mabonde

Ukurasa 18

# Papa afuta faragha kashfa za ngono



Papa Francis. **PICHA: MTANDAO.**

KIONGOZI wa Kanisa Katoliki Duniani, Papa Francis, amefuta faragha ya siri kuhusu kashfa za udhalilishaji wa kingono ndani ya kanisa hilo.

Papa Francis amechukua hatua hiyo, kutokana na kuongezeka malalamiko kwamba kanuni hiyo, ilikuwa inatumika kwa ajili ya kuwalinda wahalifu na kuwanyamazisha waliofanyiwa uhalifu wa kingono, pia ilitumika kuwazuia polisi kuchunguza uhalifu huo.

Watu waliotendewa uhalifu pamoja na mawakili wao wameushangilia uamuzi wa Papa Francis na kwa mtazamo wao, hatua hiyo ilipaswa kuchukuliwa mapema zaidi.

Hata hivyo wametahadharisha kwa kusema kwamba ufanisi wa hatua hiyo utathibitishwa pale ambapo kanisa litakapolazimishwa kukubali uchunguzi ufanyike katika nchi husika na nyaraka zote juu ya wahalifu zitolewe hadharani.

Kwa mujibu wa sheria mpya Papa Francis, ameeleza kuwa habari zinazohusu uhalifu wa kingono zitalindwa na viongozi wa kanisa lakini ameeleza wazi kwamba kanuni ya kanisa kuficha siri haitatumika tena. **DW**

AFYA

IJUE BUGANDO DAY

# Sherehe inayong'arisha tiba bora ya hospitali katika sura mpya 2020

## • Wachapakazi 'walamba' laki tano • Mkurugenzi afunguka vigezo vyote



Wafanyakazi wa Hospitali ya Bugando katika maandamano kuelekea uwanja wa CCM Kirumba, kuadhimisha Siku ya Bugando.

**Na Anthony Gervas,** MWANZA

INAPOTAJWA Bugando inaleta ujumbe kuwa ndio hospitali kubwa zaidi katika Kanda ya Ziwa na hata kuwa katika nyayo za kitaifa, nyuma ya Hospitali ya Taifa Muhimbili.

Huduma ni nyingi na daraja za juu na kila kukicha kuna upanuzi unaoendelea, katika nafasi ya miundombinu na fursa za huduma mbalimbali.

Waswahili wana usemi 'usione vinaelea vimeundwa.' Ufanisi huo ni chanzo cha tija nafasi fulani. Bugando ambayo ni Hospitali ya Kanda ya Ziwa, imeanzisha utaratibu wa kuwapa tuzo au zawadi nono.

Ni sherehe maalum iitwayo 'Bugando Day' inayoadhimishwa kila Desemba 14 na mwaka huu ilikuwa Jumamosi iliyopita, katika Uwanja wa Kirumba.

Katika sherehe hizo kuna watumishi hodari 18 'walilamba dume'baada ya kupewa zawadi ya Sh.500, 000 kila moja ikiwa jumla ya Sh.milioni tisa zilitolewa na Mkurugenzi Mkuu wa hospitali hiyo, Profesa Abel Makubi.

> **Sio wale wanaoisema vibaya, hawaleti hata wagonjwa kutoka mtaani, hao wataendelea kuwanyima zawadi za Sh.500, 000 kila mwaka.**

Anasema, lengo kuu ni kuboresha utendaji kazi wa watumishi wa hospitali, wawajibike kwa bidii, wakijituma na wazalendo zaidi wakati wa kuhudumia wagonjwa, wateja na wageni wengine.

Mkurugenzi anakumbusha utendaji unapaswa kutojali uwezo binafsi wa mgonjwa ua mgeni na unaodumisha ushirikiano na umoja wa wafanyakazi wa hospitali hiyo na Chuo Kikuu cha Tiba ya Afya (Cuhas)

Profesa Makubi ananyooshea kidole wafanyakazi wasioitakia mema hospitali kwa kutotoa huduma nzuri kwa wagonjwa ndani ya hospitali na nje inapobidi.

Anatahadharisha: "Sio wale wanaoisema vibaya, hawaleti hata wagonjwa kutoka mtaani, hao wataendelea kuwanyima zawadi za Sh.500, 000 kila mwaka."

### VIGEZO VYA ZAWADI

"Tumeshaanzisha utaratibu wafanyakazi hodari kuwapa tuzo au zawadi kila mwaka Sh.500, 000, wakati wa sherehe za Maadhimisho ya Siku ya 'Bugando Day' ila wale wanaoisema vibaya hospitali yetu, hawatapata zawadi hizo za kila mwaka," anasema.Prof. Makubi.

Anaainisha utaratibu wa kuwazawadia wafanyakazi hodari uko katika makundi 'A' hadi 'B' na vigezo vyake kwa kuangalia eneo la uboreshaji huduma za afya na katika kundi 'A' vinaangaliwa vigezo aina 10 vinavyowawezesha kupatikana zawadi au tuzo hiyo.

Anasema kuna watu 10 katika eneo la kuboresha huduma za afya na wateule husika wanaobainika kutoa mchango mkubwa wa huduma za afya kwa wananchi, wateja wake.

Profesa Makubi anasema watumishi wanaotoa mchango mkubwa wa huduma hizo na watu 10 wanaozawadiwa, akiwainisha kama vile daktari, muuguzi, mtaalamu maabara, mfamasia na wengine wanaochangia katika kupatikana huduma bora kwa wateja.

Anasema, kinachofuatia ni kigezo kwa mtumishi wengine ni anayetoa huduma vizuri; mrejesho wa kazi kwa daktari, muuguzi au kwa wagonjwa; tatu ni daktari, nesi na mtaalamu wa maabara, taarifa nzuri za wagonjwa katika kuweka kwenye mafaili mfumo mzuri' na kutia saini.

Lingine la nne, ni kigezo kinachoangalia daktari bingwa anayefanya kazi kwa wakati na kutoa majibu haraka kwa wagonjwa, pia mtu ambaye akiitwa na wenzake katika idara yeyote anaenda kwa wakati kutoa ushirikiano.

Profesa Makubi anakitaja kigezo cha tano ni pale mtumishi anapoitwa kwa namna yoyote, anaenda haraka, atakayepima kwa haraka wake, anayefanya kazi nzuri kuhudumia wagonjwa kutimiza wajibu wake.

Kigezo cha sita kwa mujibu wa Profesa Makubi, ni pale muuguzi bora au daktari anayetoa huduma vizuri za wagonjwa, bila ya kujali uwezo wa anayeumwa.

Anaendelea na kigezo cha saba, kwamba iwe ama daktari au muuguzi anayemfuatilia kwa haraka mgonjwa, ili aweze kuondoka haraka anaporuhusiwa au hata inapotokea anapoteza maisha.

Nafasi ya nane inatoa fursa kwa mtumishi anayefuatilia vipimo, ili kupata majibu ya haraka ya mgonjwa iwe kutoka maabara au kwingineko

Kigezo cha tisa kwa mujibu wa Profesa Makubi, inamhitaji mtumishi anayefanya kazi kwa kujituma, uzalendo na mfuatiliaji miongozo inayotolewa katika mikutano ya madaktari na wauguzi katika kuboresha huduma za wananchi, kliniki na upasuaji, anahudhuria mikutano ya wauguzi na madaktari.

Mkurugenzi Mkuu anahitimisha kigezo cha mwisho, kwamba katika kundi 'A' kwamba ni mtu anayefuatilia na kusimamia miongozo inayotolewa katika mikutano ya madaktari na manesi, kuhusu uboreshaji huduma za kliniki, upasuaji na mahudhurio kwenye mikutano hiyo.

AFYA

# Sherehe inayong'arisha tiba bora ya hospitali katika sura mpya 2020

**VIGEZO 'B'**

Profesa Makubi akianza kwa kufafanua kigezo cha kwanza:"Daktari ni yule anayeleta wagonjwa wengi kliniki, wodini, katika wodi binafsi na wodi mashuhuri (VIP) kutoka mtaani."

Anaorodhesha kigezo cha pili, kwa anayeongoza idadi kuleta wagonjwa wengi wa upasuaji, kutoka mitaani na kigezo cha tatu kinamuangukia mtumishi anayetoa huduma bora za vipimo au dawa kwa wagonjwa.

Mtazamo wa nne kwa mujibu wa mkurungenzi mkuu, ni kwa mfuatiliaji bora wa ukusanyaji malipo au bili za wagonjwa zinazodaiwa kutoka vyanzo tofauti.

Suala la tano, mtazamo wa mfanyakazi anayetumia mbinu za ziada kuondoa misamaha isiyokuwa ya lazima, anawahi kazini na kututatua kero za wagonjwa haraka, akidhibiti mapato na matumizi yasiyokuwa ya lazima, kubana matumizi ya maji na umeme.

Mkurugenzi Mkuu Prof. Makubi, anapigilia msumari kigezo cha tano cha kumtaka mhusika kuwajibika katika mbinu za kuhakikisha anapunguza na kuondoa misamaha ya wagonjwa isiyokuwa ya lazima. Pia, kuna suala la kumpa tathmini ya kumtambua mfanyakazi anayedhibiti mapato na matumizi yasiyokuwa ya lazima hospitalini. Hiyo inawaangukia wanaotoa vifaa bora vya huduma, kubana matumizi ya maji na umeme kutotumika vibaya.

Nafasi ya saba katika kundi 'B' inajali mtu anayekuwa mbunifu katika miradi ya maendeleo ya hospitali na ukusanyaji wa mapato. Profesa Makubi anaendelea:

"Kigezo kingine cha nane, ni mfanyakazi anayeitangaza vema hospitali ya kanda ya Ziwa-Bugando, ndiye ataendelea kupewa zawadi hizo kila mwaka."

Anatahadharisha: "Sio wale wanaoisema vibaya, hawaleti hata wagonjwa kutoka mtaani, hao wataendelea kuwanyima zawadi za Sh, 500,000 kila mwaka."

"Kigezo cha tisa ambacho ni mwisho ni mfanyakazi atapimwa kwa kutunza mali za taasisi awe msafi, asiwe mharibifu wa mali zilizopo katika hospitali hiyo," anafafanua.

**BUGANDO MPYA**

Profesa Makubi, anasema sherehe za 'Bugando Day' zilizoanzishwa mwaka jana, lengo lake ni kuwabaini watumishi wazembe na wasioitakia mema hospitali hiyo

Katika hatua nyingine, hospitali ya Bugando, itaendelea kuboresha huduma za afya na wahudumu wake kuendelea kupewa elimu bora ya utoaji huduma za afya.

Anasema hospitali inatarajia kuwa na huduma nzuri zaidi za upasuaji kwa wananchi ifikapo mwaka ujao unaoanza wiki mbili zijazo, akiwasihi wajitahidi kuwajibika katika nafasi yake kuhudumia wananchi.

Profesa Makubi, anawasihi wahusika wa vitengo vyote vinavyotoa huduma za wagonjwa hadi utawala, waboreshe huduma kwa wateja na wafanyakazi wa hospitali kwa ujumla; Chuo Kikuu Cuhas na wafanyakazi wake watoe ushirikiano wa umoja na wale wa hospitalini.

Anampongeza Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Ummy Mwalimu, kwa jitihada zake kupitia serikalini kuwa ni mchapakazi anayesaidia sehemu kubwa Bugando katika mageuzi, inayofanya sasa ichukue sura mpya.



Wafanyakazi wanawake wa Hospitali ya Bugando, wakiwa katika shindano la kuvuta kamba, kwenye uwanja wa CCM Kirumba, Jumamosi iliyopita. **PICHA ZOTE: ANTHONY GERVAS.**



Wafanyakazi wanaume wa Hospitali ya Bugando, katika shindano la kukimbia na magunia.

> **Kigezo kingine cha nane, ni mfanyakazi anayeitangaza vema hospitali ya kanda ya Ziwa-Bugando, ndiye ataendelea kupewa zawadi hizo kila mwaka.**

**MICHEZO YANOGA**

Katika maadhimisho hayo ya sherehe hizo, michezo mbalimbali ilifanyika, ikiwamo riadha, mbio za mita 100, 200 na 400 kwa wanawake na wanaume.

Pia, kulikuwapo michezo, mipira wa miguu, mikono, voleboli, kukimbia na magunia, kukimbiza kuku, kuvuta kamba kwa makundi yote ya wanaume na wanawake.

Katika sherehe hizo, Ofisa Udahili wa Cuhas, Mariam Nhaluke, anaeleza kufurahishwa na sherehe hizo, zinazohamasisha mazoezi kwa wafanyakazi kuimarisha afya zao.

"Michezo inaimarisha afya, watu wahamasike wasikae tu, wafanye mazoezi kama leo hii tulivyofanya, wengi hawapendi, sifa na umaridadi vinawaponza hasa wenye magari wanashindwa kuitumia fursa hiyo," anaesma' Nhaluke.

"Mganga hajigangi ni msemo uliopo. Hivyo, daktari, muuguzi na wengine katika idara ya afya, hawawezi kujiganga wenyewe wafanya mazoezi na michezo kuimarisha afya zao.

"Ila wakati mwingine kazi zinawabana wako kimakundi hiyo nayo ni moja pia ya changamoto walizo nazo," anasema Nhaluke.

Katika tukio hilo, ofisa huyo alishiriki katika mbio za mita 200, akiibuka kuwa miongoni mwa vinara. Ni sherehe zilifana kwa kukamilika, umma ukijumuika kwa vinywaji vya kila aina, kisha zawadi kwa wafanyakazi.

AFYA

AFANDE POLISI JINSIA:

# Kamanda Muslim: Nahisi mwisho wa mwaka huu Polisi tutapumua na ajali

• Vifo vinakomeshwaje? Sheria, kanuni zaja



Hali halisi za ajali barabarani zinavyochangia madhara katika afya za binadamu. **PICHA ZOTE: MTANDAO**.

**Na Yasmine Protace,** MOSHI

KUNA tathmini kutoka kwa Kamanda Polisi wa Usalama Barabarani, Fortunatus Muslim, anayasema uchumi wa kati na maendeleo ya viwanda, pia uhamasishaji uwekezaji na utalii nchini haufikiwi, pasipo kupungua ajali kitaifa.

Akizungumza katika mafunzo ya siku mbili jijini Moshi kwa wanahabari 40 walionolewa kuhusu uandikaji habari za usalama barabarani, chini ya usimamizi wa Shirika la Afya Duniani (WHO), Kamanda Muslim anadokeza mafanikio.

Kamanda huyo anatoa mfano, katika kipindi cha saa 24 tarehe mbili kuamkia tatu mwezi uliopo, hapakuwapo na tukio lolote la ajali lililoripotiwa, ikiwa ni kiashiria cha ujumbe kwamba, suala la usalama barabarani limeanza kuzingatiwa, ikiendana na matumizi sahihi ya vyombo vya moto.

Kamanda Muslim, anafafanua kimataifa kwamba ajali ni janga duniani na hasa katika nchi zilizopo Kusini mwa Jangwa la Sahara, akirejea takwimu za WHO anayoieleza: "Kila mwaka watu wapatao milioni 1.3 duniani hufariki kwa ajali barabarani."

Muslimu anaeleza jitihada zinazochukuliwa ni pamoja na upunguzwaji ajali hasa katika kipindi kuelekea mwisho wa mwaka na ndio falsafa inayopaswa kuendelezwa katika kipindi kilichopo na baadaye.

Mkuu huyo wa Polisi Usalama Barabarani nchini, anatoa tahadhari kwamba, kwamba hatosita kuwachukulia hatua madereva wavunjaji sheria na hatima yao itakuwa mahakamani.

> **Hivi sasa maono ya sheria ya usalama barabarani inayopendekezwa ni kwamba, lazima ikamilike kwa kuwa na alama zinazoonyesha upitaji vigezo mbalimbali vya udhibiti ambavyo hadi sasa havipo kisheria, sambamba na adhabu kali zinapokiukwa.**






Fortunatus Muslim, Kamanda wa Polisi, Kikosi cha Usalama Barabarani. **PICHA: YASMINE PROTACE.**

Pia, anavipongeza vyombo vya habari vilivyotoa mchango mkubwa kuielimisha jamii katika masuala ya usalama barabarani.

Msimamizi wa Sheria wa Polisi Kikosi cha Usalama Barabarani, Mrakibu Deus Sokoni, anakumbusha kosa la kisheria kwa dereva mmoja kuendesha basi la abiria kwa zaidi ya saa nane kutoka mkoa mmoja, kwenda mwingine.

Mrakibu Sokoni, ambaye pia ni Mwenyekiti wa Usalama Barabarani kupitia mradi uitwao 'Road Safety' ulioko chini ya WHO, anatambulisha kosa lingine ni basi la abiria kutokuwa na stika zenye namba za polisi usalama barabarani wa mikoa nchini.

Anasema, kuwapo kwa namna hizo ni mahsusi inapotokea dharura, abiria anapata fursa ya kupiga simu, akirejea stika hiyo inayotamka 'funguka'na ina maelezo ya usalama, hata kuwaripoti madereva wanaokiuka sheria za barabarani.

Ofisa huyo wa Polisi Usalama Barabarani, anasema kuwa wameandaa mapendekezo ya kisheria, dhidi ya wakiukaji sheria, kama vile kuendesha gari huku anaongea na simu, faini nzito ikiangukia hadi Sh. 500,000. Fursa aliyopewa, ni kuegesha kando gari kuhudumia simu safari yake na kisha kuendelea na safari.

Anaongeza kwamba, hivi sasa maono ya sheria ya usalama barabarani inayopendekezwa ni kwamba, lazima ikamilike kwa kuwa na alama zinazoonyesha upitaji vigezo mbalimbali vya udhibiti ambavyo hadi sasa havipo kisheria, sambamba na adhabu kali zinapokiukwa.

Mrakibu Sokoni, anadokeza kuwapo kifungu cha sheria kinachotamka mamlaka ya Polisi usimamia Sheria ya Usalama Barabarani, leseni za usafirishaji,udereva na uvaaji wao wa sera, pamoja na wahudumu wengine na kumdhibiti dereva kutumia simu, gari linapokuwa safi.

Anasema Sheria ya Bima ya Usalama Barabarani, mbali an kuitaka kila gari inayotembea barabarani kuwa na bima, pia ili mtu apate haki katika ajali ya barabarani na chimbo cha moto, anapaswa kutimiza wajibu wa usalama wake na chombo husika na nyenzo ya kuzima moto wa dharura, inapotokea..

"Kifungu namba 80, 79, 77 kinampa mamlaka asikari kukagua gari mahari popote,:" anaeleza.

Inspekta Msaidizi wa Polisi Hamad Hoza, anasema katika suala la usalama barabarani, changamoto zaidi ipo kwa jamii ambayo ama haijui iko mbali na masuala ya bima.

Anasema, mtu akisema kuna baadhi ya

wenye magari walio wadanganyifu wakitumia bima bandia, akifafanua: "Mtu anapopata ajali, kupata haki yake inakuwa shida, kutokana na gari kuwa na bima bandia."

Hoza anasema, bado Polisi ina nafasi nyingi katika kufanikisha udhibiti wa aina hiyo dhidi ya ukiukwaji sheria, ikianzia na elimu kwa watumiaji magari kuhusu hasara zinazoendana na kukosa bima, mbadala wake ni jamii itazidi kupoteza haki zake za msingi.

Anasema, baadhi ya abiria nao wamejikuta, wakipoteza haki zao kutokana na kusafiri bila ya tiketi na ajali zinapotokea, mtu hapati haki zake.

Inspekta Hoza anatoa darasa kwamba, inapotokea mtu anapokata bima, anatakiwa aisome na kuelewa kilichoandikwa, ili atambue masharti yaliyowekwa kuendana nayo.

### MRATIBU WHO

Mery Cessy, ni Mratibu waUsalama Barabarani kupitia (WHO), anayesema mwaka 2016 mafunzo ya Usalama Barabarani yalianza kutolewa na mwaka huu jumla ya waandishi wasiopungua 40 wamepatiwa mafunzo hayo.

Aidha, Ofisa kutoka Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia Wazee na Watoto, Said Makora, anaishukuru WHO kwa kufadhili majukumu mbalimbali yha kiafya nchini.

Anasema, kwa sasa madaktari wamejiendeleza kitaaluma, huku serikali nayo ina mengi kuhusu afya ya mama na mtoto, huku akidokeza kwamba magonjwa yasiyo ya kuambukiza, matibabu yake yana gharama kubwa.

Makora anasema, serikali kupitia waziri mwenye dhamana afya, alizindua kinachoitwa 'Mtandao wa Magonjwa yasiyo ya Kuambukiza.'

"Katika kipindi cha mwaka wa fedha ujao, kipaumbele kitakuwa katika magonjwa yasiyo ya kuambukiza," anasema.

### WANAHABARI VS USALAMA

Mwanahabari Mwandamizi, Lawrence Kilimwiko, ambaye ni mdau wa usalama barabarani, anataja nafasi ya wataaluma wake ni kuandika habari za ajali kwa kina na sio kuishia anachokitaja kuwa 'juujuu.'

"Unajikuta ajali imetokea mwandishi badala ya kuandika kwa uchunguzi, anaandika habari za juujuu" anasema na kuongeza, kilichopo nyuma ya pazia, ni kuwapo madereva wanaoweka kando sheria zilizoopo na kufuata kisichokuwapo.

> **Katika kipindi cha mwaka wa fedha ujao, kipaumbele kitakuwa katika magonjwa yasiyo ya kuambukiza.**

Anasema, dereva wa gari anaona kabisa kituo cha mafuta wanakataza kuvuta sigara na kuacha gari inaunguruma, lakini wao wanaenda mahali hapo wanakikuka hayo. Ni hali ya kukaribisha hatari.

Kilimwiko, anachangia hoja ya katazo la dereva kuingea na simu, tatizo bado lipo sana na ukiukwaji wa agizo hili la kisheria iko juu kwa madereva.

Anaenda mbali, akiwarejea abiria kutoendana na jitihada za polisi kutaka abiria kufunga mkanda, mfano hai ni katika magari ya wanafunzi mengi yanakiuka kwa kutofunga mikanda.

Kuhusu bodaboda, analitaja kuwa ni tatizo kubwa katika kukuka masharti na sheria mbalimbali za usalama barabarani, mfano hao ubebaji abiria zaidi ya mmoja maarufu 'mshikaki.'

# Msaada njiti aliyezaliwa bila mkono, aundiwa wa bandia

**London,** UINGEREZA

WAKATI mtoto alipozaliwa wiki nane kabla ya siku zake za kuwa nje ya tumbo la mama kutimia, sehemu kubwa ya mkono wake wa kushoto ulikuwa unapotea.

Wazazi wake, Gemma Turner na Chris Scrimshaw, kutoka Calderdale huko West Yorkshire, nchini Uingereza walifadhiliwa kiasi cha Pauni za Uingereza 16,000 kwa ajili ya matumizi yake binafsi.

Wakati wa kampeni hizo, ndipo Ben Ryan, kutoka eneo la Menai Bridge on Anglesey, alipokuja kumbunia mkono Jacob, ambaye sasa ana umri wa miaka mitano.

Ryan hakuchelewa, alianza kazi hiyo ya kubuni na kutengeneza mkono wa mtoto wakati akiwa na siku 10 tu. Ni hatua iliyomfanya aache kazi yake ya ualimu wa saikolojia na akaanzisha kampuni yake, ambayo sasa ina miaka miwili na nusu, akiita 'Ambionics' na mteja wake wa kwanza ni mtoto Jacob.

Ryan, amekuwa akifanya kazi karibu na familia ya mtoto huyo, ili kupatia mkono mzuri na familia hiyo, ilitaka kiwiko cha mkono ambacho kitawekwa sawa sehemu itakayomwezesha kumrahisishia afanye shughuli mbalimbali, pasipo shaka.

Ryan anasema, mkono huo umebuniwa kwa namna ambayo inampa urahisi Jacob kuukunja na aliutengeneza kwa ajili ya kufanya kazi kama mkono wa kawaida.

Lakini, upande wake wa pili wa Jacob, jambo la muhimu kwake ilikuwa rangi ya kijani ambayo alijiona shujaa.

"Kile nilichokitengeneza ni matakwa ya Jacob, mtoto huyo alitaka mkono mkubwa na hivyo huo mkono aliotengeneza ulikuwa sahihi kwake," anasema Ryan.





Mtoto Jacob Turner, akifurahia mkono wake bandia. **PICHA: MTANDAO**

Anaongeza kwamba, kuna wakati anamvalisha mkono huo kwa matarajio na anaongeza:"Sasa anaweza kumkumbatia kaka yake na kumpapasa kwa mkono wake."

Mama yake anasumulia hali ilivyo kwamba, Jacob alifurahia sana kuvaa mkono wake mpya na haimsumbui kuonekana kuwa tofauti na watu wengine wote na jambo lililobaki kwake ni kuzoea kutumia mkono huo.

Wakati wanachangisha fedha kwa watu, mtu ambaye hawamfahamu alitoa pauni za Uingereza alikuwa anaumwa sana na asingeweza kumaliza kwa kile alicho nacho.

Mwanzoni, Gemma aliona ugumu sana kuomba fedha kwa watu ambao hawajui ili kumtibia mwanae. Ryan anafafanua:"Familia hii haikuwa na bahati ya kupata msaada wa kumsaidia Jacob. Hakuna mtu ambaye alijitokeza na kitu ambacho kingeweza kumsaidia Jacob. **BBC**

AFYA

USHUHUDA UNAOSIKITISHA...

# Mama wa njiti wanne asimuli mazito, milima na mabonde

**NA CHRISTINA** MWAKANGALE

• Akatizwa mazikoni, aelekea wodini • Saa 24 ahamia Kenya mfuko mtupu • Miezi 4 na mume walea 'kangaroo' • Leo: Afy njema, deni zito hakuna • Daktari aliyezaliwa njiti, leo abob



Mama wa watoto njiti katika mkutano wa kuadhimisha siku yao. **PICHA ZOTE: MTANDAO.**

KATIKA watoto wanaozaliwa kuna kundi limaloitwa Njiti. Kwa mujibu wa jarida na Faty News, hao ni wanaozaliwa kabla ya kutimiza wiki 37, tangu tarehe ya kwanza mama kuona hedhi yake ya mwisho, bila ya kujali uzito aliyozaliwa nao.

Kwa kawaida mtoto anaweza kuishi vizuri nje ya mfuko wa uzazi, baada ya kutimiza umri wiki 37 na kuzaliwa kwake kuanzia muda wowote kati ya wiki 37 hadi 42.

Baada ya hapo, inaelezwa kitaalamu 'mimba imepitiliza muda' na juhudi za kitaalamu kumuwezesha mama huyo kujifungua huanza mara moja.

Kimatafa, kila ifikapo Novemba 17 kila mwaka dunia huadhimishwa Siku ya Watoto Njiti na takwimu zinaonyesha wastani wa watoto milioni 15 wanazaliwa kutoka kundi hilo na kati yao, milioni moja hufariki, kutokana na sababu mbalimbali zikiwamo za kuzuilika.

**BINGWA 'BABU NJITI'**

Bingwa wa kuhudumia watoto njiti kutoka MNH, Dk. Augustine Massawe, anasema wazaliwa hao wa uzito wanakuwa katika hatari ya kupoteza maisha ndani ya dakika 10 wanapozaliwa, iwapo hawatakingwa na baridi nakupata maradhi au niumonia.

Dk.Massawe anasema kila mwaka watoto 260,000 huzaliwa nchini wakiwa na uzito pungufu, kutokana na sababu mbalimbali za kipindi cha ujauzito, ikiwamo maradhi.

Anasema duniani kuna watoto milioni 13 njiti, wanaozaliwa barani Asia na Afrika na uzazi mapema ni sababu kuu.Dk.Massawe anaendelea:

"Asilimia 20 ya kinamama wanaozaa watoto hawa wana umri mdogo.

"Nimefanya kazi hapa Muhimbili kwa miaka mingi nimehudumia binti wa miaka 15 kazaa njiti. Nimepewa jina la 'Babu Njiti.'Mimi nilizaliwa njiti mama yangu aliniambia hivyo."

Anasema serikali iliposema binti kuolewa ni kuanzia miaka 18, kwake ina na ujumbe chanya a kupunguza vizazi njiti na vifo.

Dk. Massawe anataja vyanzo mtoto kuzaliwa kabla ya muda, mjamzito anapougua malaria, presha, kifuka kikuu na mkojo mchafu (UTI), kisukari, anemia, mapacha, uzazi wa mapema na lishe duni.

Pia, anasema kuna sababu ambazo kiasili hazijulikani na kumfanya mtoto atoke tumboni kabla ya muda.

Anajumuisha:"Tanzania kinamama wengi wanazaa watoto wenye kilo tatu wakiwa na wiki 34 ya mimba. Akizaliwa wiki 28 ujue mtoto atakuwa na kilo moja. Hii ni hatari, anatakiwa azaliwe hospitali 'wata-treat' (kushughulikia) vizuri. Akizaliwa nyumbani, akipigwa na baridi anafariki," anasema.

> **Nimefanya kazi hapa Muhimbili kwa miaka mingi nimehudumia binti wa miaka 15 kazaa njiti. Nimepewa jina la 'Babu Njiti.'Mimi nilizaliwa njiti mama yangu aliniambia hivyo.**

**MALEZI MTIHANI**

Suala la kulea wanaozaliwa kabla ya siku kutimia, lina matatizo makubwa inayowafanya kinamama waliojifungua kutumia muda mrefu kulea, gharama, kubwa, pia wanapoteza kazi na fursa za kiuchumi.

Hospitali wanawekewa vifaa maalum vya malezi kwa wastani wa miezi miwili hadi mitatu, ili waongezeke uzito kwa kuzingatia miongozo ya kitaalamu.

Aidha, Tanzania inatajwa kuwamo katika nchi ambazo shida hiyo inachangia vifo zaidi kwa watoto wachanga na Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH), inasema asilimia 13 ya watoto wanaozaliwa kila mwaka wana uzito pungufu - njiti, hivyo kuongeza vifo vya watoto wachanga.

**SIMULIZI MAMA NJITI**

Beatrice Mbawala (43),ni mama aliyekaa nyumbani miezi nane, ikiwamo miwili hospitalini baada ya kujifungua watoto mapacha wanne njiti, mnamo Januari 29 mwaka juzi,

Akizungumza katika kongamano la Siku ya Mtoto Njiti Duniani mwaka huu huko MNH, ambalo liliwakutanisha kinamama zaidi ya 50 waliojifungua njiti, kuelezea magumu yaliyowafika kulea njiti, anaanza kwa kuitaka serikali kubadili sheria ya likizo ya uzazi, itoe fursa ya miezi sita badala ya miezi mitatu ya sasa.



Watoto njiti nda... ya chum... chao maalum... hospital...

Beatrice, ambaye kabla ya kupata watoto hao, miaka 16 ya ndoa yao hakupata mtoto na alipata wa kwanza mwaka 2015 na kisha ndio akapata mapacha mwaka 2017.

Anasema, simulizi ya kuwa na njiti ilianza alipojifungua kwa upasuaji akiwa na mimba ya wiki 29, kutokana na matatizo ya kiafya yaliyomfika.

Mama huyo anasema, watoto hao wanne walikuwa na uzito mdogo, wa kwanza alikuwa na kilo 1.4; wa pili kilo1.33; wa tatu kilo 1.3; na wa nne kilo 1.2.

**ALIKOPITIA**

Beatrice anasimulia kwamba, kabla ya kujifungua, alipatwa na matatizo mbalimbali ya ujauzito, ikiwamo kupumzishwa hospitalini na kukaa nyumbani bila kufanya shughuli yoyote kwa miezi kadhaa.

"Nilipojifungua watoto wanne njiti niliathirika kisaikolojia. Hata kabla ya kuwaona nilijua namna walivyo na changamoto za watoto niliwashuhudia kwa ndugu zangu walizaa njiti, Nilifikiri sana," anasema, Beatrice, ambaye ni katibu Tarafa katika Manispaa ya Ubungo, Dar es Salaam, anaeleza aliambiwa akawaangalie watoto wake wakiwa kwenye chumba cha joto, siku mbili baada ya kufanyiwa upasuaji MNH.

"Niliambiwa niwe nawakamulia maziwa yangu. Hawakuweza kunyonya wenyewe, lakini kutokana na 'stress' nilizokuwa nazo hayakuweza kuwatosha walihitaji mililita tano kila mmoja," anasema Beatrice.

Ni jambo lililomfanya atafute mfadhili baada ya kushauriwa, ili amsaidie kuwahudumia watoto wake, kuwanunulia dawa ya kukumaza mapafu, vifaa tiba na kumlipia gharama za kukaa hospitalini.



Kinamama wakiwa wamewabeba watoto wao njiti katika mtindo wa Kangaroo.



Mtoto Njiti akinyweshwa maziwa.

"Gharama za chakula, dawa na vifaa tiba, likizo ya uzazi. Maisha ya watoto kwa asiyemudu gharama yapo hatarini na wengi huwafanya wasiweze kulipia gharama kwani hushindwa kufika hospitalini.

"Ukienda hospitali za binafsi 'pre-mature'ni gharama kubwa zaidi kwa siku ni milioni 1.5 lakini hapa MNH ni kama sh 150,000 hadi 200,000 kwa siku sasa piga hesabu kwa miezi utakayokaa hospitalini," ananukuu maelezo.

**WATOTO KUUGUA**

Beatrice anasema mapacha wawili kati ya wanne waliugua kila mara na ilifikia wakati wakahamishiwa Chumba cha Uangalizi Maalumu (ICU) na wakati huo huo yeye akitakiwa kubaki na wengine wawili katika wodi nyingine.

"Fikiri niilijigawaje mtu mmoja ingawa mume wangu alinisaidia. Nilitakiwa niwabebe kwa mtindo wa 'kangaroo' watoto wanne kila siku, kila mmoja kwa zaidi ya saa nane, nikamue maziwa,niende ICU kuwaona wale wawili wanaendeleaje," anasema Beatrice.

Anasema, pia mumewe alishiriki katika uwajibikaji hui wa 'kangaroo' unaotumiwa kuwapa joto watoto njiti kwa kuwabeba kifuani mwa mama zao.

Ni mfumo MNH wameiga kutoka kwa mnyama kangaroo, ambaye muda wote humhifadhi mtoto wake katika mfuko wake wa asili, uliopo nje ya tumbo lake.

Beatrice anataja shida za watoto wake, mmoja katika moyo na mwingine alishindwa kupumua vizuri kutokana na mapafu kutofanya kazi ipasavyo.

"Nimepitia mengi. Malezi ya hao watoto, mmoja alifariki tena mwenye uzito mkubwa. Niliumia sana na kukata tama, nikajiuliza sembuse hawa wenye uzito mdogo 'wata-survive' (watashi). Kuna wakati nilimwambia daktari iwapo mwanangu mwingine atafariki na mimi nitakufa," anasimulia.

Huku akieleza kuathirika sana kisaikolojia na kiakili, anafafanua maisha yake:"Mimi ni mtumishi wa umma, likizo ya uzazi iliishia MNH. Nilikaa miezi miwili na nusu baada ya kujifungua.

"Niliporuhusiwa kutoka hospitali usiku watoto waliugua na kwenda kulazwa tena hospitali iliyokuwa jirani. Nashukuru bosi wangu alinielewa.

"Lakini, kuna baadhi ya kinamama wenzetu tuliokuwa nao wodini walipoteza kazi kutokana na kukaa nyumbani au hospitalini kwa muda mrefu, sababu utaendaje kazini na mtoto hajaongezeka uzito? Bado unatakiwa umbebe 'kangaroo style' kwa saa 24," anasema Beatrice.

**MTIHANI WA PILI**

Beatrice anasema, baada ya alirudi nyumbani baada ya miezi miwili na nusu MNH, kabla ya kurudi nyumbani alishauriwa kuzingatia usafi mahali ambako watoto hao wanalala, kwa kuwa ni rahisi kupata maambukizi.

Anasema, siku chache baada ya kuruhusiwa, mtoto mmoja aliumwa usiku na kumpeleka hospitali ya binafsi jirani na aligundulika ana maradhi niumonia na baada ya hapo siku mbili baadaye aliruhusiwa.

Mama huyo anasema, aliporudi nyumbani kutoka alikolazwa na mtoto mmoja, akakuta watoto watatu waliobaki nyumbani nao wanaumwa, akarudi nao wote tena hospitalini.

"Baada ya siku mbili mmoja alifariki. Wakati nipo kumzika huyu mmoja,nikaja kuitwa kutoka mazishini kwamba watoto niliyowaacha nyumbani kabla ya kwenda makaburini nao wanaumwa hali si nzuri. Niliacha mazishi," anasimulia

Anasema mume wake ilibidi alazwe na mtoto mmoja hospitalini na yeye akiondoka nyumbani na watoto wawili waliopata nafuu.

"Mmoja kati ya hawa watatu baada ya mmoja kufariki, mwingine aliumwa zaidi nikaambiwa tiba yake ni shida ya mapafu ni ngumu kutibiwa hapa nchini. Wakati huo nilihamishiwa hospitali ya Aga Khan," anaeleza.

Beatrice anaeleza, baada ya ushauri kutoka kwa madaktari, ilimpasa atafute pesa mtoto wake ahamishiwe hospitali ya Aga Khan iliyoko Nairobi, Kenya kwa matibabu zaidi.

"Sikuwa tayari kumpoteza mwanangu mwingine ilinigharimu karibu Sh, milioni 100 matibabu. Nililipiwa na mfadhili shirika la msaada," anasema na alitakiwa atafute nauli ya ndege kwenda Nairobi ndani ya saa 24 kumtibu mtoto aliyekuwa na hali mbaya.

"Ndege ya kukodi kutoka Dar-Nairobi niliambiwa 'flying doctors' ni sh milioni 30 wao wanabeba mgonjwa, mama na wahudumu kwa bei hiyo.

"Kwenye akaunti benki nilikuwa nina milioni saba tu nilichanganyikiwa. Nilitamani hata nife. Bahati nzuri mume wangu alikopa mkopo wa zaidi ya Sh. milioni 10 na marafiki walituchangia hadi ikafika milioni 40," anaeleza

**MASHINE TATIZO**

Anasema baada ya pesa ya usafiri kupatikana, changamoto ilikuwa mashine ya kupumulia mtoto ambayo gharama yake ikikodiwa Sh. 200,000 kwa siku.

"Nilichanganyikiwa zaidi. Ilinibidi tutafute usafiri mwingine wa ndege wenye bei nafuu ili tuokoe pesa tukodi mashine ya kupumulia," anasimulia Beatrice.

Anasema, walikabiliwa na mtihani mwingine ndege zote zilikataa kuwabeba na mtoto mgonjwa mwenye hali mbaya, Precision Air pekee ndiyo iliwakubalia kwa bei ya safari za kawaida, Sh. 500,000 kwa abiria mmoja, huku akipata msaada wa mashine ya kupumulia kutoka kwa mtu.

**MAISHA KENYA**

Anasema, walipokuwa wanaendelea na matibabu jijini Nairobi, waliona vyema na mume wake wakatafuta nyumba ya kupanga kupunguza gharama za kukaa hotelini.

"Mtoto aliendelea vizuri na madaktari baada ya kumchunguza mwanangu waliniambia haumwi chochote, zaidi walimwekea 'carnula' kichwani. Basi tuliruhusiwa baada ya siku kadhaa," anasimulia.

Anasema waliendelea kuishi huko hadi watoto wake walipofikisha uzito wa kilo 2.5, mwingine kilo 2.7 na watatu kilo mbili, ndipo waliporudi Tanzania.

**USIKU & MCHANA**

Anasema malezi ya watoto hao, yaliifanya familia yote nyumbani kupeana zamu na mumewe pamoja na walezi wengine.

"Wengine walilala mchana ili usiku wakeshe yaani kwa miezi minne mfululizo sijawahi kulala zaidi ni kujiegesha tu," anasema Beatrice, hali iliyomfanya maziwa ya kuwanyonyesha watoto yapungue sana.

Anasema, alishauriwa ni lazima kutumia maziwa ya kopo, ingawaje sio sahihi zaidi kwa watoto njiti. Mama huyo anaendeleza simulizi:

"Niliagiza maziwa ya kopo kutoka Uingereza ilinigharimu sh milioni 1.5 kwa mwezi bado pampers sh 150,000 kwa mwezi achilia mbali nguo zao hazipatikani madukani, zaidi nilinunua mtumbani nguo zao ni ndogondogo sana."

**KURUDI KAZINI**

Beatrice anasema baada ya miezi nane ya changamoto, tofauti ikiwamo kupoteza mtoto, pesa kutumika na kumuachia madeni aliwashukuru waliomsaidia kugharamia huduma zote.

"Mimi nilipata msaada na shirika lakini gharama za malezi kwa 'Pre-mature' ni kubwa sana," huku akitambulisha, hivi sasa watoto hao mapacha watatu, Peter, Paul na Precious wana afya nzuri wakiwa na umri wa miaka miwili na nusu na dada yao akiwa na miaka minne.

"Gharama za chakula, dawa na vifaa tiba, likizo ya uzazi. Maisha ya watoto kwa asiyemudu gharama yapo hatarini na wengi huwafanya wasiweze kulipia gharama kwani hushindwa kufika hospitalini.

"Dawa ya kusaidia kukomaza mapafu ya watoto ni ghali na hadi kutoka hospitalini hapo huduma na gharama zote hufikia milioni sita hadi 10, kutegemea na miezi mama aliyokuwa na mwanawe hospitalini," anaeleza Beatrice.

"Je, ni haki wakinamama kuwa na lishe duni? Jamii inatakiwa ichukue hstua, asilimia kubwa walio na kipato duni wanajifungua njiti, sababu ya lishe duni," anasema.

***Soma zaidi Alhamisi inayofuata.***

AFYA

# Kulala na kuamka kunavyoathiri ufanyaji kazi wa mtu siku nzima



Watu wakiwa usingizini. **PICHA ZOTE: MTANDAO.**

**Na Michael Eneza**

KIMAISHA yapo mambo ambayo watu wanapaswa kujifunza maishani, kwamba bila ya kuwa na mpangilio halisi wa nini kinatakiwa kufanyika nje ya mazoea ya kila siku.

Pia, wana wajibu wa kuboresha mazoea ya hapa na pale, pindi wanahisi haja ya kufanya hivyo. Mengi yanagusa hisia binafsi za jinsi mtu anavyojisikia, kuwa na raha au kutokuwa na raha.

Ni masuala ambayo kimsingi hayana mpangilio wa pamoja kwa jamii ya binadamu, au kundi lolote la watu. Hivyo, licha ya kuwa masuala muhimu katika afya na tija kwa jumla, hayana utaalamu katika mazingira ya kawaida.

Mojawapo ni uhusiano kati ya mtu anavyolala na kuamka na linavyoathiri shughuli zake za kila siku.

### KULALA & KUAMKA

Wakati wa kulala na kuamka, unatawaliwa na mandhari tofauti ya hali ya hewa, mahali alikojiegesha mtu na wakati wa kuamka. Hali hiyo ina kawaida ya kuibadilika kulingana na muda mtu huyo aliyelala anapoamka.

Wakati wa kulala huwa kunaweza kiwa na ama joto au kinyume chake baridi. Inapokuwa joto, mwili unakataa kufunikwa na unafurahia baridi ili usingizi upatikane na katika mandhari yenye raha zaidi.

> Watu wanatofautiana kwa wanachokifanya. Wasiohitaji kulala muda mrefu, huo na kawaida, ila bado inajitokeza ukweli wa haiba, kupungukiwa uchangamfu kwa wakati fulani.



Mtu anapolala hivyo hadi asubuhi au kufika wakati wa kuamka, bado hawezi kufanya kazi. Nguvu ya kuamka inakuwa ya 'soda' ikitokana na uchangamfu wa 'juu juu' kupata baridi nzuri kuifurahia, lakini ndani kuna udhaifu mkubwa wa joto.

Hapo ina maana mwili ulihitaji ukamilishe majukumu ya kujijenga upya, wakati akili au ubongo upo mapumzikoni, kwa sehemu kubwa. Hiyo maana yake nini?

Inabidi mtu aamke muda wowote baada ya kulala akifurahia upepo au baridi, kisha ili awe ametulia, anahitaji kuwa na joto kiasi zaidi, ajifunike mwili wote, pamoja uwe na kuwa mpangilio wa joto unaofanana.

Hapo ndipo hata mipangilio ya mwili kupitia utumbo wake, utaweza kusaga chakula na ukakaa vyema, kwani wakati huo mwili unafanya kazi taratibu zaidi, unahitaji pia joto.

Inaelezwa, endapo mtu atapitisha muda wa kufurahia baridi na akashindwa kujifunika mpaka asubuhi anapomaka na akaendelea na shughuli zake kwa muda, hiyo inanagukia kuwa 'nguvu ya soda' aliyoamka nayo.

### KUSINZIA MCHANA

Baada ya hapo ni kwamba, uchovu uliojificha utajitokeza na haipiti muda mtu anaanza kusinzia. Baadhi wanadhani sababu labda ni 'tatu baridi' za jana, kumbe ni kufurahia usingizi na upepo uliopo hadi kunakucha.

Ni mazingira yanayomfaa asiyelala, lakini anaamka mapema zaidi. Mtu wa namna hiyo anaridhika kuwa amelala na anajisikia vizuri. Ziada ya hayo katika afya ya usingizi ni matokeo ya mazingira ya kazi.

Watu wanatofautiana kwa wanachokifanya. Wasiohitaji kulala muda mrefu, huo na kawaida, ila bado inajitokeza ukweli wa haiba, kupungukiwa uchangamfu kwa wakati fulani.

Historia inaendelea kuonyesha, watu walilala kwa saa nne tu kwa siku. Kwa wengi, siyo ngumu endapo inatokea kwa nadra na si rahisi kugeuzwa hali ya kawaida.

Ina maana pia kuna kitu kinachoongezwa katika mwili kujazia muda wa usingizi. Siyo rahisi kwa mtu kusema, ana mbadala katika maisha ya kila siku, lakini kuna ukweli wa kiafya kwamba, ziko njia za kupumzisha mwili dhidi ya usingizi.

Ni njia ambazo kwa kiasi fulani na zinaweza kuchukua nafasi kwa kuzingatia baadhi ya mambo na mojawapo ni kutumia baadhi ya vinywaji, mfano maziwa na chai na daima si vilevi. Pia, yako maeneo mengine ambayo hayatajwi kwa umuhimu wake kiafya, ila kama burudiko ya akili na utashi tu, ikiwa ni sehemu ya mazoea.

Katika taaluma ya 'metabolism' (mchanganuo wa kuishi na kutumia vifaa mwilini), hakuna kinachogusa mwili ambacho hakiingii katika mizania hiyo.

Mojawapo ni muziki, ambao kwa kiasi fulani unaendana na kinywaji kama mvinyo. Licha ya kuhusiana na mishipa ya fahamu zaidi, kuliko ile ya kupokea na kuyeyusha virutubishi na athari zake katika ufahamu, utulivu au msuguano mwilini. Kuburudisha mishipa kunaondoa uchovu.

Yako maeneo yanayofanana na hayo, ambako kuna tabia ya watu kutofautiana katika kupendelea kitu kimoja au kingine. Mojawapo ni kuoga au kutokuoga, kabla ya kulala. Baadhi ya watu wanapoteza usingizi, pale wanapooga, bila ya kufanya shughuli nyingine kuleta joto kiasi fulani au uchovu.

Siyo rahisi kusema, idadi ya wahitaji wa kuoga kabla ya kulala, ili wapate usingizi mzuri na wangapi wanapoteza endapo wataanza kuoga.

Mtu anachoweza kuhisi ni katika maeneo baridi, yanapunguza haja ya kuoga kila wakati na kwa eneo la joto, kuoga ni jambo ambalo halina ubishi mtu anapoamka asubuhi, siyo akienda kulala.



# Wauza gesi ya kupikia wapewa mbinu soko

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

MAMLAKA ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (Ewura), imewashauri wafanyabiashara wa gesi ya kupikia kuchangamkia fursa ya soko la bidhaa hiyo katika mikoa ya Kanda ya Nyanda za Juu Kusini kwa madai kuwa soko hilo halijatumika ipasavyo.

Ushauri huo ulitolewa jijini Mbeya na Meneja Uhusiano wa Ewura, Titus Kaguo, wakati wa mafunzo maalumu ya taratibu za uuzaji wa gesi hiyo kwa wafanyabiashara na wasambazaji wa gesi katika mikoa hiyo.

Kaguo alisema Kanda ya Nyanda za Juu Kusini ni ya pili kwa ukubwa nchini, lakini matumizi ya gesi ni asilimia nane pekee, hali ambayo alidai inaashiria kuwa wananchi wa mikoa hiyo wanakata miti kwa wingi kwa ajili ya kuni na mkaa.

Aliwashauri wafanyabiashara kupeleka bidhaa hiyo kwa wingi na kutoa elimu kwa wananchi juu ya umuhimu wa kuitumia bidhaa hiyo badala ya kuni na mkaa kwa maelezo kuwa bidhaa hiyo ni bei nafuu zaidi kuliko mkaa.

Alisema kitendo cha wananchi kuendelea kutumia kuni na mkaa kinasababisha uharibifu wa mazingira hasa misitu, hivyo kuwa chanzo cha mabadiliko ya tabianchi ikiwamo kupungua kwa kiwango cha mvua tofauti na ilivyozoeleka.

"Kanda ya Mashariki ambayo ni ndogo kuliko ukanda huu wanatumia asilimia 50, Kanda ya Kaskazini wanatumia asilimia 25, lakini ukanda huu ni asilimia nane pekee, sasa tafsiri yake ni kwamba huku bado kuna fursa kwa wafanyabiashara," alisema Kaguo.

Aidha, Kaguo aliwataka wauzaji wote wa gesi nchini kuwa na mizani ya kupimia uzito wa bidhaa hiyo kwa maelezo kuwa kanuni zinataka, hivyo na kwa mfanyabiashara ambaye hatafuata utaratibu huo adhabu yake ni faini ya mpaka Sh. 5,000,000.

Alisema lengo la utaratibu huo ni kuepuka wafanyabiashara kuwaibia wananchi kwa kupunguza kiwango na hivyo baada ya muda mfupi inaisha.

Ofisa Mwandamizi wa Huduma kwa wateja Kanda ya Nyanda za Juu Kusini, Muhiba Chakupewa, aliwataka wananchi kutumia gesi kupikia badala ya kuni na mkaa kwa maelezo kuwa ni bei nafuu na inachukuliwa kwa urahisi.

Alisema bei ya mkaa ni kubwa kwa zaidi ya Sh. 600 kuliko bei ya mkaa kwa maelezo kuwa mkaa unaonunuliwa kwa Sh. 2,400 ni sawa na gesi inayonunuliwa kwa Sh. 1,800.

"Tumeamua kutoa mafunzo haya kwa sababu tumebaini kuwa wengi wa wafanyabiashara hawa hawafuati taratibu za uuzaji wa gesi, na tunawataka wakitoka hapa wakawe walimu wazuri kwa wateja wao ili hata matumizi ya bidhaa hii yaongezeke," alisema Chakupewa.

Mmoja wa wafanyabiashara hao, Hamoud Said ambaye ni Mwakilishi wa Kampuni ya Gesi ya Oryx, alisema mafunzo hayo ni muhimu kwao na kwa wateja wao kwa maelezo kuwa gesi isipotumika vizuri ni hatari.



Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Albert Chalamila, akiagana na Mwenyekiti wa Bodi ya Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya NHIF, Anna Makinda, baada ya mkutano wa uzinduzi wa kampeni ya kuhamasisha wananchi kujiunga na bima ya afya kupitia mfumo wa vifurushi. **PICHA: NEBART MSOKWA.**

## Dawa wanaoharibu miundombinu shule

**Na Nebart Msokwa,** CHUNYA

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi), Selemani Jafo, amesema kwa sasa mwanafunzi yeyote atakayeharibu miundombinu ya shule mzazi wake atawajibika kulipa ili kukomesha vitendo hivyo.

Waziri Jafo aliyasema hayo alipotembelea Shule ya Sekondari ya Kiwanja iliyopo katika Wilaya ya Chunya na kukagua maendeleo ya ukarabati wa mabweni matatu ya shule hiyo ambayo yalichomwa na wanafunzi hivi karibuni.

Alisema vitendo hivyo vinakwamisha maendeleo ya sekta hiyo kwa maelezo kuwa serikali inatumia fedha nyingi kwa ajili ya uendeshaji, hivyo ni lazima ichukuwe hatua kali za kudhibiti uharibifu huo.

Alisema mbali na wanafunzi wa shule hiyo kufanya uharibifu huo, pia kuna tukio lingine la aina hiyo lilitaka kutokea katika Mkoa wa Morogoro ambako wanafunzi walitaka kuchoma shule mpya na wakadhibitiwa kabla hawajatekeleza.

Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Albert Chalamila, ambaye aliambatana na Waziri Jafo, alisema katika mkoa huo mbali na wazazi kuwajibika kulipa, lakini mwanafunzi husika ni lazima afungwe ili kuwa mfano.

Alisema katika tukio la wanafunzi wa shule hiyo kuchoma mabweni, waliamua kuwashughulikia ipasavyo kwa kuwacharaza bakora, kuwafunga na kuwaamuru walipe gharama za ukarabati.

Alisema ukarabati wa mabweni hayo umefanywa kwa fedha ambazo wanafunzi hao walilipa pamoja na baadhi ya wadau ambao walijitolea kuchangia kupitia harambee iliyoitishwa na Mkuu wa Wilaya.

Mkuu wa Shule hiyo, Elly Mnyarape, alisema wanafunzi hao kwa ujumla walilipa Sh. milioni 82 ambazo zimetumika kukarabati mabweni hayo.

# Mafanikio saba ya Hospitali Rufani Mbeya kwa miaka ninne

**Na Augusta Njoji,** MBEYA

KATIKA kipindi cha miaka minne ya serikali ya awamu ya tano, Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Mbeya imetaja mafanikio saba ambayo yamechangia kuwapo na huduma bora za afya na kuhudumia kinamama 600 kwa mwezi.

Imeelezwa kuwa mafanikio hayo, yamepaisha ukusanyaji mapato kutoka wastani wa Sh. milioni 45 - 60 na kufikia Sh. milioni 100 kwa mwezi.

Hayo yalielezwa na Mganga Mfawidhi wa Hospitali hiyo, Dk. Gloria Mbwile, alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari walioambatana na maofisa habari wa taasisi zilizopo chini ya Wizara ya Afya katika kampeni ya 'Tunaboresha Sekta ya Afya' inayolenga kuangalia mafanikio yaliyopatikana kwa kipindi cha miaka minne ya serikali ya awamu ya tano.

Alitaja mafanikio hayo ni upatikanaji wa dawa na vifaa tiba, ukarabati na ujenzi wa miundombinu, huduma za uchunguzi, huduma za mama na mtoto, utoaji wa huduma, mifumo ya usimamizi na uendeshaji wa hospitali, upatikanaji wa madaktari bingwa.

Alieleza hospitali imejitahidi kuhakikisha dawa kwa wateja zinapatikana kwa asilimia 100 na wamejenga duka la dawa la kuhudumia wagonjwa kutokana na mapato ya hospitali kwa kushirikiana na serikali.

Aidha, alisema katika uboreshaji miundombinu wanajenga jengo la upasuaji ambalo linatarajiwa kugharimu zaidi ya Sh. bilioni nne na wamepokea Sh. milioni 900 na ujenzi unaendelea.

"Pia tumepokea fedha kutoka serikalini kwa kushirikiana na mdau ambaye ni Global Fund tumepata Sh. milioni 190 ya kujenga jengo la huduma za haraka ujenzi huu utaanza mapema na sasa tupo kwenye maandalizi ya ujenzi huo," alisema.

Kuhusu huduma za uchunguzi alisema zimeboreshwa kwenye upande wa mionzi na X-Ray na wanatarajia kupata mashine ya kidigitali ya X-Ray hivi karibuni.

"Kwenye maabara vipimo vyote vinapatikana na tumekarabati maabara kwa ajili ya uchunguzi wa wingi wa Virusi vya Ukimwi ambapo maabara hii imeshakamilika kwa kushirikiana na serikali na wadau," alisema.

Alisema huduma za mama na mtoto zimeboreshwa ambapo kwa sasa madaktari bingwa wameongezeka kutoka wawili hadi wanne.

Alibainisha kwa mwezi wanahudumia kinamama 600 na inatokana na huduma kuboreshwa, upatikanaji wa dawa vifaa tiba na uchunguzi ambapo imesaidia kinamama hao kufika hospitalini.

"Tuna kitengo cha kuhudumia watoto wachanga ambacho kilianza mwaka 2017 kwa siku tunalaza watoto 35 na kipekee kabisa kutokana na kipaumbele cha wizara cha kuhudumia watoto njiti kwa mara ya kwanza tumehudumia mama aliyejifungua watoto wanne na wapo hai hadi sasa," alisema.

Akizungumzia utoaji huduma za afya, alisema wamefanikiwa kuboresha huduma na wana ofisa wa hospitali ambaye anapokea malalamiko na maoni kutoka kwa wananchi.

Alisema kwa sasa wana bodi ya ushauri ya hospitali hiyo ambayo awali haikuwapo na imesaidia kutokana na kuwa na wataalamu na kufanya kazi kwa karibu na hospitali.

Kadhalika, alisema kuna mafanikio makubwa kutokana na uboreshaji wa mifumo ambapo kwa upande wa fedha mfumo umesaidia ukusanyaji wa mapato kwa kiasi kikubwa.

"Huko nyuma kwa mwezi tulikuwa tunakusanya kati ya Sh. milioni 45-60, lakini kutokana na uboreshaji wa mifumo na miundombinu hospitali inakusanya wastani wa Sh. milioni 100 kwa mwezi na zimesaidia kuboresha huduma kwa kununua vifaa, dawa, ukarabati wa majengo, na tunajenga jengo la upasuaji wa macho kutokana na fedha zinazokusanywa," alisema.

"Tumeanzisha kliniki za kibingwa hasa kwa upande wa idara ya kinamama ni mafanikio makubwa kwenye kipindi hiki," alisema.



# TALGWU yakerwa wanasiasa wanaowadhalilisha watumishi

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

CHAMA cha Wafanyakazi wa Serikali za Mitaa Tanzania (TALGWU) kimeelezwa kukerwa na baadhi ya wanasiasa wenye tabia ya kuwawajibisha na kuwadhalilisha watumishi wa umma kwa kuwaweka mahabusu.

Akisoma risala ya TALGWU, Mkuu wa Idara ya Habari na Uhusiano Kimataifa wa TALGWU, Shani Kibwasali kwa niaba ya Katibu Mkuu wa chama hicho, Rashidi Mtima, alisema kuwa kwa sasa imeibuka tabia ya wanasiasa kuwadhalilisha watumishi wa serikali ya umma.

Shani, alisema kuwa kitendo cha wanasiasa hao kutumia madaraka yao vibaya wanawadhalilisha watumishi hao kwa kuwaweka mahabusu bila sababu za msingi na kutozingatia sheria zinazowapa mamlaka hayo ni kushusha heshima ya hadhi, na morali ya watumishi hata kwa kufanya kazi zao ipasavyo.

"Hivyo tunaiomba serikali yetu sikivu ambayo inawajali wafanyakazi wake, kukemea vitendo hivyo kuwaelekeza viongozi hao wanasiasa kuzingatia sheria, kanuni na taratibu za masuala ya nidhamu kwa watumishi. "Endapo italazimu mtumishi kuwekwa mahabusu kwa hofu ya uvunjifu wa amani basi matakwa ya kisheria yazingatiwe," alisema Shani.

Alisema kero nyingine ni kukosekana kwa miundombinu na huduma za msingi katika maeneo mapya yalipohamishiwa ofisi za halmashauri ili kusogeza huduma kwa wananchi.

Alisema watumishi wamehamishwa katika maeneo yao bila kuzingatia maandalizi ya kutosha, huku maeneo mengi hakuna majengo yenye hadhi ya ofisi, huduma ya maji, huduma ya kijamii, usafiri, umeme, nyumba za kuishi pamoja na huduma nyingine za msingi.

Shani akiendelea kutaja changamoto, alisema pamoja na serikali kuwarejesha kazini wanachama waliotolewa kwa kukosa cheti cha ufaulu wa elimu ya kidato cha nne ambao waliajiriwa kabla ya Mei 20 mwaka 2004 na kuahidi kulipa malimbikizo ya mishahara kwa miezi yote, lakini imepita miezi 20 sasa hawajalipwa.

Jambo lingine alisema ni wastaafu kutolipwa mafao yao kwa wakati jambo hilo si jema kwa watumishi hao.

Waziri wa Kilimo, Japhet Hasunga, akijibu risala ya Talgwu, alisema kuwa ni kosa kwa wanasiasa kuvuka mipaka kwa kuwawajibisha watumishi.

Alisema mwanasiasa anatakiwa kutambua mipaka yake ya kufanya kazi bila kuwadhalilisha watumishi na mtumishi anatakiwa kuwajibishwa kwa mujibu wa kanuni na sheria za utumishi.



Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Dk. Binilith Mahenge, akizungumza kwenye kikao cha Bodi ya Barabara cha Mkoa, jana. Kulia ni Katibu Tawala Mkoa wa Dodoma, Kesy Maduka na Mbunge wa Bahi, Omari Baduwel. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Kaya zenye vyoo nchini zaongezeka

**Renatha Msungu,** DODOMA

SERIKALI imesema jumla ya kaya zenye vyoo bora nchini zimeongezeka hadi kufikia asilimia 62.4 mwaka 2019 kutoka asilimia 34 iliokuwa mwaka 2015 kupitia kampeni maalum.

Kampeni hiyo ni 'Usichukulie Poa, Nyumba ni Choo' iliyoendeshwa miaka miwili na Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto.

Hayo yalielezwa na Waziri wa Afya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Ummy Mwalimu, katika kilele cha Wiki ya Usafi wa Mazingira kitaifa na mkutano wa maofisa afya wa mikoa, halmashauri na wadau uliofanyika jijini hapa.

Waziri Ummy alisema katika kipindi cha miaka miwili ya kampeni, kaya zenye vyoo bora zimeongezeka na zile kaya zisizokuwa na vyoo kabisa zimepungua kutoka asilimia 7.5 hadi asilimia 1.9 katika kipindi hiki cha miaka miwili ya kampeni hiyo.

Aidha, alisema kwa upande wa vijiji ambavyo kaya zake zote zina vyoo imeongezeka kutoka 743 hadi 4,311 na kwa upande wa taasisi wameweza kuboresha huduma ya maji na usafi wa mazingira katika vituo vya tiba 1,267 kati ya lengo la vituo 1,000 ambavyo walipanga kuvifikia.

"Haya si mafanikio ya kubeza na kimsingi ninapenda kuwashukuru wadau kwa kushirikiana na serikali kufanikisha kampeni hii, lengo letu ni kufuta kabisa kaya zisizokuwa na vyoo na kuongeza kaya zenye vyoo bora hadi asilimia 75 ifikapo Juni, 2021," alisema Mwalimu.

Alisema kwa upande wa maeneo ya kutupia taka ngumu serikali ina nia ya dhati ya kuboresha maeneo ya kutupia taka husuan madampo yaliyopo kwenye miji ili yawe ya kisasa.

Alisema uchafuzi wa mazingira utokanao na taka ngumu umeendelea kuwa changamoto katika maeneo ya mijini, hivyo serikali imejipanga kuongeza nguvu kwenye mamlaka za serikali za mitaa ili kuboresha miundombinu iliyopo katika mitaa nchini. Alisema serikali imeandaa mwongozo wa uwekezaji katika taka ngumu ili kuhamasisha uwekezaji na kuongeza jitihada za kuboresha usimamizi wa taka nchini, jambo ambalo anaamini litasaidia.

Waziri Ummy alisema utafiti mbalimbali unaonyesha kwamba nchi inapoteza takribani asilimia moja ya pato ghafi la taifa (GDP) kutokana na hali duni ya usafi na utafiti uliofanywa na Benki ya Dunia mwaka 2012, ulionyesha kila mwaka Sh. bilioni 450 zinapotea kutokana na madhara ya uchafu.

Kutokana na hilo, alisema wana kila sababu ya kupambana ili kuokoa kiasi hicho cha fedha ambacho hupotea.

# Wanahabari wafundwa ripoti CAG

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

MSEMAJI Mkuu wa Serikali, Dk. Hassan Abbas, amewataka waandishi wa habari nchini kuacha kutumia uchambuaji wa wanasiasa kuandika habari zinazohusu ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) badala yake wasome ripoti kwa makini ili kupata taarifa sahihi.

Akizungumza katika semina ya wanahabari na asasi za kiraia, Dk. Abbas, alisema taaluma ya habari ni moja ya nyenzo ya ulinzi wa taifa, hivyo wanapaswa kutoa habari zenye uhakika na mashiko kupitia ripoti kwa makini na si kupitia uchambuzi wa wanasiasa.

Alisema wanahabari wanapaswa kutumia kalamu zao vizuri kuhabarisha ili kuendeleza amani iliopo badala ya kuandika taarifa isio ya kweli na iliojaa uchochezi.

Dk. Abbas alisesema kuwa vyombo vya habari vinapaswa kutambua wajibu mpana wa taaluma hiyo katika kuelimisha jamii kwa kuwa taaluma hiyo ni adhimu na ina umuhimu katika taifa kwa sababu inahabarisha umma.

"Waandishi mnapaswa kujua umuhimu wa taaluma ya habari nimegundua wengi wenu ni wavivu wa kusoma ripoti na vitabu, mnapaswa kufanya hivyo ili kutoa taarifa zilizo kamili," alisema Dk. Abbas.

Alifafanua kuwa vyombo vya habari vinapaswa kujua umuhimu wa kuchambua sera ikiwamo kukosoa madudu yanayofanywa iwe katika sekta binafsi au umma, ili serikali ijue na kuchukua hatua.

"Taaluma ya habari ina wajibu wa kulinda amani na kutangaza maendeleo ya nchi, hivyo kukosoa mabaya yenye ukweli si tatizo... shida ni kuandika bila kuangalia pande zote,"alisema Dk. Abbas.

Kutokana na hali hiyo, aliwataka wanahabari kuwa makini na kazi wanazozifanya ili wasipotoshe jamii kwa sababu watu wanaiamini taaluma hiyo.

Aidha, aliwataka wanahabari kujijengea tabia ya kusoma kila wakati ili kuripoti vitu sahihi ambavyo vinajenga na si kubomoa kama wanavyofanya wengine, ambao wanaandika taarifa ambazo hazijaangalia pande zote husika katika ukweli wa taarifa hiyo.

Vilevile, alisema kuwa waandishi wa habari wengi wanakosa uelewa wa kuandika ripoti za ukaguzi wa hesabua za serikali kutokana na uvivu wa kusoma taarifa za kitaalamu katika ripoti za ukaguzi.



# Serikali yaandaa mfumo nyendo kesi udhalilishaji

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

SERIKALI ya Mapinduzi ya Zanzibar imesema inakusudia kuweka mfumo mzuri zaidi katika kufuatilia kesi za udhalilishaji wa kijinsia katika sehemu mbalimbali, vikiwamo vituo vya polisi.

Hayo yalisemwa na Waziri wa Uwezeshaji Wanawake, Wazee na Watoto, Mauldline Castico, wakati wa maadhimisho ya Siku 16 za Kupinga Ukatili wa Kijinsia mjini Unguja.

Castico alisema bado takwimu zinaonyesha matukio ya vitendo vya udhalilishaji wa kijinsia yamekuwa yakiongezeka siku hadi siku katika Visiwa vya Unguja na Pemba.

Alisema katika Mkoa wa Mjini Magharibi A kwa mfano, matukio 134 ya udhalilishaji wa kijinsia yametokea na katika Mkoa wa Mjini Magharibi B matukio 113 yameripotiwa mwaka huu.

Aliitaja mikakati inayotarajiwa kuchukuliwa kuwa ni pamoja na kuweka mfumo mzuri wa takwimu za matukio ya udhalilishaji wa kijinsia katika maeneo muhimu vikiwamo vituo vya polisi.

"Tunataka kuweka vizuri takwimu za matukio ya vitendo vya udhalilishaji wa kijinsia katika mfumo unaofahamika, zikihitajika zinapatikana zikiwa sahihi," alisema.

Castico alisema katika mikakati hiyo, wanakusudia pia kuzifuatilia kesi za udhalilishaji wa kijinsia zilizokwama katika sehemu mbalimbali vikiwamo vituo vya Jeshi la Polisi.

# Waitaka ZEC itoe elimu wapigakura

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WAKATI Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar (ZEC) inakusudia kuandikisha na kuhakiki taarifa za wapigakura kuanzia Januari 18 hadi Machi 4, mwakani, baadhi ya wadau wa uchaguzi wameitaka kutoa elimu mapema kwa wananchi.

Wadau hao pia wameitaka tume kutoa elimu kwa wananchi kuhusu upigaji wa kura ya mapema kwa wasimamizi wa uchaguzi wanaotakiwa kupiga kura siku moja kabla ya uchaguzi mkuu.

Wakizungumza katika mkutano kati ya wadau hao na ZEC, walisema elimu hiyo itakayotolewa itaepusha migogoro inayotokana na uchaguzi.

Seif Ali Iddi kutoka chama cha NCCR-Mageuzi, aliitaka tume hiyo kufanya tathmini ili kujua idadi kamili ya watakaopiga kura ya mapema kabla ya siku ya uchaguzi ili kuepusha malalamiko kutoka kwa wananchi.

Mdau huyo pia aliitaka tume kuwawekea ulinzi wataopiga kura hiyo ya mapema ili kuepusha machafuko yatakayohatarisha amani ya nchi na kuandika historia mbaya.

Mwenyekiti wa ZEC, Jaji mstaafu Hamid Mahmoud, alisema uandikishaji daftari la wapigakura wapya utajumuisha wale wote wenye sifa ya kupiga kura ambazo ni pamoja na kuwa na umri wa kuanzia miaka 18.

Alisema watahakikisha wanatoa elimu ya kutosha kwa jamii na wadau mbalimbali ili kuwa na ufahamu wa kina juu ya suala hilo.

Alisema tume hiyo kwa sasa imekuwa na uzoefu mkubwa wa kusimamia suala hilo na imejifunza kupitia maeneo tofauti ikiwamo mitandao na nchi mbalimbali.

Alisema tume kwa sasa iko katika mpango wa kununua vifaa vyote vinavyohitajika ili kufanikisha uchaguzi huo bila kuwapo usumbufu wowote.

Akiwasilisha mada kuhusu utaratibu wa kupiga kura ya mapema Zanzibar, Mkurugenzi wa Uchaguzi, Thabit Idarous Faina, alisema watahakikisha hakutokei udanganyifu wowote.

Alisema kutakuwa na daftari maalum lenye majina ya wapigakura na picha zao na kila atakayepiga kura kutawekwa alama kwenye jina lake na atapakwa wino maalum.

Aliwataja watakaopiga kura ya mapema kwa mujibu wa sheria kuwa ni pamoja na watendaji wa tume hiyo na vyombo vya ulinzi na usalama ambao watasimamia shughuli za uchaguzi.



Watanzania wanaoishi ughaibuni (Diaspora), wakila tunda la fenesi baada ya kutembelea shamba la Zanzibar Village Icon, la Mbuzini Wilaya ya Magharibi 'A', Unguja. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Spika abaini dawa ya ongezeko la talaka

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

NAIBU Spika wa Baraza la Wawakilishi Zanzibar, Mgeni Hassan Juma, ameitaka Ofisi ya Mufti Zanzibar kuangalia uwezekano wa kukifanya cheti cha mafunzo ya ndoa kuwa cha lazima kwa wanandoa ili kupunguza wimbi la talaka.

Amesema anatamani kuona cheti hicho kiwe ni cha lazima kwa wanandoa na asiyekuwa na cheti hicho asifungishwe ndoa kama ilivyo kwa upimaji wa Virusi vya Ukimwi (VVU).

Akizungumza katika ufungaji wa mafunzo ya ndoa ya awamu ya tano, kiongozi huyo wa baraza alisema vyeti vya mafunzo ya ndoa ni muhimu na mafunzo hayo yatasaidia kupunguza wimbi la talaka. Alisema Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inasikitishwa na ongezeko la talaka Zanzibar, hali ambayo alidai inasababisha kukosekana kwa nguvu kazi ya taifa kwa kuwa vijana wengi wanajiingiza katika vitendo viovu baada ya kukosa malezi ya wazazi wawili.

Aliiomba Wizara ya Elimu Zanzibar kuingiza mafunzo ya ndoa katika mtaala wa elimu hasa katika somo la dini ili kuwapa uelewa mzuri vijana wanapofikia uamuzi wa kuingia katika ndoa. Pia aliiomba Ofisi ya Mufti Zanzibar kuhimiza na kushajihisha mashekhe wa wilaya kuanzisha madarasa ya mafunzo ya ndoa katika wilaya zote za Unguja na Pemba.

Mwenyekiti wa Baraza la Sanaa Zanzibar, Mariyam Hamdani, alisema mafunzo hayo ya ndoa yamekuja wakati mwafaka na yana mchango mkubwa katika jamii.

Mwalimu Mkuu wa mafunzo hayo, Shekhe Thabit Nouman Jongo, aliwataka wanafunzi kuwa walimu wazuri katika jamii na kuwa mfano bora katika ndoa zao kwa kuyatekeleza kwa vitendo mafunzo waliyoyapata.

Akizungumza kwa niaba ya wanafunzi wenzake waliomaliza mafunzo hayo ya ndoa, Ziada Suleiman Khamis, aliishukuru serikali kwa kuyaendeleza vyema mafunzo hayo. "Tuna imani kuwa tuliopata mafunzo haya, tutakuwa mabalozi wazuri kwa wenzetu katika kuimarisha mapenzi na mahaba katika ndoa ili kupunguza wimbi la talaka zisizo na msingi," alisema.

# Balozi Sokoine aanika mbinu kuhimili mabadiliko tabianchi

**Na Mwandishi Wetu**

MIFUMO ya ikolojia yenye afya ndiyo itakayotupatia huduma za uhakika kama chakula, majisafi na salama, kutuepusha na magonjwa, mafuriko, uharibifu wa ardhi na wakati huo huo kutuwezesha kuhimili athari zitokanazo na mabadiliko ya tabianchi.

Kauli hiyo ilitolewa jana na Naibu Katibu Mkuu Ofisi ya Makamu wa Rais, Balozi Joseph Sokoine, alipofungua warsha ya mafunzo kuhusu kuhimili mabadiliko ya tabianchi kwa kutumia mifumo ya ikolojia iliyofanyika katika ukumbi wa Chuo cha Mipango jijini Dodoma.

Alisema kukosekana kwa huduma hizo kutapelekea kushindwa kufikia malengo ya maendeleo ya milenia, hivyo anaamini mradi huo umekuja wakati mwafaka ambao serikali inaendelea kukuza uchumi katika njia endelevu.

"Kama mnavyofahamu, mabadiliko ya tabianchi yameleta athari mbalimbali kwenye mazingira yetu nchini. Kati ya madhara hayo, ni kuharibika kwa kanda za Ikolojia Kilimo (Agro Ecolojical Zones) ambazo kwa mujibu wa utafiti, kanda hizi ziko saba. Utafiti unaonyesha kwamba, ni rahisi kuhimili kuliko kukabili," alifafanua.

Akimkaribisha mgeni rasmi huyo katika warsha hiyo, Kaimu Mkurugenzi wa Mazingira, Faraja Ngerageza, alisema itawawezesha washiriki kufahamu zaidi kuhusu kuhimili mabadiliko ya tabianchi kwa kutumia mifumo ya ikolojia iliyoko vijijini.

Warsha hiyo ya mafunzo ya siku tatu imeandaliwa na Ofisi ya Makamu wa Rais kupitia mradi wa kuhimili mabadiliko ya tabianchi kwa kutumia mifumo ya ikolojia vijijini (EBARR).

Warsha hiyo imehudhuriwa na washiriki kutoka wizara na taasisi mbalimbali za serikali.




Ofisa Mtendaji Mkuu wa Benki ya Biashara ya Kimataifa (ICB), Villy Vellayappan (kushoto), akizungumza jambo na Naibu Gavana wa Benki Kuu Tanzania (BOT), Dk. Bernard Kibesse (katikati), katika hafla ya kusherehekea miaka 22 ya mafanikio ya benki hiyo hapa nchini, iliyofanyika jijini Dar es Salaam jana. Kulia ni Mwenyekiti wa Bodi ya Benki ya ICB, Josephine Sevaretnam. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Waliokaidi kulima pamba kukamatwa

**Na Tiganya Vincent**

MKUU wa Wilaya ya Uyui, Gift Msuya, amewaagiza watendaji wa vijiji kushirikiana na Mgambo kuwakamata wakulima ambao hawakulima zao la pamba licha ya kuchukua mbegu na dawa za kuua wadudu wakaribifu msimu uliopita.

Aliagiza kuchukua hatua hiyo baada ya wakulima hao kushindwa kulima pamba na wengine kuitorosha na kwenda kuuzia maeneo mengine, jambo ambalo limesababisha kushindwa kulipa deni lao la Sh. milioni 53 wanazodaiwa na kampuni za Kahama Cotton Company Limited na Kahama Oil Mill wiki hii.

Msuya alitoa kauli hiyo juzi wakati wa ziara ya Mkuu wa Mkoa wa Tabora, Aggrey Mwanri, kwenye kampeni yake ya kuhamasisha kilimo ikiwamo cha pamba katika Kijiji cha Migungumalo.

Alisema deni hilo wanalodaiwa wakulima limesababisha kampuni hizo kukataa kulipa deni la ushuru wa Halmashauri ya Wilaya ya Tabora wanaodaiwa Sh. milioni 46 zinazotokana na mauzo ya kilo milioni 1.2 za msimu uliopita.

Msuya alisema uchelewashaji wa fedha hizo kutoka kampuni hizo kwa ajili ya ushuru wa halmashauri umesababisha kukwamisha baadhi ya shughuli za maendeleo ikiwamo za ujenzi wa vyumba vya madarasa.

Kwa upande wake Mwanri alimwagiza ofisa ushirika kuorodhesha wakulima wote wanaodaiwa na kukabidhi majina ya wakulima hao ambao hawataki kulipa ili hatua zichukuliwe dhidi yao.

Alisema haiwezekani mkulima achukue mbegu bila kupanda na kuacha bila kudaiwa, na kuongeza kuwa ni vema ikiwezekana kwa yule mwenye mifugo ataoa ili kulipa deni.

Katika hatua nyingine Mkuu huyo wa Wilaya alisema kwa mujibu wa sheria ndogo ndogo za Halmashauri ya Wilaya ya Tabora, kila kaya ni lazima ilime ekari tatu za mazao ya chakula na ekari tatu za mazao ya chakula.

Alisema asiyetekeleza jambo hilo anavunja sheria, na hatua kali dhidi yake zitachukuliwa.

# Mikakati yaanza Veta wadau hoteli kutoa mafunzo

**Na Mwandishi Wetu**

MAMLAKA ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi (VETA), imekutana na wadau wa sekta ya hoteli (Ukarimu) na utalii wa mikoa ya Lindi na Mtwara kuweka mikakati ya kuanza kutoa mafunzo kwa ushirikiano kupitia programu ya uwanagenzi pacha.

Akifungua warsha hiyo mkoani Mtwara, Mkuu wa Chuo cha Veta Mtwara, Joseph Kibehele, alisema utoaji mafunzo kupitia programu hiyo unategemea sana wenye viwanda, kampuni na hoteli kushiriki kikamilifu.

"Tunawaomba sana mshiriki katika programu hii ili tuweze kuandaa wafanyakazi wenye viwango mnavyovihitaji kwenye hoteli zenu," alisema.

Aliongeza kuwa Veta inatambua umuhimu wa kushirikiana na viwanda katika kutoa mafunzo kwa kuwa ushirikiano huo unawezesha kuandaa nguvu kazi mahiri zaidi inayoendana na mahitaji halisi ya viwanda hasa kwa kuzingatia kuwa sehemu kubwa ya mafunzo hayo yanafanyika sehemu za kazi.

Mratibu wa programu hiyo, Francis Komba, alisema Veta imeamua kutoa mafunzo ya uanagenzi pacha katika sekta hiyo kupitia mfumo huo baada ya utafiti wa soko la ajira kufanyika katika mikoa hiyo na kubaini mahitaji makubwa ya wataalamu wa hoteli na utalii kwa ngazi ya ufundi stadi.

Alisema mafunzo katika programu hiyo kwa mikoa ya Lindi na Mtwara kwenye fani ya ukarimu na utalii yanatarajiwa kuanza kutolewa mwezi Januari, 2020 kupitia Chuo cha Veta Mtwara.

Kwa mujibu wa Komba, mafunzo kupitia programu hiyo yanamwezesha kijana kupata ujuzi wa fani husika akiwa chuoni na sehemu ya kazi, hivyo kumwezesha kwa kiasi kikubwa kujifunza kwa vitendo na kuendana na mahitaji ya soko la ajira pamoja na kupata uzoefu na uelewa wa mazingira halisi ya kufanyia kazi.

Meneja wa Shangani Apartments, Athumani Akida, alisema kuwa mfumo huo wa mafunzo utasaidia wenye hoteli kupata wafanyakazi bora zaidi kwa kuwa wenye hoteli wanapata fursa ya kushiriki kuwaandaa wakati wa mafunzo.

Alisema: "Naamini kabisa programu hii itaondoa lile pengo linalojitokeza kati ya sisi waajiri na wanafunzi wanaozalishwa vyuoni."

Naye Ofisa Mwandamizi wa hoteli ya BNN Royal Palm, Grace Paul, alisema kuwa hoteli yake iko tayari kushiriki kikamilifu katika kutoa mafunzo hayo na kushauri wadau wengine kujitokeza kushiriki kutoa mafunzo kupitia programu hiyo yenye faida kwao.

HABARI KIMATAIFA

# Trump atuma barua kali kwa Spika

**WASHINGTON,** Marekani

RAIS Donald Trump, ameukosoa uchunguzi unaokaribia kufanyika kwa kuandika barua ya hasira kwa Spika wa Bunge, Nancy Pelosi, akimtuhumu kwa kutangaza vita vya wazi dhidi ya demokrasia ya Marekani.

Trump alipigiwa kura ya uchunguzi jana kuhusu madai kwamba aliishinikiza Ukraine kwa ajili ya maslahi binafsi ya kisiasa.

"Umeshushia hadhi umuhimu wa neno uchunguzi!" Aliandika katika barua iliyotumwa Jumanne.

**Haki ya mchakato ilitolewa zaidi kwa wale walioshtaki katika kesi ya Salem Witch Trials.**

Uchunguzi huo utapalilia njia ya kuandaa kesi katika bunge la Senati.

Huku kukiwa na matumaini kidogo ya kubadili matokeo ya kura ya uchunguzi huo, Trump, alitumia barua yake ya kurasa sita kuonyesha hasira yake dhidi ya mchakato huo na kumpinga Pelosi, ambaye ni Spika wa Bunge anayetoka katika Chama cha Democrat.

Ilikuwa ni hatua isiyo ya kawaida iliyochukuliwa na Rais, ambaye alipigana kuzuia mchakato wa kumchunguza kwa kuwazuia washirika muhimu kutoa ushahidi katika Bunge la Wawakilishi.

Rais huyo anadai katika barua yake kwamba alinyimwa haki ya kimsingi ya kikatiba kuanzia mwanzoni mwa mchakato wa uchunguzi.

"Haki ya mchakato ilitolewa zaidi kwa wale walioshtaki katika kesi ya Salem Witch Trials," aliandika.

Hata hivyo Rais Trump alialikwa na Mwenyekiti wa Kamati ya Sheria ya Bunge kutoka Chama cha Democrat kutoa ushahidi katika mchakato wa uchunguzi huo, jambo ambalo lingeruhusu timu yake ya kisheria kuwahoji mashahidi, lakini alikataa.

Meya wa Salem, Kim Driscoll, alituma ujumbe wa Twitter kwamba Rais anapaswa "kujifunza historia," akisema kuwa kesi za kichawi zilizowapata na hatia wahusika zilifanyika wakati hakuna ushahidi, huku kesi dhidi ya Rais ikiwa na shahidi wa kutosha.

Pelosi akizungumza na waandishi wa Bunge kwamba alikuwa bado hajaisoma barua ya Rais kama ipo kamili, lakini ameona dhanayake na anafikiri ana matatizo. **BBC**

## Mume amcharanga mkewe mapanga, kisa kuchinja jogoo

**KAMPALA,** UGANDA

MWANAUME mmoja mwenye umri wa miaka 50 kutoka Wilaya ya Budaka Mashariki mwa Uganda, amemjeruhi mke wake vibaya baada ya kumchinja kuku aliyetakiwa kufanywa kitoweo kwenye siku kuu ya Krismasi.

Kwa mujibu wa gazeti la Daily Monitor, bwana huyo alimnunua kuku kwa Sh. 15,000 za Uganda akipanga kumchinja siku ya Krismasi, lakini kwa bahati mbaya mke wake aliamua kumchinja na kumuandaa siku ya Jumapili ya Desemba 15, mwaka huu.

Kwa mujibu wa katibu wa habari wa eneo hilo, Bw Joseph Gadimba, amesema baada ya mume kugundua kuwa kuku huyo hayupo, alimpiga mke wake na kumlaumu kwanini amemchinja bila ruhusa yake.

''Alimpiga na kumchapa mke wake mara nyingi, huku akimuacha akipigania uhai wake," alisema Gadimba.

Kwa sasa mwanamke huyo anatibiwa katika kituo cha afya cha Budaka, Mashariki mwa Uganda.



Jogoo mfano kama huyu ndiye aliyeleta majanga huko Budaka, Uganda. **PICHA: MTANDAO**



Moja ya picha bora ya 2019 ikimwonyesha mwanamke akiwa na zana yake ya jadi wakati wa maandamano ya kumpinga Rais wa Ecuador, Lenin Moreno, katika mji wa Quito hivi karibuni. **PICHA: REUTERS**

## Mahakama India yaahirisha kesi ya sheria yenye utata

**MOMBAI,** India

MAHAKAMA ya juu ya India imeahirisha kikao cha kusikilizwa hoja za kupinga sheria mpya ya uraia ambayo imezusha upinzani na maandamano makubwa kote nchini humo.

Katika maelezo yake mahakama imesema itazisikiliza hoja hizo Januari 22. Sheria hiyo inahusu kuharakisha maombi ya uraia kwa wahamiaji wa Kihindu, Kikristo na makundi mengine ya kidini ya walio wachache ambao wako nchini India kinyume na sheria.



Hata hivyo, ndani ya sheria hiyo inawatenga wahamiaji wa Kiislamu kutoka nchini Bangladesh, Pakistan na Afghanistan.

Wakosoaji wanasema kwamba sheria hiyo mpya ni ajenda ya serikali ya Waziri Mkuu Narendra Modi (pichani) inayoongozwa na chama cha siasa kali za Kihindu, BJP, kuwatenga Waislamu.

Waislamu nchini humo wanafikia milioni 200 na kwamba inakwenda kinyume na mtazamo wa nchi hiyo wa katiba isiyoelemea katika dini. **DW**

## Misaada kuingia Syria kupitia nchi nne

**DAMASCUS,** Syria

HATIMAYE katika muda wa miaka sita Umoja wa Mataifa na makundi mengine ya misaada ya kiutu, umefanikiwa kuvuka mpaka kuingia nchini Syria.



Msafara wa magari yaliyobeba shehena ya msaada unatokea katika nchi za Uturuki, Iraq na Jordan, ambako ni maeneo manne ambayo yameidhinishwa na chombo hicho kupeleka misaada ya kiutu kwa mamilioni ya watu nchini humo.

Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa, Antonio Guterres, alisema mataifa 15 wanachama yanalengo la kuongeza muda wa operesheni hiyo wiki hii.

Hata hivyo Urusi imetaka kupunguzwa kwa idadi ya maeneo hayo ya vivuko, lakini Ubelgiji, Kuwait na Ujerumani waliliridhia azimio la kuongeza maeneo ya vivuko vya mipakani kuingia Syria.

# Lissu aiomba Chadema imsaidie kurejea nchini

INATOKA UK. 3

mfupi baada ya kumalizika kwa kikao cha mchana cha Bunge alichochangia hoja.

**'UCHAGUZI MITAA URUDIWE'**

Akizungumza katika mkutano huo jana, Mwenyekiti wa Chadema, Freeman Mbowe, aliitaka serikali kuitisha upya uchaguzi wa serikali mitaa ili kuimarisha ushirikiano mwema baina ya wananchi na viongozi wao, akionya uwezekano wa kutokea machafuko siku zijazo iwapo hilo halitafanyika.

"Mnaweza mkaona hili ni jambo dogo, lakini mpaka sasa nchi imemwagiwa mafuta na mimi naogopa kutia kibiriti," Mbowe alidai.

Kiongozi huyo wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni pia alionya Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa nchini, akidai inatumika vibaya kudumaza upinzani badala ya kuimarisha na kulea vyama hivyo kwa mujibu wa sheria na inafanya kazi kwa upendeleo.

Kuhusu kutakiwa kuondoa bendera za chama hicho zilizowekwa katika barabara ya kuelekea Mlimani City, Mbowe alidai kushangazwa na amri hiyo ya manispaa kwa kile alichodai ni kinyume cha sheria.




Wakala wa kampuni ya simu za mkononi wa Airtel Tanzania mkoani Arusha, Joseph Mlaki, akimsajili mteja wa kampuni hiyo laini ya simu kwa alama ya vidole wakati wa uzinduzi wa kampeni ya 'Haachwi Mtu Nyuma, Kamilisha Usajili Wako' jana. **NA MPIGAPICHA WETU**

# Mradi wa kituo cha biashara Kurasini kuuza mnada mazao

**Na Mwandishi Wetu**

SERIKALI imeanza utekelezaji wa mradi mkubwa wa kituo cha biashara katika eneo la Kurasini (Kurasini Trade and Logistic Centre) kwa ajili ya kuuza kwa mnada mazao ya biashara kwa ajili ya kuchangia uchumi wa nchi.

Gharama halisi za mradi huo zitafahamika baada ya kufanyika upembuzi yakinifu na timu maalum iliyoundwa na bodi ya wakurugenzi ya Mamlaka ya Maeneo Maalum ya uwekezaji (EPZA) iliyokutana jana, jijini Dar es Salaam.

Inakadiriwa kuwa kituo hicho ambacho kitajengwa na EPZA kuwa na thamani ya Dola za Kimarekani milioni 30 (zaidi ya Sh. bilioni 60) hadi utakapokamilika.

Waziri wa Viwanda na Biashara, Innocent Bashungwa, alisema mradi huo utafungua fursa kubwa ya soko kwa ajili ya bidhaa za kilimo ambazo zitauzwa kwa wafanyabiashara nje ya nchi kupitia soko la bidhaa la Tanzania Mercantile Exchange (TMX) na kuongeza pato la wakulima.

"Utekelezaji wa mradi huu utabadilisha kwa kiasi kikubwa sekta ya kilimo na kuchangia kwa kiasi kikubwa pato la mkulima na la taifa kwa kuuza bidhaa za kilimo katika soko la Afrika Mashariki na Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika," alisema.

Katika utekelezaji wa mradi huo, mnada mkubwa wa mauzo ya chai (Tea Trade Logistic Centre) utajengwa ambao utajumuisha eneo la kukusanya chai, maghala ya uhifadhi na viwanda kwa ajili ya kuchakata chai.

Ujenzi wa mnada huo utafanya chai ya Tanzania iweze kuuzwa hapa hapa nchini badala ya kupelekwa kwenye mnada wa Mombasa ambao una gharama kubwa za usafirishaji na uhifadhi wa chai.

Waziri Bashungwa alisema, kamati maalum iliyoundwa itatakiwa kuwasilisha ripoti yake kwenye mkutano mwingine wa bodi ya EPZA mwezi Februari, mwakani. Ripoti hiyo itaonyesha mwelekeo wa utekelezaji wa mradi huo.

Mamlaka ya EPZA imeelekezwa kuanza mara moja utekelezaji wa mradi huo ambao unatarajiwa kufungamanisha sekta za kilimo na viwanda.

Mkurugenzi Mkuu wa EPZA, Joseph Simbakalia, alisema utekelezaji wa mradi huo, utaanza mara moja na tayari wamepanga kukutana na wadau wote wa mazao ya kilimo ili kujua mahitaji yao katika utekelezaji wa mradi huo.

"Tunaaza kukutana na leo kupata maoni yao na mahitaji ili kuanza mara moja ujenzi wa miundombinu katika kituo kikubwa cha kibiashara," alisema.

Hadi sasa serikali imeshalipa fidia ya thamani ya Sh. bilioni 101 kwa wakazi wa Kurasini ili kutekeleza mradi katika eneo la ukubwa wa ekari 61.87 la ardhi.

# UVCCM yaanzia Iringa kufufua vyuo vyake

INATOKA UK. 3

Alisema kituo hicho kitawaandaa vijana, makada na viongozi kuongoza mapambano ya kuandaa vijana na ujenzi wa uchumi imara.

Akizindua chuo cha mafunzo Ihemi Makamu Mwenyekiti wa CCM Taifa, Philip Mangula, aliwataka vijana kufuta fikra za kuajiriwa badala yake iwe kujiajiri.

"Mnapokuja chuoni futeni mawazo ya kujifunza kuajiriwa, hapa sehemu ya mafunzo ni kubadilisha fikra na mitizamo ya kwamba kusoma ni kuajiriwa,"alisema Mangula.

Aliwataka vijana kubadili mitizamo wakijua watajitegemea na chuoni hapo watafundishwa namna ya kujiajiri na ajira kubwa ni kilimo.

Mlezi wa CCM Iringa, Waziri Mkuu mstaafu, Mizengo Pinda alisema moja ya malengo ya chuo hicho ni kujenga hisia ndani ya vijana kuhusu siasa za nchi kwa maslahi ya Watanzania.

Alisema ni muhimu vijana kutambua thamani ya uzalendo ni muhimu kujikita katika siasa na itikadi ili waweze kujua taifa linataka nini kwa upande wa chama.

"Nimefurahi kuona chuo cha Ihemi kimekuwa ni kituo cha kuamsha hali na fikra mpya kwa vijana kisiasa na kimaendeleo. Mna hekari 1963 zitatumika katika majengo lakini vilevile kutoa mafunzo ya uzalishaji, kuna vitalu, nyumba ufugaji wa nyuki na kilimo kwa ujumla,"alisema Pinda.

Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu kazi, Ajira na Vijana, Antony Mavunde, alisema vijana zaidi ya 200 katika chuo hicho walifundishwa kilimo kupitia kitalu nyumba na 60 walifundishwa kupinda vyuma.

"Lengo lilikuwa ni baada ya muda mfupi tuwe na uwezo wa kuwatoa vijana wengi zaidi kutengeneza kitalu nyumba (green house) badala ya kuagiza nje kama ilivyo sasa,"alisema Mavunde.

Mkuu wa Mkoa wa Iringa, Ally Hapi, alisema wakati wa ukombozi kazi kubwa ya chama ni hamasa, lakini baada ya uhuru siasa imebadilika imekuwa sayansi ni wakati sasa vijana wapate kufundishwa namna ya kujenga hoja na kukipigania chama na kukilinda.

Christpher ole Sendeka, Mkuu wa Mkoa wa Njombe alisema anaipongeza CCM kwa kuyafufua mawazo ya muasisi wa taifa Julius Nyerere, kwa vitendo kwa kukifufua chuo hicho cha CCM.

"Huwezi kuwa na chama madhubuti, makini bila kuwa na mahali pa kuwapika viongozi wake, chuo cha Ihemi kitaipa CCM nguvu mpya itakayoendana na kasi ya Rais John Magufuli," alisema.

## TANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

### KAZI /AJIRA

**Nafasi za kazi** ualimu masomo ya sst/diploma 0656490706/0784142792

### VIWANJA/MASHAMBA

**SHAMBA LINAUZWA,** SHAMBA EKA 40 MOROGORO. Linafaa kufuga na kilimo, limeshavunwa misimu 3, lina nyumba vyumba 2 na Gari inafika. Bei ml.25 zenye mjadala. Wasiliana 0718965491 / 0784653304 / 0629478005.


**NIPASHE NI JIBU LAKO**

NJOO UTANGAZE NASI BIDHAA YAKO

KWA BEI NAFUU SANA

Tutumie E-mail: advertise@guardian.co.tz,

au piga simu: 0782253676


**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**KUITWA SHAURINI MDAIWA**
**Mahakama ya wilaya ya Dodoma Mjini**

Madai na. 68/2019
Mdai: Anna Kimwala
MDAIWA: Costantine Mayala

Kwa Costantine Mayala Mwanza
Kwa kuwa mdai ameleta madai yake kwamba

MADAI YA TALAKA
Hivyo unahitajiwa /mnahitajiwa kuhudhuria binafsi katika mahakama hii siku ya Tarehe 23/12/2019 saa 2.30 asubuhi kwa kujibu madai na kwa kuwa siku hiyo ya kuitwa shauri hilo ni lazima kuleta mashidi wako/wenu na hati zote zinazohusu shauri hilo kwa ajili ya kujitetea shauri hilo.

Na kama hukuhudhuria siku iliyotajwa hapo juu mahakama itadhibitisha kama umepokea /mmepokea kuitwa shaurini hii itaweza kutoa hukumu kuwa umeshundwa /mmeshindwa.

Hati hii yatolewa kwa amri yangu na chapa ya mahakamahii leo tarehe 10/12/2019

115560102

**KUPOTEA KWA KADI YA GARI**

Godfrey Seme Masanja mkazi wa Wilaya ya Meatu Mkoani Simiyu anatangaza kupoteza kadi yake ya gari aina na Mitsubish Fuso yenye namba T449 DLN. Kadi hiyo ilipotea Juni 2019. Anaomba yoyote atakayekuwa ameiokota aiwasilishe katika kituo cha polisi Wilayani Meatu.

Taarifa ya polisi:
SIM/MEA/RB/544567/2019.

115560602

**SHERIA YA UMILIKI WA ARDHI YA MWAKA 1999**

**(SURA YA 113)**
**KUHAMISHA KWA BARUA YA TOLEO YA KUMILIKI ARDHI**
**MMILIKI ALIYEANDIKISHWA: TALIAN NGAWA MARIKI**

KWENDA KWA: JEFTA SHIKEE ULOMI
ARDHI: KIWANJA NA. 856 KITALU 'M'
ENEO LA MBAGALA

MANISPAA YA TEMEKE JIJINI DAR ES SALAAM.
Taarifa inatolewa kwamba AFISA ARDHI MTEULE anakusudia kuhamisha BARUA YA TOLEO TAJWA YA KUMILIKI ARDHI kwenda kwa JEFTA SHIKEE ULOMI kutoka kwa TALIAN NGAWA MARIKI aliyewasilisha nyaraka zake za makubaliano ya kuuziana kiwanja tajwa hapo juu. Ninakusudia kutoa HATI MILIKI iwapo hakuna pingamizi litakalotolewa kwa muda siku 30 tangu tarehe ya taarifa hii ilipotangazwa katika gazeti.

P.A. Masoy
AFISA ARDHI MTEULE
MANISPAA YA TEMEKE

115560002


**Uza, Chenye Thamani**

**Kubwa Kwa**

**Kutangaza Nasi**

**Kwa Bei Poa**

**Tupigie 0782253676**

**Kwa Habari Motomoto**

usikose Gazeti lako
la Nipashe kila siku

Tupigie 0782253676

Nipashe
www.ippmedia.com
MWANGA WA JAMII

**OFISI ZA MATANGAZO**
**MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,**
**PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 745 700 710.**
**E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com**

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.



# GUARDIOLA: ARSENAL AMUENI KWA ARTETA

**MANCHESTER,** England

KOCHA wa Manchester City, Pep Guardiola anatarajia majaliwa yajao ya Mikel Arteta yataamuliwa haraka baada ya kufanya mazungumzo na Arsenal.

Arteta, kwa sasa ni kocha msaidizi wa Guardiola, na ndiye anayeongoza katika orodha ya wanaotakiwa kurithi mikoba ya Unai Emery kama kocha mkuu wa 'Wawashika Bunduki' hao.

Na sasa kocha huyo wa City anataka jambo hilo lifanyike mapema ili Arteta aweze kujua hatima yake.

Alipoulizwa kama anataka maamuzi hayo yafanyike haraka, Guardiola alisema Jumanne: "Ndio nafikiri hivyo. Itatokea haraka. Sidhani kama itatokea kabla ya mwishoni mwa wiki."

Kocha huyo wa zamani wa Barcelona anataka Arteta kubakia na mabingwa hao wa Ligi Kuu ya England, lakini amepanga kutafuta mwingine kama Mhispania mwenzake huyo ataondoka.

Guardiola alisema: "Tutasonga mbele. Tunakwenda kujiandaa kwa ajili ya mchezo ujao. Tunakwenda kuangalia nini cha kufanya kwa wakati uliopo na kipi kinatakiwa kifanyike haraka zaidi."

"(Arteta) anajua nini anachokitaka na sisi tupo tayari kuendelea baada ya yeye kuondoka, kama ataamua kuondoka klabuni na sisi tutafanya haraka maamuzi mengine yanayofaa."

# Koke aipa pigo Atletico Madrid

**MADRID,** Hispania


NAHODHA wa Atletico Madrid, Koke anaweza kuukosa mchezo wa Ligi Kuu ya Hispania, LaLiga, dhidi ya Real Betis Jumapili baada ya kuumia misuli.

Kiungo huyo mwenye umri wa miaka 27, aliumia wakati Atletico ikishinda 2-0 dhidi ya Osasuna wikendi iliyopita.

Koke alifanyiwa uchunguzi na madaktari wa timu na kugundulika kwamba ameumia misuli ya nyama za paja na Atleti imethibitisha katika taarifa yake Jumanne.

Hata hivyo, klabu hiyo haikutoa muda ambao Koke atakaa nje, huku Atleti wakikabiliwa na mchezo unaofuata dhidi ya Betis Jumapili, ukiwa ni mchezo wa mwisho kabla ya mapumziko ya mwishoni mwa mwaka kwa nchini Hispania.

Kikosi hicho cha kocha, Diego Simeone kipo nafasi ya tano kwenye msimamo wa LaLiga, huku pia wamepangwa kucheza na Liverpool kwenye hatua ya mtoano wa timu 16-bora katika michuano ya Ligi ya Mabingwa Ulaya.





# *Van Dijk mchezaji bora wa mwaka wa mashabiki EPL*

**LONDON,** England

VIRGIL van Dijk amempiku Raheem Sterling wa Manchester City kwa kutwaa tuzo ya mchezaji bora wa mashabiki.

Nahodha huyo wa Uholanzi alipata kura 340,000 alizopigiwa na Chama cha Mashabiki zilizomchagua kuwa mchezaji bora wa mwaka.

Nafasi ya tatu ilishikwa na Sadio Mane (Liverpool), Son Heung-min (Tottenham Hotspurs), Jamie Vardy (Leicester City) na Pierre-Emerick Aubameyang wa Arsenal.

Van Dijk anakuwa mchezaji wa nne Liverpool kutwaa tuzo hiyo ndani ya miaka saba, akitanguliwa na Mo Salah, Philippe Coutinho na Luis Suarez.

Mapema mwezi huu, beki huyo mwenye miaka 28 alishika nafasi ya pili katika mbio za kuwania tuzo ya mchezaji bora wa dunia nyuma ya Lionel Messi wa Barcelona.

Tangu Van Dikj aliponunuliwa kwa bei mbaya na kocha Jurgen Klopp akitokea Southampton mwaka jana amefunga mabao saba katika mechi 69 alizocheza.

# HABARI MICHEZO

## Icardi hatajiunga Juventus- Nara

**PARIS,** Ufaransa

MAURO Icardi hatajiunga na Juventus mwakani, wakala wake ambaye ni mke wake, Wanda Nara amesema.

Icardi mwenye umri wa miaka 26, anafurahia maisha yake ya uchezaji soka pale kwenye klabu ya Paris Saint-Germain, ambako anacheza kwa mkopo kutoka Inter Milan, na amefunga mabao 13 katika mechi 16 kwenye mashindano yote.

Lakini huku kukiwa na mazungumzo kwamba anaweza kujiunga na Juve hapo baadaye, Nara amekanusha madai hayo ya Icardi kuweza kurudi kwenye Serie A mwakani.

"Hapana, hapana. Kwa sasa Mauro yupo Paris, yeye anafurahia maisha pale na anafurahi kufunga mabao," alisema Nara akiiambia Rete 4.

"Kitu pekee ambacho nakipenda mimi ni furaha yake na ana furahia kucheza pale PSG."

Icardi aling'ara pale Inter kwa misimu sita, ambako ana mkataba hadi Juni 2022.

Nara alituma salamu kwa miamba hao wa Serie A, akisema aliamua kujiunga PSG na si kuwasaliti Inter.

"Nina kumbukumbu nzuri za pale San Siro na Interisti. Na kama mara zote ambavyo nimekuwa nasema, Inter Milan wanajua kwamba mara zote moyo wake ulikuwa pale," alisema.

"Na chaguo hili la kwenda Paris lilifanywa kwa ajili ya kutowasaliti Nerazzurri.

"Tuliamua kuachana kwa amani bila kusalitiana, Mauro alikwenda kwenye klabu ambayo hata Inter wenyewe wasingejiona kama wamesalitiwa."






## ALONSO AJITOA NAFASI YA UKOCHA BAYERN

**MADRID,** Hispania

XABI Alonso amejiondoa mwenyewe kwenye nafasi ya kuwa kocha ajaye wa Bayern Munich kwa sababu hana uzoefu wa kutosha.

Kiungo huyo wa zamani wa Hispania, ambaye alimalizia kipindi chake cha uchezaji pale Bayern akicheza kati ya mwaka 2014 na 2017, kwa sasa ni kocha wa Real Sociedad B.

Licha ya kuwa na mahusiano ya karibuni na mabingwa hao wa Bundesliga, Bayern, Alonso anaamini ni mapema mno kwake kuingia kwenye mbio za kuwania uongozi wa klabu hiyo.

Alipoulizwa kuhusu nafasi ya kazi pale Bayern, aliliambia gazeti la Marca: "Nipo sehemu ambayo natakiwa kuwa kwa sasa ambako nataka kuendelea kuwa hapa San Sebastian na Real Sociedad.

"Ndio mwanzo wangu wa ukocha kwa sasa na sina malengo zaidi ya hapa kwa sasa. "Natumaini naweza kuwa kocha bora hapa Real Sociedad, kuimarisha uzoefu wangu kila mwaka.

"Chochote kitakachonisimamisha kitatokea. Klabu zinatakiwa kuwasajili makocha bora duniani na mimi ndio kwanza naanza."

Hansi Flick kwa sasa ndiye kocha wa muda pale Bayern baada ya kutimuliwa kwa Niko Kovac Novemba mwaka huu kutokana na timu kuwa na matokeo mabaya uwanjani.

Alonso mwenye umri wa miaka 38, alishinda taji la Ligi Kuu ya Hispania, LaLiga, na Ligi ya Mabingwa Ulaya wakati wa misimu yake mitano aliyokaa pale Real Madrid.

## Jesus: Hata Liver itachezea

**DOHA,** Qatar

KOCHA wa Flamengo, Jorge Jesus amedai kikosi chake hakimhofii yeyote ikiwamo Liverpool, baada ya kufuzu kucheza fainali ya Klabu Bingwa Dunia.

Klabu hiyo ya nchini Brazil ilitoka nyuma na kuifunga klabu kutoka Saudi Arabia, Al Hilal 3-1 kwenye nusu fainali iliyopigwa Uwanja wa Kimataifa wa Khalifa hapa Doha.

Al Hilal ilianza kwa kuongoza bao likifungwa na Salem Al Dawsari kabla ya Giorgian de Arrascaeta kuwasawazishia mabingwa hao wa Copa Libertadores, baada tu ya kuanza kwa kipindi cha pili.

Bruno Henrique aliongeza la pili kwa Flamengo kabla ya Ali Hadi Albulayhi kujifunga mwenyewe.

"Kwa kutinga kwetu fainali hatumhofii yeyote," alisema Jesus baada ya mchezo huo akiwaambia waandishi wa habari.

"Wakati tulipowasili hapa tulifikiri tunaweza kuwa mabingwa; sasa tupo kwenye fainali. Sisi ni timu ambayo kamwe haishindwi ikifika fainali.

"Niliwaambia vijana baada ya kipindi cha kwanza, kwamba tutafunga. Nilijua wanaweza kukwama kipindi cha pili na sisi tulikuwa tayari.

"Tulikuwa na matatizo katika kipindi cha kwanza, halafu tukatulia na tukajipanga kufanya vizuri."

Mabingwa wa Ligi ya Mabingwa Ulaya, Liverpool jana Jumatano walikuwa wanacheza na klabu kutoka nchini Mexico, Monterrey kwenye nusu fainali na mshindi atakutana na Flamengo katika fainali itakayopigwa Jumamosi.



# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# RONALDO KUSTAAFIA JUVENTUS - MENDES

**Ni mwenye furaha hapo Juve, anafanya kazi na kocha mkubwa...**

**TURIN,** Italia

WAKALA wa Cristiano Ronaldo, Jorge Mendes, amesema mshambuliaji huyo raia wa Ureno anaweza kutundikia daluga lake akiwa katika Klabu ya Juventus.

**Ronaldo, 34, alijiunga na Juventus mwaka jana na kutwaa ubingwa wa Serie A pamoja na tuzo ya mwanasoka bora wa mwaka katika msimu wake wa kwanza.**

Na licha ya Ronaldo kutibuana na kocha mpya Maurizio Sarri baada ya kufanyiwa mabadiliko ['sab'] mapema dhidi ya AC Milan Novemba mwaka huu, Mendes amesema mteja wake huyo ni mwenye furaha na anaweza kustaafia katika klabu hiyo.

"Ni mwenye furaha hapo Juventus, anafanya kazi na kocha mkubwa."

Wakati Ronaldo ameendelea kutwaa tuzo Serie A, mwaka huu ameikosa Balon d'Or aliyoitwaa mara tano na kuzidiwa mara moja na mpinzani wake Lionel Messi ambaye alitwaa kwa mara ya sita.

Kwa mara ya mwisho aliitwaa tuzo hiyo mwaka 2017, lakini Mendes anadhani Ronaldo hakuwa na bahati ya kutazamwa na haraka akamsifu mshambuliaji huyo kama bora duniani na mwenye athari kwa klabu na nchi yake.

"Alistahili kushinda angalau mara moja kwa zaidi ya miaka miwili iliyopita," alisema Mendes. "Kama angekuwa bado anaichezea Real Madrid, angeweza kushinda Ballon d'Or.

"Anaweza kushinda mwaka ujao. Ninaweza kusema kile ninachofikiri tu, na kwangu mimi ni dhuluma. Cristiano bado anafikiri tu kuhusu kufanya kazi na kushinda mwaka ujao.

"Wakati alipotua Real Madrid, alihitimisha utawala wa Barcelona. Hakuna wakumlinganisha, Cristiano ni bora."

Ronaldo ambaye ameshafunga mabao 39 katika mechi 62 tangu alipotua Juve, ikiwa ni pamoja na mabao 11 katika michezo 19 msimu huu, ana mkataba na klabu hiyo hadi mwaka 2022.

## ZISIKUPITE

### POGBA KUZUIWA JANUARI

MANCHESTER United haitamruhusu kiungo Mfaransa Paul Pogba, 26, kuondoka klabuni hapo Januari mwakani. ***(Mail)***

### BARCELONA YAMKANA KANTE

BARCELONA haina lengo la kumsajili kiungo wa Chelsea na Ufaransa, N'Golo Kante, 28. ***(Mundo Deportivo - in Spanish)***

### RB LEIPZIG KWA HAALAND

KLABU ya RB Leipzig nayo imeonyesha nia ya kumsajili mshambuliaji wa Red Bull Salzburg na Norway, Erling Braut Haaland, 19. ***(Kicker, via Mail)***

### KUMBAKISHA FERGUSON

CARLO Ancelotti ataendelea kumbakisha kocha wa muda wa Everton, Duncan Ferguson, katika benchi lake la ufundi kama atateuliwa kuwa kocha mkuu wa 'Toffees' hao. ***(Telegraph)***

### YAJIAMINISHA KWA HAALAND

MANCHESTER United inajiamini itafanikiwa kumsajili mshambuliaji wa Red Bull Salzburg na Norway, Erling Braut Haaland kwa dili la pauni milioni 76 katika dirisha la usajili la Januari - kama itakubali kumrejesha kwa mkopo katika klabu yake hiyo ya nchini Austria hadi mwishoni mwa msimu. ***(Sun)***

### KUZITOSA CHELSEA, LIVER

WINGA wa Bayer Leverkusen, Mjerumani Kai Havertz, 20, anayewindwa na Chelsea, Liverpool na Man United - anataka kubaki na klabu hiyo ya Bundesliga. ***(Sky Sports)***

### IBRAHIMOVIC AISUBIRIA MILAN

MSHAMBULIAJI wa zamani wa Sweden, Zlatan Ibrahimovic, 38, anaitaka AC Milan kumlipa mara mbili ofa yao ya pauni milioni 1.7 waliyompa ya zaidi ya miezi 18 ili kumsajili. Straika huyo wa zamani wa Manchester United amekuwa akihusishwa na Everton na kwa sasa ni mchezaji huru. ***(Sun)***

### KUSAIDIWA NA MWANAWE

MTOTO wa Carlo Ancelotti, Davide, alikuwa ndiye msaidizi wake katika klabu ya Napoli na Mtaliano huyo atamteua tena mwanawe huyo mwenye umri wa miaka 30 katika benchi lake la ufundi hapo Everton. ***(Mirror)***

### CHELSEA NA ABRAHAM, JAMES

CHELSEA inataka kukubaliana mkataba mpya na wachezaji wao makinda wawili wa Kiingereza - mshambuliaji Tammy Abraham, 22, na beki Reece James, 20, lakini wamekuwa wakijisuasua. ***(Telegraph)***

### SPURS KUAMUA KWA GIOVANI

REAL Betis inaitarajia Tottenham Hotspur kutekeleza kipengele cha kumnunua jumla Giovani lo Celso ambaye anaichezea kwa mkopo. Kiungo huyo raia wa Argentina mwenye umri wa miaka 23, alijiunga na Spurs akitokea klabu hiyo ya Hispania Agosti mwaka huu. ***(Estadio Deportivo - in Spanish)***

### BENDA AZIVUTIA VILLA, LIVER

LIVERPOOL na Aston Villa zimekuwa zikimfuatilia kipa wa Swindon Town, Mjerumani Steven Benda, 21.***(Football League World)***

## HABARI MICHEZO

## Benki ya DCB yaziasa familia kushiriki mazoezi ya viungo

**Na Mwandishi Wetu**

BENKI ya Biashara ya DCB imezihamasisha familia kujenga tabia ya kushikiri mazoezi ya viungo ili kuweza kuwa na taifa lenye watu wenye afya bora jambo ambalo ni muhimu katika shughuli za uzalishaji mali za kila siku.

Akizungumza na washiriki wa mbio zilizopewa jina la Familia Marathon katika viwanja vya Chumvi, Bahari Beach, nje kidogo ya Jiji la Dar es Salaam hivi karibuni, Mkuu wa Mawasiliano na Masoko wa DCB, Rahma Ngassa alisema ni muhimu kufanya mazoezi ili kuupa mwili afya na nguvu na kuzalisha mali.

"Ni ukweli usiopingika kuwa magonjwa mengi yasiyo ya kuambukiza huchangiwa kwa kiasi kikubwa na aina ya maisha tunayoishi na uzito mkubwa, mazoezi ya mwili yanasaidia sana kupambana na hali hizo," alisema.

Rahma aliongeza kuwa, ili tuweze kuendelea na pia kutimiza azma ya serikali yetu ya kuwa na uchumi wa kati unaotegemea viwanda, tunahitaji sana kuwa na rasilimali watu wenye nguvu na afya bora ya kuweza kuzalisha mali kwa wingi.

Mkuu huyo wa mawasiliano alisema ndiyo maana DCB ilipopata maombi ya kudhamini Familia Marathon walipokea maombi hayo kwa mikono miwili hasa kutokana na umuhimu wa mazoezi kwa afya za wateja wao na Watanzania kwa ujumla.

"Wateja wetu wakiwa na afya bora wataongeza kasi ya uzalishaji mali hivyo hata nasi benki tutanufaika kutokana na kuwa na wateja wetu wafanyakazi, wakulima na wafanyabiashara kwani biashara zao zikikua na benki inakua.

"Endapo tukiwa na Watanzania wenye afya bora, tutapunguza mzigo wa gharama za matibabu kutoka ngazi ya familia hadi serikalini, natoa wito kwa Watanzania kujitokeza kwa wingi na kuwa na utamaduni wa kushiriki mazoezi ya mwili ili kujenga afya bora ya miili yao," aliongeza.

Aidha, alisema DCB imeendelea kutoa fursa na bidhaa mbalimbali kwa wateja zinazolenga kutoa suluhisho la mahitaji ya kifedha kwa wateja wao. "Bidhaa hizi zinawalenga wateja wetu wote wakubwa kwa wadogo, wafanyabiashara wakubwa na wadogo, wakulima pamoja na wateja wa kati na makundi mengine," alisema.

# DK. SHEIN ATEMBEZA BAHASHA Z'BAR HEROES

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

RAIS wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Ali Mohamed Shein, ametoa pongezi kwa wachezaji wa timu ya Taifa ya Zanzibar (Zanzibar Heroes) sambamba na viongozi wao kwa kuweza kuwawakilisha kwa nidhamu katika mashindano ya Chalenji 2019 na kutoa upinzani mkubwa kwa timu zote waliocheza nazo.

**Dk. Shein aliyasema hayo Ikulu mjini Zanzibar juzi katika hafla ya chakula cha mchana alichowaandalia wachezaji wa Zanzibar Heroes ambao wameshiriki mashindano ya Chalenji nchini Uganda huku akiwatembezea bahasha za kaki zilizotuna (fedha taslim ambazo hakutaja ni kiasi gani).**


Akisoma hotuba kwa niaba ya Rais, Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Issa Ussi Haji Gavu, alisema kipindi hiki bahati haikuwa upande wa Zanzibar Heroes kama ilivyokuwa mwaka jana, lakini timu hiyo imeendelea kuwa tishio katika mashindano hayo.

Aidha, Rais Shein alieleza kuwa Zanzibar Heroes imeonyesha upinzani na ufundi wa hali ya juu lakini kwenye mpira wataalamu wanasema kwamba kosa moja dogo linaweza kukugharimu.

Alitoa pongezi kwa wananchi wote wa Zanzibar kwa hamasa waliyoionyesha na kwa kuiunga mkono timu hiyo wakati wote wa mashindano, lakini akieleza kufurahishwa kwa heshima na nidhamu ya hali ya juu iliyoonyeshwa na wachezaji hao jambo ambalo limelinda sifa ya watu wa Zanzibar.

Dk. Shein aliendelea kueleza kuwa ana matumaini makubwa na ubora wa timu ya Zanzibar Heroes pamoja na viongozi na mwalimu wa timu hiyo. Hemed Morocco na ndio maana kwa mara nyingine aliamua kuwaalika Ikulu ili wafarijike na kupata chakula cha mchana pamoja.

Zanzibar Heroes ilitolewa katika hatua ya makundi ya michuano hiyo inayoandaliwa na Baraza la Vyama vya Soka Afrika Mashariki na Kati (Cecafa) inayofikia tamati leo nchini Uganda kwa wenyeji hao kucheza fainali na Eritrea, huku Kilimanjaro Stars ikivaana na Kenya kusaka nafasi ya tatu.



Rais wa Zanzibar, Dk. Ali Mohamed Shein akimzawadia Kocha wa Z'bar Heroes, Hemed Morocco. **PICHA: HAWA ABDALLAH**



Baadhi ya wafanyakazi wa Benki ya Biashara ya DCB, walioshiriki mbio za Familia Marathon wakionyesha medali zao baada ya mbio hizo kumalizika na kutunukiwa katika viwanja vya Chumvi, Bahari Beach jijini Dar es Salaam hivi karibuni. **NA MPIGAPICHA WETU**

# Azam yamtema Ndikumana, yamfunga Kipagwile

**Na Mwandishi Wetu**

KLABU ya Azam imemwongezea mkataba mpya wa miaka miwili winga wake, Idd Kipagwile huku ikifikia makubaliano ya pande mbili ya kuachana na mshambuliaji Suleiman Ndikumana, imeelezwa.

Ndikumana aliyejiunga na Azam FC kwenye dirisha lililopita la usajili Juni mwaka huu, ameamua kuondoka ili kwenda kusaka changamoto mpya kwingineko na kuendeleza kipaji chake, baada ya kukosa kupata nafasi ipasavyo ndani ya kikosi hicho.

"Tunapenda kumtakia kila la kheri katika maisha yake mapya ya soka popote aendako," ilieleza taarifa ya Azam FC.

Kwa upande wa Kipagwile anayesifika kwa mashuti, kuchachafya mabeki kwa kasi yake uwanjani, taarifa hiyo ilieleza ataendelea kubaki kutoa huduma yake ndani ya Azam Complex hadi mwaka 2022. Winga huyo anakuwa mchezaji wa pili kuongeza mkataba ndani ya kipindi hiki cha usajili wa dirisha dogo, baada ya kipa Mwadini Ally aliyeongeza mkataba wa mwaka mmoja awali.

Kipagwile alisaini mkataba wake mpya juzi, Jumanne mbele ya Ofisa Mtendaji Mkuu wa Azam FC, Abdulkarim Amin 'Popat' baada ya Mwadini kumwaga wino wa kusalia hapo Azam Complex hadi Julai 2021.

Mwadini ambaye alijiunga na Azam FC mwaka 2011 akitokea Mafunzo ya Zanzibar, amekuwa akiwania nafasi ya kuanza sambamba na Mghana Razack Abalora pamoja na Benedict Haule.

# Michezo

Alhamisi Desemba 19, 2019
Nipashe




Ronaldo kustaafia Juventus- Mendes HABARI UK.30



Katibu Mkuu wa Yanga, David Luhago (kulia) na beki mpya wa klabu hiyo, Adeyun Ahmad Saleh wakionyesha mkataba baada ya mchezaji huyo aliyesajiliwa akitokea JKT Tanzania kutia saini ya kuitumikia kwa miaka miwili kufuatia kung'ara kwenye michuano ya Kombe la Mataifa ya Afrika Mashariki na Kati (Cecafa), nchini Uganda. **NA MPIGAPICHA WETU**

## Karia sasa Rais mpya wa Cecafa

**Na Somoe Ng'itu,** KAMPALA

RAIS wa Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), Wallace Karia, amechaguliwa kuwa Rais mpya wa Baraza la Soka Afrika Mashariki na Kati (Cecafa), ambalo lilifanya mkutano wake mkuu wa mwaka jana jijini hapa.



Hata hivyo, Karia, ambaye alikuwa mgombea pekee katika nafasi hiyo, hakupigiwa kura, bali alipitishwa rasmi na wajumbe wa baraza hilo ambalo ni marais wa nchi wanachama wa Cecafa.

Mbali na Karia, viongozi wengine waliopitishwa ni Francis Amin wa Sudan Kusini ambaye amekuwa Makamu wa Kwanza wa Rais na Essaya Taaji wa Ethiopia, ametangazwa kuwa Makamu wa Pili wa Rais wa baraza hilo.

Karia ambaye amerithi mikoba iliyowahi kushikwa na Mwenyekiti wa Baraza la Michezo Tanzania (BMT) na Rais wa zamani wa TFF, Leodegar Tenga, atakaa madarakani kwa miaka minne.

Nafasi tatu za wajumbe wa Kamati ya Utendaji zitajulikana katika mkutano mwingine wa mwaka wa baraza hilo.

Karia na safu yake itakuwa na Katibu Mkuu mpya mwakani kufuatia Nicholas Musonye kutangaza kuachia ngazi katika nafasi hiyo na kuhamia kwenye siasa.

# Nchimbi azua utata kusajiliwa Yanga

**Na Mwandishi Wetu**

## ●●● Polisi Tanzania yaigomea Azam FC, yadai bado ana mkataba halali, huko Jangwani wamtangaza Adeyun...

IKIWA ni siku moja baada ya Azam FC kutangaza kumalizana na Yanga iliyomsajili mshambuliaji wao, Ditram Nchimbi anayeichezea kwa mkopo Polisi Tanzania ya Kilimanjaro, utata mpya umeibuka huku 'Walinda Usalama' hao wa nchi wakieleza straika huyo bado ni mali yao.

**Juzi Msemaji wa Azam FC, Jaffari Maganga, alisema uongozi wa Azam FC tayari umemalizana na Yanga ambayo ilituma maombi ya kumsajili Nchimbi na kwamba wameshapokea dau la Wanajangwani hao baada ya kufikia makubaliano.**

Hata hivyo, jana Ofisa Habari wa Polisi Tanzania, Frank Lukwaro, alimwambia mwandishi wetu kuwa bado Nchimbi, ambaye ni mchezaji wa kwanza kufunga hat-trick msimu huu, ni mali yao kwa kuwa wana mkataba na mchezaji huyo wa kuichezea klabu yao kwa mkopo akitokea Azam hadi mwishoni mwa msimu.

"Ni kweli tulimsajili Nchimbi kwa mkopo kwa kipindi cha msimu mzima na hakuna kipengele katika mkataba wake kinachoeleza kwamba anaweza kukatiza mkataba wake katikati ya msimu na kurudi Azam ama klabu hiyo kuamua kumuuza, hivyo hatutambui kuhusu kuuzwa Yanga.

"Tumewekeza sana kwa Nchimbi na ndiyo maana Yanga ikaweza kumuona kutokana na sisi kumtengeneza na kumpa nafasi, kama wanamtaka waje mezani tuzungumze maana tutahitaji mchezaji mwingine wa kuziba pengo lake," alisema Lukwaro.

Na alipoulizwa hukusu madai hayo ya Polisi Tanzania, Ofisa Habari wa Azam FC, Maganga alisema Azam ni klabu kubwa na haiwezi kufanya mambo kienyeji na kwamba taratibu zote zimefuatwa kabla ya kufikia makubaliano ya kumuuza Nchimbi kwa Yanga, aliyoifunga hat-trick wakati wakitoka sare ya mabao 3-3 msimu huu.

"Unapompa mtoto wako mtu akusaidie kulea, siku ukimtaka anakataaje kukurudishia? Sisi tulifuata taratibu zote, hasa kwa kutoa kipaumbele kwanza kwa Polisi Tanzania kwa kuwaeleza kama wanamtaka Nchimbi tuwauzie.

"Tuliwaeleza dau tunalohitaji na ambalo Yanga ilikuwa tayari kulitoa, lakini walitueleza hawana huwezo huo, hivyo tunaweza kuendelea na taratibu nyingine [za kumuuza], ndipo tukamalizana na Yanga.

"Huyo anayedai kuwa hawakupewa taarifa, sisi tuna mawasiliano yote ya barua tulizokuwa tukiwasiliana na mtendaji mkuu wa Polisi Tanzania, hivyo awasiliane naye kwanza," alisema Maganga.

Katika hatua nyingine Klabu ya Yanga imemsajili beki wa JKT Tanzania, Adeyun Saleh Ahmad kwa mkataba wa miaka miwili.

Akizungumza baada ya Adeyun kumwaga wino jana, Katibu Mkuu wa Yanga, David Luhago alisema: "Huo ni mwendelezo wa usajili wenye lengo la kuziba nafasi zilizo wazi na ambao tuliahidi kuufanya kwa ajili ya kukiboresha zaidi kikosi chetu."

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P

9 770856 541002 >